MALALAMIKO YA QUR'ANI TUKUFU

Huu ni mfululizo wa mihadhara aliyo itoa Ayatollah, sheikh Muhammad Yaqoobi (Allah amhifadhi) kwa wanafunzi wa vyuo vya kidini (hawzatul ilmiyah) katika mji wa Najaf, kwa mnasaba wa kuingia mwaka mpya wa masomo ulioanza tarehe 19 mfungo nne 1422 Hijiria, sawa na 14/04/2001.

بسم الله الرحمن الرحيم

وَيَوْمَ تَشَقَّقُ السَّمَاء بِالْغَمَامِ وَنُزِّلَ الْمَلائِكَةُ تَنزِيلاً، الْمُلْكُ يَوْمَئِذٍ الْحَقُّ لِلرَّحْمَنِ وَكَانَ يَوْماً عَلَى الْكَافِرِينَ عَسِيراً، وَيَوْمَ يَعَضُّ الظَّالِمُ عَلَى يَدَيْهِ يَقُولُ يَا لَيْتَنِي اتَّخَذْتُ مَعَ الرَّسُولِ سَبِيلاً، يَا وَيْلَتَى لَيْتَنِي لَمْ أَتَّخِذْ فُلاناً خَلِيلاً، لَقَدْ أَضَلَّنِي عَنِ الذِّكْرِ بَعْدَ إِذْ جَاءنِي وَكَانَ الشَّيْطَانُ لِلإِنسان خَذُولاً، وَقَالَ الرَّسُولُ يَا رَبِّ إِنَّ قَوْمِي اتَّخَذُوا هَذَا الْقُرْآنَ مَهْجُوراً، وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوّاً مِّنَ الْمُجْرِمِينَ وَكَفَى بِرَبِّكَ هَادِياً وَنَصِيراً، وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْلا نُزِّلَ عَلَيْهِ الْقُرْآنُ جُمْلَةً وَاحِدَةً كَذَلِكَ لِنُثَبِّتَ بِهِ فُؤَادَكَ وَرَتَّلْنَاهُ تَرْتِيلاً، وَلا يَأْتُونَكَ بِمَثَلٍ إِلا جِئْنَاكَ بِالْحَقِّ وَأَحْسَنَ تَفْسِيراً.

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

“Na siku zitapo funguka mbingu kwa mawingu, na wateremshwe malaika kwa wingi, ufalme wa haki siku hiyo utakuwa wa Arrahman, Mwingi wa rehema, na itakuwa siku ngumu kwa makafiri. Na siku ambayo mwenye kudhulumu atajiuma mikono yake, na huku anasema: Laiti ningeli shika njia pamoja na Mtume! Ee ole wangu! Laiti nisingeli mfanya fulani kuwa rafiki! Amenipoteza, nikaacha ukumbusho, baada ya kwisha nijia, na kweli Shet'ani ni khaini kwa mwanaadamu. Na Mtume alikuwa akisema: Ee Mola wangu Mlezi! Hakika watu wangu wameifanya hii Qur'ani ni kihame. Na vivi hivi tumemfanyia kila Nabii adui miongoni mwa wakosefu, na Mola wako Mlezi anatosha kuwa Mwenye kuongoa na Mwenye kunusuru. Na wakasema walio kufuru: Kwa nini hakuteremshiwa Qur'ani kwa jumla moja? Hayo ni hivyo ili tuuthibitishe moyo wako, na ndio tumeisoma kwa mafungu.Wala hawatakuletea mfano wowote, ila na Sisi tutakuletea (jawabu) kwa haki, na tafsiri iliyo bora”[1].

[1] Surat Al-Furqan: 25-33.

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

Kila sifa jema ni za Mwenyezi Mungu na yeye ndie msitahiki wa sifa hizo, na sala za Mwenyezi Mungu na amani kemukemu zimuendee mjumbe wake Muhammad (s.a.w.w) na maimamu watakasifu watokanao na kizazi chake.

[رَبِّ اشْرَحْ لِي صَدْرِي، وَيَسِّرْ لِي أَمْرِي، وَاحْلُلْ عُقْدَةً مِّن لِّسَانِي، يَفْقَهُوا قَوْلِي]

(Ewe Mola wangu Mlezi! nikunjulie kifua changu, unirahisishie jambo langu, unifungulie fundo lililoko katika ulimi wangu, wapate kufahamu maneno yangu)[٢] .

UFUNGUZI

Watu wamezoea kufungua vikao, mikutano, makongamano, na vipindi vya redio na televisheni kwa kusoma aya za Qur'ani tukufu lengo likiwa ni kutaka baraka na kuzitukuza aya hizo. Ada hii imekuwa ikifanywa hata nawasio kuwa waislam, jambo linaloonyesha haiba ya kitabu hiki katika nyoyo za maadui na wapinzani wake. Basi ni uzuri ulioje na sisi wanahauza (wanafunzi wa masomo ya dini) tukawa tukifungua masomo yetu kwa Qur'ani tukufu, na yapaswa ufunguzi wetu uwe wenye ufahamu na unaoendana na roho ya Qur'ani, madhumuni na maana zake, na usiwe ni ufunguzi wa kimaoyesho, mfano wa nyimbo na kaswida za kidini au ikiwa ni mfano wa kinga na hirizi.

MALALAMIKO YA QUR'ANI

Nimekusudia nianze kwa kusoma hadithi ilinukuliwa katika kitabu cha Al-kafi na Al-khiswar kutoka kwa Abu Abdillah (a.s) alisema:

(ثلاثة يشكون إلى الله عز وجل مسجد خراب لا يصلي فيه أهله وعالم بين جهّال ومصحف معلّق قد وقع عليه الغبار لا يُقرأ فيه)

[٢]. Surat Taha: 25-28.

(Vitu vitatu, vitamlalamikia Mwenyezi Mungu:

١. Msikiti ulioachwa na usio na mtu ajae kusali humo.
٢. Aalimu (msomi) aliye miongoni mwa wasiojua dini, na
٣. Qur'ani tukufu iliyowekwa mahali ambapo hakuna mtu wa kuisoma na ikabakia katika hali ya kujaa mavumbi.)[٣]

Na Ahlul bayt wa mtume (a.s), hasahasa imamu wa zama hizi na alieshikilia madaraka kwa sasa (a.t.f) ni mifano iliyo wazi ya aalimu. Hivyo, vitu vitatu vitakavyomlalamikia Mwenyezi Mungu vitakuwa ni: Qur'ani, Ahlul bayt na msikiti, na kuna riwaya nyingine ilipokelewa kutoka kwa bwana mtume (s.a.w.w) ikionyesha maana hii pia, alisema:

(يجيء يوم القيامة ثلاثة يشكون: المصحف والمسجد والعترة يقول المصحف يا ربّ حرّفوني ومزّقوني، ويقول المسجد: يا رب عطّلوني وضيّعوني وتقول العترة يا رب قتلونا وطردونا وشردونا، فأجثو للركبتين في الخصومة فيقول الله عز وجل لي: أنا أولى بذلك منك)

"Vitu vitatu siku ya kiyama vitakuja hali ya kuwa vikimlalamikia Mwenyezi Mungu: Qur'ani, msikiti na Ahlul bayt. Qur'ani itasema: Ewe Mola wangu mlezi! Walinipotosha na wakaniacha, na msikiti utasema: Ewe Mola wangu mlezi! Walinifunga na wakanipoteza, kisha Ahlul bayt wanasema: Ewe Mola wetu mlezi! Walituuwa, walitufukuza na walitutimua katika miji yao, kisha nitakaa kwa magoti yangu (ili kutatua) mgogoro, Mwenyezi Mungu ataniambia: Mimi ndiye ninayesitahiki kuliko wewe katika hili"[٤].

Kutokana na hadithi hii tunajifunza mambo kadhaa:

Jambo la kwanza: hakika misingi inayojenga uma wa kiislamu na mihimili ya uwepo wa jamii ya kiislamu ni haya matatu yaliyotajwa ndio maana yametiliwa manani. Hivyo, kwa msingi huu hadithi hii itakuwa na maana sawa ile hadithi maarufu ya thaqalaini (vizito viwili) isemayo:

---

[٣] Al-kaafi: kitabu fadhlil Qur'an, babu qiraatil Qur'ani fil mushaf, hadithi:3, na Al-khiswal: 1/142 abwabu thalatha.

[٤] Wasailus Shi'a: kitabu salat, abwabu ahkamil masajid, babu:5, hadith:2.

(إني تارك فيكم الثقلين كتاب الله وعترتي أهل بيتي ما إن تمسكتم بهما لن تضلوا بعدي أبداً وقد نبأني اللطيف الخبير أنهما لن يفترقا حتى يردا علي الحوض يوم القيامة)

‘‘Mimi ninaacha kati yenu vizito viwili, Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi change, ikiwa mtashikamana navyo, kamwe hamtapotea baada yangu, naye mwingi wa huruma aliyemjuzi wa yote amenijulisha kwamba havitotengana kamwe mpaka vitakaponijia kwenye hodhi (ya kauthar) siku ya kiyama’’[٥].

Qur’ani na Ahlulbayt ni viwili kati ya vile vitu vitatu vitakavyomlalamikia Mwenyezi Mungu, na cha tatu ni msikiti ambao ndio sehemu Qur’ani na Ahlulbayt hutekelezea majukumu yao katika jamii kwani vyote huhusiana na uma kupitia nyanja mbalimbali za msikiti.

Jambo la pili: Kuujulisha uma kwamba utapuzia na kuipa mgongo mihimili hii mitatu, hivyo bwana mtume (s.a.w.w) alielezea malalamiko haya ikiwa ndio ukweli na uhalisia uliopo, na hivyo kuutahadharisha uma na msiba huu wa kuipuzia mihiili hii, na akaonyesha adhabu ya jambo hilo na ukubwa wake pale alipofanya Mwenyezi Mungu kuwa ndio mwenye haki yake iliyopotea, na wakati huohuo yeye ndio hakimu mwadilifu.

Na kwakuwa mihimili hii mitatu ndio misingi ya uwepo wa Uislamu, kuipuuza na kuipa mgongo maana yake ni kutoweka kwa Uislamu na kumalizika kabisa. Ndio maana ikiwa ni wajibu wetu kuudurusu kila muhimili kivyake ili kubainisha athari yake katika maisha ya uma wa kiislamu, kuelezea hasara kubwa itokanayo na kuupa mgongo kila muhimili na kuzungumzia njia zitakazoweza kuhuisha nafasi yake chanya katika maisha ya waislamu.

Hivyo, nimeona ni wajibu wangu nijichague ili kuwasilisha malalamiko na mashitaka haya matatu nikianza na lalamiko na shitaka la kizito kikubwa zaidi ambacho ni Qur’ani:

[٥]Hadithi hii imenukuliwa na vitabu vya kisuni na vile vya kishia, kwa maelezo zaidi rejea kitabu cha (Almuraja’t) cha Sayyed Abdulhuseini Sharafud Diin Almusawi.

Qur'ani tukufu ndio kamba iliyonyoshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu hadi kwa waja wake, na yafuatayo ni malalamiko atakayofikisha mtume (s.a.w.w) siku ya kiyama mbele ya Mwenyezi Mungu pale atakaposema:

[وَقَالَ الرَّسُولُ يَا رَبِّ إِنَّ قَوْمِي اتَّخَذُوا هَذَا الْقُرْآنَ مَهْجُورًا]

''Na mtume alikuwa akisema: Ewe Mola wangu mlezi! Hakika watu wangu wameifanya Qur'ani hii yenyekuhamwa''[٦], na akawatahadharisha waislamu na hatari hii pindi alipowaeleza sababu ya kupotoka kwa umati zilizopita, sababu ambayo ni kuyaacha waliyotelemshiwa na Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu anasema:

[قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ لَسْتُمْ عَلَى شَيْءٍ حَتَّى تُقِيمُواْ التَّوْرَاةَ وَالإِنجِيلَ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْكُم مِّن رَّبِّكُمْ]

''Sema: Enyi watu wa kitabu! Hamna lenu jambo mpaka muishike Taurati na Injili na yote mliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wenu mlezi''[٧]. Hivyo, yeyote atakaye shikamana na yaliteremshwa na Mwenyezi Mungu, kwa hakika atakuwa kafuata njia imfikishayo kwake na atakaye yaacha na kujitenga nao atakuwa ameangamia na kuhiliki.

Na chanzo cha mashtaka na malalamiko haya ya bwana mtume (s.a.w.w) ni jamii zetu za kiislamu[٨] kupuzia usomaji wa Qur'ani, kuipa umuhimu na kutafakari aya zake, achilia mbali kuipa hadhi ya kuongoza katika maisha ili iwe ndio kigezo na muongozo unafuatwa na wenyekutaka kuongoka katika nyanja zote za maisha, mpaka imefikia hatua Qur'ani inasahaulika katika jamii za kiislamu, haikumbukwi isipokuwa kidogo katika mwezi mtukufu wa Ramadhani, hata huko kuikimbuka

---

٦. Surat Al-Furqaan: 30.

٧. Surat Al-Maidah: 8.

٨. Nimechunguza idadi kadhaa ya sampuli za watu waliochaguliwa, walikuwa ni miongoni mwa wanafunzi wa mwanzo kukubaliwa katika shule za kidini (hawza za kielimu), ili kujua namna wanavyoipenda Qur'ani, kwani makadirio ni kwamba, hawa ndio wanaoshika nafasi za juu katika ufahamu wa mambo ya dini na katika imani, kiasi kwamba ufahamu na Imani zao zimewasukuma kuchangua njia hii, lakini (lakushangaza) nimekuta baadhi yao hawajawahi kuhitimisha Qur'ani hata mara moja –wakati wao ndio watu wa mimbari-! Na wengine wamehitimisha mara mbili tu maishani mwao! Na wengine husoma sura tofauti totauti wawapo kwenye minasaba ya kidini. Haya ni kwa upande wa kusoma Qur'ani tu, achilia mbali kuifahamu na kuelewa mana ya aya zake na kutafakari juu ya mafunzo na madhumuni yake. Ikiwa upande ule ni shida, basi upande huu kutofahamu kwao ni zaidi.

na kuitilia manani ndani ya mwezi wa Ramadhani, ni kwa sababu ya mahusiano makubwa yaliyopo baina na Qur'ani na mwezi mtukufu wa Ramadhani, kwani imepokelewa hadithi kutoka kwa bwana mtume (s.a.w.w) kwamba:

(إن لكل شيء ربيعاً وربيع القرآن شهر رمضان)[٩]

''Hakika kila kitu kina msimu, na msimu wa Qur'ani ni mwezi wa Ramadhani''[١] , lakini hii haimanishi kuipuuza na kuipa mgongo au kupunguza kuisoma ndani miezi mingine.

KUJIWEKA MBALI NA QUR'ANI NDIO SABABU YA KUFELI WAISLAMU

Uchaguzi wa hadithi izungumzayo kunako malalamiko haya haukufanyika bila sababu au kwa fikra za kianasa, bali umetokana na ufahamu na muono wa mbali katika kuuchambua uhalisia wa waislamu na hali waliyofikia, kiasi kwamba wamefikia kuzitoa nafsi zao zikiwa kwenye sahani za dhahabu, kwa maadui wao ambao ni ibilisi na nafsi inayo amrisha maovu, iliyoandaliwa na makafiri wakimagharibi ambayo wanajitahidi wakati wote kuwaondolea waislamu heshima, sharafu na utukufu wao ambao ni kitabu kitakatifu cha Qur'ani, hadi imefikia hatua leo hii Qur'ani imekuwa ngeni kwao ،jambo ambalo limesababisha maumivu ya moyo wangu.

Sababu kuu ya kufeli, kudhoofika na kusambaratika Waislamu ni kuipa mgongo kamba ya Mwenyezi Mungu na kutoshikamana nayo, kamba aliyowaamuru kushikamana nayo pale aliposema:

[وَاعْتَصِمُواْ بِحَبْلِ اللهِ جَمِيعاً وَلاَ تَفَرَّقُواْ]

---

٩ :

١ :''Ma'anil Akhbaar: sheikh Swadooq, uk: 226.

"Na shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu wala msifarakane"[١١] , kisha bwana mtume (s.a.w.w) akabainisha makusudio ya kamba hiyo aliposema:

(وإني مخلف فيكم الثقلين: الثقل الأكبر القرآن والثقل الأصغر عترتي أهل بيتي هما حبل الله ممدود بينكم وبين الله عز وجل ما إن تمسكتم به لم تضلوا، . . . الحديث).

"Mimi ni mwenye kukuachieni vizito viwili: kizito kikubwa ni Qur'ani na kizito kidogo ni kizazi na ahlul-bayt wangu, viwili hivyo ndio kamba ya Mwenyezi Mungu baina yenu na Mwenyezi Mungu, iwapo mtashikamana nayo hamtapotea, ..."[١٢] .

KUWAACHA AHLUL-BAYT (A.S) NI KUTOSHIKAMANA NA QUR'ANI

Kwa bahati mbaya umma wa kiislamu ulikiacha kitabu cha Mwenyezi Mungu na ukajitenga nacho mbali pale ulipowaengua Ahlul-bayt kwenye nafasi yao ambayo Mwenyezi Mungu aliwachagulia, kwa kuwa ni jambo lisilowezekana kuvitenganisha viwili hivyo. Ambapo, kwa kuwaondoa Ahlul-bayt kwenye nafasi yao, waliacha na kuipinga kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

[وَرَبُّكَ يَخْلُقُ مَا يَشَاء وَيَخْتَارُ مَا كَانَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ]

"Na Mola wako Mlezi huumba na huteuwa atakavyo. Viumbe hawana khiari"[١٣] .

Kama ni kauli mbovu, ushawishi wa shetani na matamanio mabaya yatokanayo na nafsi inayo amrisha uovu maneno ya anayesema: "Kinatutosha kitabu cha Mwenyezi Mungu", maneno ambayo bado yanakaririwa na kupitishwa na shetani kwenye ulimi wa kila anayetaka kubomoa Uislamu, kuanzia kwenye misingi na mihimili yake, Qur'ani ikiwa ni moja ya misingi hiyo, kwa madai eti

---

[١١] Suurat Aal Imran:103.

[١٢] Biharul Anwaar: 92/102.

[١٣] Suuratul Qasas: 68.

Qur'ani hiyo inamtosha, wakati anatambua wazi kabisa kwamba, Qur'ani haiwezi kutekeleza jukumu lake la hidaya la (uongofu) isipokuwa itakaposimimwa na msimamizi wenye ufahamu wa hukumu na mafunzo yake, msimamizi ambaye si mwingine isipokuwa Ahlul-bayt na kizazi kitakatifu cha bwana mtume (s.a.w.w).

Ukweli ni kuwa fitina hii ya kutenganisha Qur'ani na msemaji wake (msimamizi wake) ina historia ndefu, na Amiirul muumina Ali (a.s) ni miongoni mwa waliopatwa na fitina hii, pale alipolazimishwa usuluhishi na Muawiya na Qur'ani kufanywa ndio hakimu baina yao, hapo ndipo Amiirul muumina (a.s) aliposema:

(هذا القرآن إنما هو خط مستور بين الدفتين لا ينطق بلسان ولا بد له من ترجمان وإنما ينطق عنه الرجال)

"Hakika Qur'ani hii ni maandishi yaliyo andikwa kwenye karatasi, haiongei kwa ulimi na inahitaji wakuifasiri na wanaoitafsiri ni watu waliyo ifahamu"[١] .

Hivyo, Qur'ani na Ahlul-bayt (a.s) ni mihimili miwili isiyo achana wala kutengana, na haiwezekani kudai eti nimeshikamana na kimoja hali yakuwa kingine umekitelekeza. Hakika Ahlul-bayt ndio ule mlango wa Mwenyezi Mungu ambao haiwezekani kuingia kwake isipokuwa kupitia mlango huo, na Mwenyezi Mungu ametuamuru tusiingie kwenye majumba isipokuwa kwa kupitia kwenye milango yake.

Kwa minajili hiyo, madai ya wapinzani wetu kuwa wao ndio wenye kuipa umuhimu Qur'ani zaidi yetu, ni madai batili na yasio na msingi kabisa. Ni kweli kwamba wao wamejishulisha na utamkaji wa herufi zake, kuipendezesha sauti kiasi hadi ikafikia kama wanaimba waisomapo, na kuhifadhi kanuni na hukumu za tajuwidi walizoweka wenyewe, ambapo baadhi ya kanuni hizo hupingana na hukumu ya dini, lakini kutilia umuhimu vyote hivyo ni marembo tu, jambo la muhimu zaidi ni kufahamu na kuelewa malengo na madhumuni ya Qur'ani na kuyafanyia kazi, kwa sababu neno ni vazi la maana na maana ndio kiini cha lengo, na msemaji huwa haliangalii neno kama lenyewe, bali kuliangalia kama chombo

[١] Nahajul Balaghah, hotuba:125.

cha kubebea maana na zana ya kufikishia maana ile kwa hadhira, hivyo maana ndio lengo na kusudio halisi la msemaji.

Zimepokewa hadithi nyingi zikiwalaumu wenye kung'ang'ania matamshi ya Qur'ani na herufi zake hali ya kuwa wanapoteza maana na hukumu zake. Imekuja katika hadithi maarufu kwamba:

(كم من قارئ للقرآن والقرآن يلعنه)

"Ni wasomaji wangapi Qur'ani wanaoisoma huku ikiwalaani!",[١٥]

Wakati huyo msomaji huwa ni mpinzani wa Qur'ani, kwa sababu hatendi kwa mujibu wa mafundisho yake. Na hadithi nyingine kutoka kwa Abu Ja'fari alisema:

(قرّاء القرآن ثلاثة: رجل قرأ القرآن فاتخذه بضاعة واستدر به الملوك واستطال به على الناس فذاك من أهل النار، ورجل قرأ القرآن فحفظ حروفه وضيع حدوده فذاك من أهل النار، ورجل قرأ القرآن فوضع دواء القرآن على داء قلبه فأسهر به ليله وأظمأ به نهاره وقام به في مساجده وتجافى به عن فرشه فبأولئك يدفع الله العزيز الجبار البلاء، وبأولئك يديل الله من الأعداء–أي ينصرهم على الأعداء– وبأولئك ينزل الله الغيث من السماء فوالله هؤلاء قراء القرآن أعز من الكبريت الأحمر) .

"Wasomaji wa Qur'ani wako makundi matatu:

١. Ni wale wanao soma Qur'ani na kuifanya ni mtaji wao, na kupokea ajira kutoka kwa wafalme (watawala) na wanajikweza kwa watu, hawa ni watu wa motoni.
٢. Ni wale watu wanao soma Qur'ani wakahifadhi herufi zake na kupoteza hukumu zake, hawa nao ni watu wa motoni, na
٣. Wengine ni wale wanao soma Qur'ani, wakaifanya Qur'ani kuwa dawa ya maradhi ya mioyo yao, wakasimama usiku kusali kupitia Qur'ani, na wakafunga na kuvumilia kiu ya mchana kupitia Qur'ani, wakasimamisha sala misikini kupitia Qur'ani na wakaachana na magodoro yao kupitia Qur'ani. Mwenyezi Mungu kwa sababu ya watu hawa huondoa mabalaa, hutoa

[١٥] Mustadekul Wasail: ketabu salah, ab'wabu qiraatul qur'an, mlango:7, hadithi:7.

[١٦] Alkhswaar:142.

ushindi dhidi ya maadui na hushusha mvua. Ninamuapa Mwenyezi Mungu kwamba wasomaji hawa ni adimu kupatikana kuliko kibiriti chekundu".

Imekuja katika hadithi yingine kutoka kwa Imamu Hassan (a.s) kwamba:

(وإن أحق الناس بالقرآن من عمل به وإن لم يحفظه وأبعدهم منه من لم يعمل به وإن كان يقرأه)

"Na hakika watu walio karibu zaidi na Qur'ani, ni wale wanaifanyia kazi hata kama hawakuihifadhi (aya zake), walioko mbali zaidi na Qur'ani, ni wale wasio tenda kwa mujibu wa Qur'ani hata kama wanaisoma".[١] ٧

Hivyo, inadhihiri wazi kabisa kwa mkakati wa kutenganisha Qur'ani na Ahlul-bayt (a.s) ili kwa njia hiyo kuikosesha Qur'ani malengo na madhumuni yake na kufanya ushawishi wa kuyapa umuhimu maneno yake tu ni mkakati wenye muda mrefu, na maimamu walio takasika (a.s) walitabahisha wafuasi wao juu ya jambo hilo. Ni umuhimu upi huo inaopewa Qur'ani pale isomwapo kauli yake Mwenyezi Mungu:

[وَرَبُّكَ يَخْلُقُ مَا يَشَاء وَيَخْتَارُ مَا كَانَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ]

"Na Mola wako Mlezi huumba na huteuwa atakavyo. Viumbe hawana khiari"[١] .

Kisha wakaachwa walioteuliwa na Mwenyezi Mungu, na kutangulizwa wasiokuwa wao? ili hali Mwenyezi Mungu kaupa uteuzi wao hadhi sawa na risala nzima ya Uislamu, pale aliposema:

[يَا أَيُّهَا الرَّسُولُ بَلِّغْ مَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِن رَّبِّكَ وَإِن لَّمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَّغْتَ رِسَالَتَهُ واللهُ يَعْصِمُكَ مِنَ النَّاسِ]

"Ewe Mtume! Fikisha uliyo teremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi. Na ikiwa hukufanya hayo basi hukufikisha ujumbe wake. Na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu.[١] " ٩

Ni umuhimu upi huo wanaoipa Qur'ani pale inapopaza sauti ikisema:

---

١٧ Irshadul quloob:79.

١٨ Suratul Qasas: 68.

١٩ Surat Al-Maidah: 67.

[قُل لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً إِلا الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَى]

“Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kwa jamaa zangu wa karibu (Ahlul-bayt wangu)”[٢] ,

ili hali wakifanya uadui kwa watu wa nyumba ya mtume (s.a.w.w), na kuwafuatilia kwa ubaya kila mahali? Laiti wangelikuwa wakiipa umuhmu Qur’ani, wangeliweka aya hiyo pamoja na hii:

[قُلْ مَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ إِلا مَن شَاء أَن يَتَّخِذَ إِلَى رَبِّهِ سَبِيلاً]

“Sema: Sikukuombeni ujira juu yake; ila atakaye na ashike njia iendayo kwa Mola wake Mlezi”[٢] ,

ili wapate ukweli kwamba Ahlul-bayt (a.s), ndio ile njia ambayo Mwenyezi Mungu aliamrisha ifuatwe, ni pale aliposema:

[وَأَنَّ هَذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيماً فَاتَّبِعُوهُ وَلاَ تَتَّبِعُواْ السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِ ذَلِكُمْ وَصَّاكُم بِهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ]

“Na kwa hakika hii ndiyo njia yangu Iliyo nyooka. Basi ifuateni, wala msifuate njia nyingine, zikakutengeni na njia yake. Haya amekuusieni ili mpate kumcha Mungu.”[٢] , na hivyo Imamu Baqir (a.s) alivyoifasiri aya hiyo, akasema:

(نحن السبيل فمن أبى هذه السبل فقد كفر).

“**S**isi ni njia, na yeyote mwenye kupinga njia hizi, atakuwa amekufuru.[٢] ”

Maneno yasemayo: “Kinatutosha kibatu cha Mwenyezi Mungu” na wapambe wa maneno hayo ambao wamekuwa wakiyakariri hadi leo hii na kuhitaji dalili ya kila kitu kutoka ndani ya Qur’ani tu, sisemi wala kuyaita kuwa ni maneno ya haki yenye malengo ya batili (kama wasemavyo wengine), bali hayo ni maneno ya batili yaliyolenga batili. Na wafuasi wa maneno hayo hawataki kingine zaidi ya kubomoa, na kuvunja misingi ya Uislamu kwa madai kuwa Qur’ani inajitosheleza. Kwani

---

[٢] Surat Ash-Shura: 23.

[٢] Surat Al-Furqaan: 57.

[٢] Surat Al-An’aam: 153.

[٢] Behaarul Anwaar: 13/24, mlango: Maimamu ndio njia, wao na wafuasi wao.

madai hayo maaa yake kutokuwa na haja hata ya mtume (s.a.w.w)! ambako kuna manisha kubaki na ujinga wa ufafanuzi wote wa sheria ya Uislamu, kwa sababu mtume (s.a.w.w) na maimamu (a.s) ndio wasimizi wa Qur'ani, wasemaji na wenye kufafanua hukumu zake.

Leo hii angalia elimu zilizo enea ulimweguni, je unaweza ukawa dakitari au muhandisi bila kujifunza kwa wataalamu na wajuzi wa elimu za udakitari na uhandisi? Ikiwa hilo haliwezekani, inakuwaje kupata ujuzi wa Qur'ani? Kitabu ambacho: "kinabainisha kila kitu"[٢٤] na "hakikupuuza wala kuacha chochote"[٢٥] na kuna masilahi ya wanadamu wote katika kila zama: "Mna nini? Mnahukumu vipi nyinyi?". Ndio maana bwana mtume Mohammad (s.a.w.w) akautahadharisha umma wake juu ya hatari hii akisema:

(لا ألفين أحدكم متكئاً على أريكته يأتيه الأمر من أمري مما أمرت به أو نهيت عنه فيقول: لا ندري ما وجدنا في كتاب الله اتبعناه)

"Nisimuone mmoja wenu hali ya kuwa ameegamia kwenye kochi lake, akajiwa na amri miongoni mwa amri nilizo amrisha au katazo nililokatazwa kisha akasema: sijui! Kwa hoja kwamba, sisi tunakubali na kufuata tulichokipata ndani ya Qur'ani.[٢٦] "

Isipokuwa maadui wa Mwenyezi Mungu na wafuasi wa shetani, walitambua wazi kuwa Qur'ani ndio ngome yenye kuulinda umma huu wa Kiisamu kutokana na upotovu, na kwamba Ahlul-bayt (a.s) ndio wasimamizi wa Qur'ani. Na hapo ndipo walipoandaa mkakati wa kuwaweka mbali Ahul-bayt na umma ili ubaki bila mlinzi, na Qur'ani ibaki bila msimamizi, kwa njia hiyo umma ukawa ni windo rahisi kwa maadui wake na kwa wale wanaoutakia mabaya. Bila shaka mwenyewe unauona umma huo ulikofikia, umekuwa ukitikiswa na shub'ha ndogo, ukifeli katika kila fitina na kuanguka mwanzoni mwa kila jaribio. Kuwaacha Ahlul-bayt

---

[٢٤]. Suurat An Nah'l:89.

[٢٥]. Suurat Al-An-a'am:38.

[٢٦]. Al-Mizan fii tafsiril-qur'an: jz: 3, katika bahathi ya riwaya katika aya: 28-32, suurat Al-Imran, akinukuu kutoka kwa: Ahmad, Abuu Daud, Tirmidhii, Ibin Majah, Ibin Habban na wengineo mimongoni wa wanazuoni wa kisuni.

(s.a) ni pigo kubwa lililo ukumba mfumo wa Uislamu, na kusababisha elimu ya Qur'ani na namna ya tafakuri sahihi iliyokuwa ikilinganiwa na Qur'ani kusahaulika na kuachwa. Ushahidi wa hilo upo wazi kabisa, kwani inatosha kulitambua hilo kwa kuangalia uchache wa hadithi zilizo nukuliwa katika vitabu vya hadithi kutoka kwa Ahlul-bayt (a.s), na hasa ukizinagatia hadhi na heshima ya elimu ya hadithi iliyokuwa katika kipinda cha makhalifa, na shauku kubwa ya waliyokuwa nayo katika kupokea hadithi. Unaweza kustaajabu sana pindi unapo hesabu hadithi zilizo pokelewa katika zama hizo kutoka Imamu Ali (a.s), Imamu Hassan (a.s) na Imamu Hussein (a.s) katika uga wa tafsiri ya Qur'ani! Kwa mfano: hauwezi kukuta swahaba alinukuu hadithi kutoka kwa Imamu Ali (a.s)! Ama hadithi zinazohusu Qur'ani walizo nukuu walio kuja baada ya maswahaba (matabiina) kutoka kwake (a.s) zikihesabiwa hazizidi hadithi mia moja, wakati zilizo pokelewa kutoka kwa Imamu Hassan (a.s) hazifiki hata kumi, ama kutoka kwa Imamu Hussein (a.s) hakujapokelewa hadithi yoyote ile! Hivi ndivyo hali ilivyo kwa Ahlul-bayt (a.s), wakati Suyuti katika kitabu chake cha Al-Itqan ametaja kwamba jumla ya hadithi zilipokelewa kuhusu tafsiri ya Qur'ani zinafikia elfu kumi na saba. Hii ni idadi inayotajwa kupitia njia za jamhuri ya wanahadithi peke yao, na ukija kwenye fikihi utakuta hali ni kama hiyo hiyo pia"[٢] .[٧]

Unadhani ipi ilikuwa ni hasara ya Qur'ani baada ya kuwaweka mbali Ahlul-bayt (a.s) na nafasi yao aliyo wachagulia Mwenyezi Mungu? Angalia hasara hizi katika yafuatayo:

١. Kufichikana elimu nyingi za Qur'ani ambazo hawazifahamu isipokuwa Ahlul-bayt (a.s).
٢. Qur'ani kushidwa kutekeleza jukumu lake katika kujenga nafsi na jamii, kwakuwa Qur'ani na Ahlul-bayt (a.s) ni mihili miwili isiyo tengana, hivyo Qur'ani haiwezi kuathiri maisha ya umma wa Kiislamu ispokuwa iwapo mikononi mwa Ahlul-bayt.

---

[٢٧] Al-Mizan fii tafsiril-quran: jz: 5, katiba bahathi ya taarikh, chini ya aya: 15-19 katika suurat Al-Maida.

٣. Qur'ani kuwa windo la maadui, watu wenye tamaa na wenye malengo binafsi. Utawaona kila mmoja akitumia Qur'ani kuthibitisha imani ya madai yake, hata makhawariji nao walikuwa wakitumia Qur'ani katika majadiliano yao na Ibin Abbasi ili kuthibitisha batili yao baada ya tukio la usuluhisho, ndipo Imamu Ali (a.s) alipo mkataza kuhojiana nao kwa kutumia Qur'ani; kwa kuwa ina maana zaidi ya moja[٢٨] , hatimaye maana halisi za Qur'ani zikapotea kwa sababu ya tafsiri ambazo Qur'ani imetahadharisha kuzifuata kwa kusema: ٨

[فَأَمَّا الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ زَيْغٌ فَيَتَّبِعُونَ مَا تَشَابَهَ مِنْهُ ابْتِغَاء الْفِتْنَةِ وَابْتِغَاء تَأْوِيلِهِ]

"Ama wale ambao nyoyoni mwao umo upotovu wanafuata zile za mifano kwa kutafuta fitna, na kutafuta maana yake…", lakini jawabu limetolewa na Qur'ani yeynyewe iliposema:

[وَمَا يَعْلَمُ تَأْوِيلَهُ إِلاَّ اللهُ وَالرَّاسِخُونَ فِي الْعِلْمِ]

"Na wala hapana ajuaye maana yake ila Mwenyezi Mungu na wale wenye msingi madhubuti katika ilimu"[٢٩] . Ahlul-bayt (a.s) ni mfano ulio wazo wa wenye elimu madhubuti.

٤. Umma wa Kiislamu kusambaratika na kufarakana, kwa sababu uhifadhi na msingi wa kuuangana kwake ni Qur'ani na Ahlul-bayt (a.s) kwa mujibu wa bwana mtume (s.a.w.w) alivyoitafsiri kauli yake Mwenyezi Mungu:

[وَاعْتَصِمُواْ بِحَبْلِ اللهِ جَمِيعاً وَلاَ تَفَرَّقُواْ]

"Shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu kwa pamoja na wala msifarakane", Alisema (s.a.w.w) kuwa: kamba hiyo ni Qur'ani na Ahlul-bayt.

Bibi Fatima Zahraa (a.s) naye pia amewazungumzia Ahlul-bayt katika hotuba yake aliyo itoa katika msikiti wa Mtume (s.a.w.w) pale Madina Munawara akisema:

(وجعل إمامتنا نظاما للملة)

---

٢٨. Behar Al-Anwaar: 2/245.

٢٩. Suurat Al-Imran: 7.

“Mwenyezi Mungu kaufanya uongozi wetu kuwa ndio mfumo wa dini”[٣] , kwa maana kwamba kupitia Ahlul-bayt mambo ya waislamu hunyooka na huimarika. Ndio maana matokeo ya jamii ya Kiislamu kuwaweka kando Ahluli-bayt ilimekuwa kuangukia mikononi mwa watawala waovu na watumwa wa matamanio ya nafsi zao, ambao waliitumia Qur’ani hii hii kuteketeza mimea na viumbe, ambapo huambatanishwa nao kila aliyewapigia debe na kutetea vitendo vyao viovu, kama wale walio tumia kauli ya Mwenyezi Mungu:

[أَطِيعُواْ اللهَ وَأَطِيعُواْ الرَّسُولَ وَأُوْلِي الأَمْرِ مِنكُمْ]

“Mtiini Mwenyezi Mungu na mumtii Mtume na wenye madaraka katika nyinyi”, kuwafanya hao watawala makafiri na wapotovu, kuwa ndio wenye madaraka na wenye kuwatawala waislamu.

WASIA WA KUHIFADHI QUR’ANI

Yasiwaghuri madai ya wasemao kwamba, wao ndio wenye kuijali zaidi Qur’ani kuliko sisi[٣] . Ninasema: hifadhini Qur’ani kwani inà hadhi ya kuhifadhiwa na kufanyiwa kazi. Kuweni kama alivyo kuusieni Amiirul muunina Ali bin Abi Talib (a.s) kabla ya kufariki kwake kishahidi:

(الله الله بالقرآن لا يسبقكم إلى العمل به غيركم)

“Ninamuapa Mwenyezi Mungu ninamuapa Mwenyezi Mungu kuhusiana na Qur’ani. Asiyekuwa nyinyi asikutangulieni kuifanyia kazi”[٣١]na kama ilivyo katika usia wa mtume (s.a.w.w) kwa Imamu Ali (a.s) akimuusia kuzifanyia kazi hadithi arobaini, alisema:

(وأن تكثر من قراءة القرآن وتعمل بما فيه).

---

[٣] Kashful Ghummah: 2/110.

[٣١] Ninasisitiza sana juu ya nukta hii, kwa kuwa watu wengi wakaiwaida na wasiokuwa na ujuzi wa mambo wamekuwa wakidanganyika na madai ya amna hii, na hivyo kusadikisha kisemwacho kuwa haifani kuamini chochote kisichokuwa na dalili kutoka ndani ya Qur’ani, na hivyo kufutilia mbali ushahidi na dalili ya hadithi!

[٣٢] Behar Al-Anwaar:42/256.

“Na ukithirishe (uzidishe) kuisoma Qur’ani na kuyafanyia kazi yaliyomo ndani yake”[٣] .

QUR’ANI NI NJIA IKUFIKISHAYO KWENYE KUMTAMBUA MWENYEZI MUNGU

Yeyote yule amtakae Mwenyezi Mungu, na akawa anahitaji kufika kwake, ni wajibu wake ashikamane na Qur’ani, kwani jambo la kwanza katika dini ni kumtambua yeye. Imepokelewa kutoka kwa Imamu Swadiq (a.s) kwamba: “Hakika Mwenyezi Mungu amejionyesha kwa viumbe wake kupitia maneno yake (Qur’ani), lakini hawamuoni”[٣] . Na anayetaka kujenga na kutakasa nafsi kutokana na maradhi yake mbali mbali, ni wajibu wake pia ashikamane na Qur’ani. Hali kadhalika, mwenye kutaka ustawi wa jamii yake na kuisimamisha kwa misingi ya amani, furaha na utulivu, naye pia analazimika kuishikilia Qur’ani. Kwa sababu Qur’ani ndio njia ya uongofu na kiongozi wa kila heri na wema.

Inastaajabisha kuona kwamba kifaa chako kinapo haribika unakichukua kwa aliye kiunda ili akirekebishe, kwa kuwa aliye kitengeza kitu ndio mwenye ujuzi nacho zaidi. Na unapo ugua unaenda kwa daktari bingwa ili akutibu. Lakini unapo taka kurekebisha nafsi ya binadamu iliyo sheheni mambo mengi yaliyo fichikana kwa mwenye nafsi hiyo, achilia mbali asiyekuwa mwenye nayo, au unapo hitaji kuweka nidhamu na mfumo utakao dhamini furaha ya mwanadamu na kumrekebisha, eti unaenda kutafuta hilo kwa mwanadamu huyo huyo mwenye mapungufu na asiye jiweza, badala ya kwenda kwa muumbaji wa mwandamu huyo na mjuzi wa nafsi ya alichokiumba ili akupe muongonzo!

Uzoefu wa Qur’ani katika kujenga nafsi na jamii, ulithibitika kwa bwana mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w). Kwani kuna ulingano mdogo tu, baina ya jamii ya kabla ya Uislamu na ile ya baada ya Uislamu, na mabadiliko makubwa yaliyo patikana kutokea kwenye jamii ya watu waliokuwa nyuma kitamaduni, wakiwa wamesambaratika, na maovu yakiwa yametapakaa baina yao,

---

٣٣. Al-Khesaal: Ab’wabul arbai’na, hadithi:19.

٣٤. A’waalil- Alaalii:4/116.

wakijifakharisha kwa matendo maovu na machafu, mpaka kufikia hatua ya kuwa ni jamii iliyo endelea, yenye tamaduni, maadili mema na nidhamu ambayo haikuwahi wala haitakuja tokea mfano wake kwa jamii iliyojitenga mbali na Mwenyezi Mungu, ndani ya muda mfupi, yote hayo hayakutokea isipokuwa kwa baraka ya kitabu hiki kitukufu, na msimamizi wake mbora wa viumbe.

TUNA HAJA YA KUREJESHA QURANI KWENYE MAISHA YETU

Leo hii tuna haja kubwa sana ya kurejesha ustawi ya Qur'ani kwenye maisha ya waislamu na kuitoa kwenye kutengwa, kiasi kwamba imefikia hatua uwepo wa Qur'ani umekuwa unaishia kwenye hitima zisomwazo kwa ajili ya marehemu na kuifanya kama kinga.

Kumekuwa na msemo usemao kuwa :(Hakika mwisho wa umma huu hautaimarika isipokuwa kwa kile kilicho uimarisha mwanzo), na ni wazi kwamba mwanzo wa umma huu haukuimarika isipokuwa kwa Qur'ani, hivyo jamii ya kiislamu ikitaka kurudi kwenye msitari haina namna zaidi ya kurudi kwenye Qur'ani na kuiweka maishani mwake. Imepokelewa kutoka kwa Miqdad (Mwenyezi Mungu amridhie) kutoka kwa mtume wa Menyezi Mungu (s.a.w.w) aliposema:

(فإذا التبست عليكم الفتن كقطع الليل المظلم فعليكم بالقرآن فإنه شافع مشفع وماحل مصدق ومن جعله أمامه قاده إلى الجنة ومن جعله خلفه ساقه إلى النار وهو الدليل يدل على خير سبيل)

"Itakapo kupateni fitina mfano wa usiku wa giza, basi rudini kwenye Qur'ani (mshikamane nayo), kwani Qur'ani ni mwombezi ambaye uombezi wake utapokelewa, na yenye kutoa taarifa itakayo kubaliwa, mwenye kuiweka mbele yake inamongoza kwenye pepo, na mwenye kuiweka nyuma yake itampeleka motoni, Qur'ani muongozo unao ongoza kwenye njia bora zaidi"[٣] . Na Imamu anasema katika moja ya khutba zake:

(واعلموا أن هذا القرآن هو الناصح الذي لا يغش والهادي الذي لا يضل، والمحدث الذي لا يكذب، وما جالس هذا القرآن أحد إلا قام عنه بزيادة أو نقصان: زيادة في هدى ونقصان من عمى، واعلموا أنه ليس على أحد بعد القرآن من فاقة ولا لأحد

٣٩Al-Kafii: 2/299.

قبل القرآن من غنى فاستشفعوه من أدوائكم واستعينوا به على لأواءكم فإن فيه شفاءً من أكبر الداء وهو الكفر والنفاق والغي والضلال فاسألوا الله عز وجل به وتوجهوا إليه بحبه ولا تسألوا به خلقه إنه ما توجه العباد إلى الله بمثله، واعلموا أنه شافع مشفع وماحل ومصدق وأنه من شفع له القرآن يوم القيامة صدق عليه فإنه ينادي مناد يوم القيامة: (ألا إن كل حارث مبتلى في حرثه وعاقبة عمله غير حرثة القرآن)، فكونوا من حرثته وأتباعه واستدلوه على ربكم واستنصحوه على أنفسكم واتهموا عليه آراءكم واستغشّوا فيه أهواءكم).

"Na tambueni kwamba Qur'ani hii ni mnasihi asiye haini, na kiongozi asiye potosha, na msemaji asiye ongopa, na hakuna aliye kaa na Qur'ani (aliye soma Qur'ani) isipokuwa alipo simama (alipo maliza kuisoma) oungofu wake uliongezeka na upotovu wake ulipungua. Na tambueni kwamba, hakuna muhitaji baada ya kujifunza Qur'ani, na hakuna aliye tosheka kabla ya kujifunza Qur'ani. Basi, yatibuni maradhi yenu (ya dhahiri na yaliyo jificha, ya kiroho na kimwali) kwa Qur'ani, na katika matatizo yenu ombeni msaada kupitia kwayo, kwani ndani yake kuna tiba ya maradhi makubwa zaidi, ambayo ni ukafiri, unafiki na upotofu. Hivyo, muombeni Mwenyezi Mungu kwa Qur'ani na mjielekeze kwake kwa kuipenda, kwani waja hawamwelekei Mwenyezi Mungu kwa chochote kile kama wamuelekeavyo kwa Qur'ani, na kamwe msiombe viumbe wake kwa Qur'ani. Tambueni kuwa Qur'ani ni mwombezi ambaye uombezi utakubaliwa na ni mtoa ripoti anaye sadikiwa, na mwenye kuombewa na Qurani siku ya Kiyama uombezi wake utakubaliwa, kwani siku hiyo mwenye kunadi atanadi kwa kusema: "Tambueni kwamba kila mkulima atatihaniwa kwa kazi yake isipokuwa wakulima wa Qur'ani", hivyo kuweni miongoni mwa wakulima wa Qur'ani na wafuasi wake na ifanyeni kuwa muongozo wa kukupelekeni kwa Mola wenu Mlezi, na muitake nasaha kwa ajili ya usalama wa nafsi zenu, na zituhumuni fikra zenu kwa Qur'ani na matashi yenu mbele yake yahesabuni kuwa ni hiyana"[٣] .

MTUME (s.a.w.w) NA AHLUL–BAYT (a.s) KUIPA UMUHIMU QUR'ANI

Hakika umuhimu utolewao na Ahlul-bayt kwa Qur'ani ni wa hali ya juu sana, kiasi kwamba imefikia hadi Imamu Sajadi (a.s) anasema:

٣. Nahjul balagh, sharhi ya Mohammad Abduhu: 1/347. Khutba: 177.

(لو مات من بين المشرق والمغرب لما استوحشت بعد أن يكون القرآن معي).

''Lau wangalikufa watu wote waliopo baina ya mashariki na magharibi nisingeli ogopa kuwa mpweke maadamu nina Qur'ani''[٣٤] . Na bwana mtume (a.s.w.w) aliamrishwa na Mwenyezi Mungu kuisoma Qur'ani pale aliposema: ٧

[وَرَتِّلِ الْقُرْآنَ تَرْتِيلاً]

''Na soma Qur'ani kwa utaratibu na utungo''[٣٥] , vilevile akamuamuru kufanya maandalizi ya kuibeba Qur'ani kwa kusali sala ya usiku bila kuacha, asema MwenyeziMungu: ٨

[إِنَّا سَنُلْقِي عَلَيْكَ قَوْلاً ثَقِيلاً، إِنَّ نَاشِئَةَ اللَّيْلِ هِيَ أَشَدُّ وَطْئاً وَأَقْوَمُ قِيلاً]

''Hakika sisi tutakuteremshia kauli nzito, hakika kuamka usiku kunafiakiana zaidi na moyo, na maneno yake yanatua zaidi''[٣٦]Kisha bwana mtume (s.a.w.w) hakutosheka na kuisoma Qur'ani tu, bali alikuwa akimtaka Abdullah bin Masoud amsomee Qur'ani, lakini Abdullah akawa anatoa udhuru kwa mtume akisema: ''Ewe mjumbe wa Allah! Hakika Qur'ani imeshuka kwako, sasa unataka uisikie kutoka kwangu''. Kisha bwana mtume (s.a.w.w) akawa akisema: ''Mimi ninapenda kuisikia kutoka kwako''. Hapo ndipo Abdallah alikuwa akisoma Qur'ani huku macho ya bwana mtume (s.a.w.w) yakibubujikwa na machozi. Akitakata kwa kitendo hicho kuviburudisha viungo vyake vyote kwa Qur'ani: macho yake, masikio yake, moyo wake na ulimi wake, kwakuwa alikuwa akitambua kwamba kila kiungo kina njia yake ya kuhamisha elimu na maarifa. Hivyo licha ya mtume (s.a.w.w) kuwa mbora wa viumbe, lakini alitaka kwa njia hiyo zimkamilikie sababu zote za maarifa. Hata imepokelewa hadithi ambayo maana yake ni kwamba: (mweye kukosa moja ya hisia tano, kwa hakika atakuwa amekosa elimu), ndio maana bwana mtume (s.a.w.w) akawa ananufaika na maarifa ya Qur'ani kwa kutumia viungo vyake vyote. Hali kadhalika imepokewa kuwa ni mustahabu (suna) kusoma Qur'ani kwa sauti inayo sikika, ukiachilia mbali fadhila na thawabu zilizo pokelewa kuhusu kunyamaa pindi isomwapo, na kutazama kwenye msahafu hata kama msomaji amehifadhi kile akisomacho, hata kama ni ndani ya sala, kama itakavyokuja katika orodha ya hadithi hapo baadae inshaa Allah.

---

٣٤ Al-Kafii: 2/602.

٣٥ Suurat Al-Muzzammil: 4.

٣٦ Suurat Al-Muzzammil: 5-6.

Mtume (s.a.w.w) alikua akiathirika kwa Qur'ani. Aliwasomea waislamu surat Ar-Rahman hali ya kuwa wamekaa kimya wakimsikiliza, mtume (s.a.w.w) akawaambia: Niliwasomea majini sura hii lakini wakawa ni wasikivu zaidi yenu. Kivipi ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu? Wakauliza. Akasema (s.a.w.w): Kila nilipo soma:

[فَبِأَيِّ آلاء رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ]

"Basi ni ipi katika neema za Mola wenu mlezi mnayo ikanusha?" walikuwa wakisema: Hakuna chochote katika neema za Mola wetu Mlezi tunacho kikanusha. Na alikuwa akisoma kauli yake Mwenyezi Mungu:

[أَلَيْسَ ذَلِكَ بِقَادِرٍ عَلَى أَن يُحْيِيَ الْمَوْتَى]

"Je huyo hakuwa ni muweza wa kufufua wafu?", akisema: Ndio, umetakasika ewe Mwenyezi Mungu. Kwakuwa kupitia aya zile alikuwa akisikia moja kwa moja kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na itakuja huko mbele kwamba Imamu Kadhim (a.s) alikuwa akisoma Qur'ani kana kwamba anamhutubia mwanadamu.

Mtume (s.a.w.w) alimsomea surat Az- Zumar kijana mmoja aliyekuwa na moyo safi na nia njema, alipo fika kwenye aya zifuatazo:

[وَسِيقَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِلَى جَهَنَّمَ زُمَراً]

"Na walio kufuru wataongozwa kuendea Jahannamu kwa makundi" ءna kauli yake Mwenyezi Mungu:

وقوله تعالى:[وَسِيقَ الَّذِينَ اتَّقَوْا رَبَّهُمْ إِلَى الْجَنَّةِ زُمَراً]

"Na walio mcha Mola wao Mlezi wataongozwa kuendea peponi kwa makundi"[٤٠] , alitoa kwikwi kubwa iliyo pelekea kufariki dunia.

Na alisoma surat Al-Insaan wakati imemteremkia akiwa na mtu mmoja mweusi, alipo fika kwenye sifa za pepo, yule mtu alipepesuka mpepesuko ulio sababisha kuiaga dunia, na hapo bwana mtume (s.a.w.w) akasema: Kilichoitoa nafsi ya ndugu

[٤٠] Surat Az-Zumar: 71.

[٤١] Surat Az-Zumar: 73.

yenu ni shauku ya pepo. Hawa ndio wale ambao aya hii tukufu iliwasifu kwa kauli yake Allah (s.w.t):

[الَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ يَتْلُونَهُ حَقَّ تِلاَوَتِهِ أُوْلَئِكَ يُؤْمِنُونَ بِهِ وَمن يَكْفُرْ بِهِ فَأُوْلَئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ]

"Wale tulio wapa kitabu wakakisoma kama ipasavyo kusomwa, hao ndio kweli wanao kiamini. Na wanao kikataa, basi hao ndio wenye kukhasirika"[٤] .

SABABU ZA KUIPA UMUHIMU QUR'ANI

Hakika sababu nyingi zinatusukuma kuipa Qur'ani umuhimu zimedhihiri. Hapa, Mwenyezi Mungu akipenda nitajaribu kuziorodhesha, pamoja na kuongeza nukta mpya tofauti na ulizo zisikia katika aya za Qur'ani na hadithi kama ifuatavyo:

١. Kuipa umuhimu Qur'ani ni tiba kamili na ya uhakika kwa ajili ya maradhi ya binadamu: maradhi ya kinafsi, kijamii, kiroho bali hata yale ya kimwili pia, kama itakavyo kuja katika baadhi ya hadithi.
٢. Mtafuta ukamilifu na furaha yakudumu duniani na akhera– ambalo ndio lengo la juu na mama wa malengo- anahitajia Qur'ani ili kumuongoza kwenye njia sahihi. Na mwanadamu hupanda daraja na kukamilika zaidi kila anavyo nufaika na Qur'ani zaidi.
٣. Kuipa umuhimu Qur'ani ni kumfuata mtume (s.a.w.w) na Ahlul-bayt wake watukufu. Na Mwenyezi Mungu ametuamuru hivyo alipo sema:

[لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُو اللَّهَ وَالْيَوْمَ الآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيراً]

"Hakika nyinyi mnacho kigezo chema kwa mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mugu na siku ya mwisho na akamtaja Mwenyezi Mungu sana"[٤] . [٣]

٤. Qur'ani ni barua na ujumbe wa mpendwa asiye na ukomo. Na mwanadamu huwa hachoki kusoma ujumbe wa mpendwa wake, kuuchunguza kwa kina na kutafakari juu ya maana za maneno yake. Mwenyezi Mungu aliyetukuka ndiye

[٤] Surat Al-Baqarah: 121.

[٣] Surat Al-Ahzab: 21.

mpendwa wa kweli, kwani kila sababu ya kupendwa anayo. Kwa sababu upendo unaweza kusababishwa na ukamilifu na uzuri wa mpendwa, na kwake Mwenyezi Mungu kumejumuika sifa za ukamilifu na majina mazuri. Au sababu ya upendo inaweza kuwa ni fadhila na wema aufanyao mpendwa, na Mwenyezi Mungu ndio mnemeshaji na mwenye kutoa hata kwa wasiostahiki, yeye hutoa hata kwa waja wake waasi:

[وَإِن تَعُدُّواْ نِعْمَةَ اللهِ لاَ تُحْصُوهَا]

"Na mkizihesabu neema za Mwenyezi Mungu hamwezi kuzidhibiti"[٤٤].

Na maana hii imekuja katika hadithi, iliyopokelewa kutoka kwa Imamu Swadiq (a.s), alisema:

(القرآن عهد الله إلى خلقه فقد ينبغي للمرء المسلم أن ينظر في عهده وان يقرأ منه كل يوم خمسين آية).

"Qur'ani ni ahadi ya Mwenyezi Mungu kwa viumbe wake, hivyo yafaa kwa muislamu aiangalie ahadi yake na asome kila siku aya hamsini"[٤٥].

٥. Kuna thawabu nyingi na malipo makubwa yasiyo na ukomo, anayo pewa msoma Qur'ani na mwenye kutafakari katika aya zake, kama tutakavyo soma katika hadithi tukufu panapo majaliwa.

٦. Kwa kuwa Qur'ani ni kitabu hai chenye kudumu kwa ajili ya kila zama na kila sehemu, hivyo mambo iliyo yatolea ufumbuzi, na matatizo iliyo yakabili sio maalumu kwa ajili ya zama fulani. Hivyo, utatuzi tuupatao ndani ya Qur'ani ni utatuzi wa kudumu na endelevu unaofaa kutatua matatizo mapya, na tutataja mifano mingi katika uchunguzi huu. Kama vile: suala la kulinganisha baina ya ujahilia wa kale na ujahilia mpya au ujahilia mambo leo. Ipo hadithi iliyo pokelewa kutoka kwa Harithi Al-a'war, alisema: Niliingia msikitini mara nikawakuta watu wameshughilishwa na mazungumzo (yasiyo husiana na msikiti), nikaenda kwa Imamu Ali (a.s) nikamwambia: Je, huoni kwamba watu wanashughulishwa na mazungumzo msikitini? Wamefanya hivyo? Akauliza Imamu. Nikasema: Ndio. Imamu akasema: Kwa hakika nimemsikia mjumbe

[٤٤] Surat An-Nahl: 18.

[٤٥] Al-Kafii: 2/609.

wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) akisema: Itatokea fitina, nikamuuliza: Ni ipi njia ya kutoka katika fitina hiyo? Akasema: Kitabu cha Mwenyezi Mungu, Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Ndani yake kuna habari za waliokuwa kabla yenu na watakuja baada yenu na kuna hukumu za yaliyo baina yenu. Qur'ani ni upambanuo wa haki na batili na ndani yake hakuna mzaha. Dhalimu atakae ipa mgonga Mwenyezi Mungu atamuangamiza, na yeyote atakae tafuta uongofu kwengine Mwenyezi Mungu atampoteza. Yenyewe ni kamba ya Mwenyezi Mungu madhubuti, nayo ni ukumbusho wenye hekima na njia iliyo nyooka..."[٤٦].

٧. Tunajifunza maarifa, elimu mbali mbali na siri zilizo hifadhiwa ndani yake. Kiasi kwamba mtu kama Imamu Ali (a.s) ambaye Ibin Abbasi anayejulikana kama kamba ya Umma na mfasiri wa Qur'ani, anasifia elimu kwakusema: "Elimu yangu na elimu ya masahaba wa mtume (s.a.w.w) si chochote ikilinganishwa na elimu ya Ali (a.s) isipokuwa ni kama tone la maji baharini". Imamu Ali (a.s) na wingi wa elimu yake, alipo ulizwa: Je una elimu yoyote itokanayo na wahyi (ufunuo)? Alisema: Hapana. Ninamuapa ambaye aliye otesha mmea na akaumba mwandamu, hafahamu elimu yoyote itokanayo na wahyi (ufunuo), isipokuwa mja aliye pewa na Mwenyezi Mungu ufahamu wa kitabu chake"[٤٧].

Ndani ya kitabu hiki cha Qur'ani kuna kila mahitaji. Kuna itikadi sahihi, maadili mema, sheria zenye hekima na busara, nukta za kibalagha na mchanganuo mzuri wa mambo. Ndani ya Qur'ani kuna siri za viumbe na maajabu yao. Maajabu yaliyomo katika mwili wa mwandamu, katika ulimwengu na hata katika mazingira. Ndani yake kuna mambo ambayo akili za wafumbuzi haziyafikii. Lakini hii haina maana kwamba Qur'ani ni kitabu cha elimu ya fizikia, au elimu ya kemia, au unajimu wa elimu ya utabibu, hadi ifikie hatua za kasoro zinazo nasibishwa kwenye elimu hizo zihamishiwe kwe Qur'ani. La hasha, Qur'ani ni

---

[٤٦] Sunan Ad-Daarimi: 2/435, kitab fadhailil-qur'an, na mfano wa hadithi hii ipo katika vitabu vya Kishia.

[٤٧] Hadithi hii imetajwa katika Al-Mizan, jz:3, akinukuu kutoka kwenye baadi ya vyanzo, katika tafsiri ya aya 7-□ □□ □□□□□ □□-□□□□□.□

kitabu cha hidaya na uongofu. Hutumia nyenzo zote ili kulifikia lengo lake. Na elimu zote hizi zinajikita katika lengo hili, na Qur'ani huchukua katika elimu hizi kiwango kinacho hakikisha lengo lake.

٨. Kuipa umuhimu Qur'ani ni kujivua dhima kutokana na malalamiko yake pindi itakapo achwa, kama ilivyo tajwa katika hadithi iliyo tangulia huko nyuma: "Vitu vitatu vitamlalamikia Mwenyezi Mungu...". Bila kusahau kwamba mashtaka ya Qur'ani hayatapingwa mbele ya Mwenyezi Mungu aliye tukuka, kama ilivyo elezea hadithi kwamba: "Qur'ani ni mtoa ripoti anaye kubaliwa", kwa maana kwamba yenyewe ni mshitaki mkweli na atakae pewa haki. Na hasa ikizingatiwa kuwa shahidi wa malalamiko ya hatakuwa isipokuwa mtume (s.a.w.w), anasema Mwenyezi Mungu:

[وَقَالَ الرَّسُولُ يَا رَبِّ إِنَّ قَوْمِي اتَّخَذُوا هَذَا الْقُرْآنَ مَهْجُوراً]

"Na mtume atasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika watu wangu wameifanya Qur'ani hii yenye kuhamwa"[٤٨] .

٩. Kufaulu kwa kupata uombezi na shafaa ya Qur'ani. Hadithi imeisifia Qur'ani kuwa ni "mwombezi mwenye kukubaliwa oumbezi wake". Hadithi nyingine katika kuelezea uombezi wa Qur'ani inasema:

(وكان القرآن حجيزاً عنه – أي حاجزاً وساتراً عن قارئ القرآن – يوم القيامة، يقول: يا رب إن كل عامل أصاب أجر عمله غير عاملي فبلّغ به أكرم عطائك، قال: فيكسوه الله العزيز الجبار حلتين من حلل الجنة ويوضع على رأسه تاج الكرامة ثم يقال له: هل أرضيناك فيه؟ فيقول القرآن: يا رب قد كنت أرغب له فيما هو أفضل من هذين قال: فيُعطى الأمن بيمينه والخلد بيساره ثم يدخل الجنة فيقال له: اقرأ آية فاصعد درجة ثم يقال له هل بلغنا به وأرضيناك؟ فيقول: نعم).

"Na Qur'ani siku ya Kiyama itakuwa ni kiziwizi chake –yaani kinga na kiziwizi cha msoma Qur'ani–. Itasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika kila aliye tenda jambo atapata malipo ya kazi yake, isipokuwa aliye nifanyia kazi mimi. Mpe malipo yako yaliyo bora zaidi. Mwenyezi Mungu mwenye nguvu na afanyae alitakalo, atamvisha mavazi mawili mazuri katika mavazi ya peponi, na atawekewa taji la utukufu kichwani mwake, kisha Qur'ani itaulizwa: Je tumekuridhisha kwa mtu

[٤٨] Surat Al-Furqan: 30.

huyo? Qura'ani itasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Nilikuwa nikimtakia kilicho bora zaidi ya hivyo viwili ulivyo mpa. Kisha atapewa amani kuliani kwake na kuishi milele kushotoni kwake, kisha ataingizwa peponi na ataambiwa: Soma aya ya Qur'ani upande daraja. Hapo ndipo Qur'ani itaulizwa: Je tumemfikisha (ulipo pataka afike) na je tumekuridhsha? Ndio. Qur'ani itajibu"[٤٩].

Na kuna faida nyingine nyingi zisizo kuwa hizi. Kama uonavyo baadhi ya faida hizo sio maalumu kwa waislamu tu, ndio maana utaona mwitiko wa wanafikra, wasomi na viongozi mbali mbali wakiielekea Qur'ani na kuchukua ndani yake wakitakacho, hata kama sio waislamu.

Mpaka hapa nadhani sababu nilizo zitaja zinatosha kumwamsha mwanadamu na kumsukuma kuielekea Qur'ani na kuipa umuhimu, stahiki kiasi cha nyama na damu yake kuchanganyikana na Qur'ani. Na mimi hapa, ninamuhimiza[٥٠] kila anaye jua kuwa nina haki juu yake, sawa wasa haki hiyo iwe kisheria au kimaadili, ahitimishe Qur'ani kwa uchache ndani ya mwaka mara mbili. Kiasi hiki ni rahisi sana, hasa ikizingatiwa kuwa ndani ya mwezi wa Ramadhani pekee huwa ikisomwa nusu ya kiasi hiki au zaidi.

Na sababu muhimu zaidi nilizo zitaja ni zile zilizo pokelewa katika hadithi nilizo zichagua kwa ajili yako, kiasi kwamba hadithi hizo zinazidi arobaini, ikiwa ni katika kufuata suna ya wanazuoni wema walio pita ya kutunga vitabu vyenye anwani ya *hadithi arobaini* kwenye nyanja mbalimbali za elimu na maarifa. Ni matarajio yangu wasomi hao nami nikiwa nao tuwe ni miongini mwa watu walio lengwa na hadithi hii kutoka kwa mtume (s.a.w.w), alisema:

(من حفظ عني من أمتي أربعين حديثاً في أمر دينه يريد به وجه الله عز وجل والدار الآخرة بعثه الله يوم القيامة فقيها عالماً)

"Yeyote katika umma wangu, atakae hifadhi hadithi arobaini katika jambo la dini yake, kwa kitendo hicho akawa anatafuta radhi za Mwenyezi Mungu aliye tukuka,

---

[٤٩] Al-Kafii: 2/604.

[٥٠] Muhimizo huu umekuwa na msukumo mkubwa kwa walio wengi katika kuifanyia kazi Qur'ani. Mwenyezi Mungu awalipe malipo bora zaidi ya wafanya mema.

na nyumba ya akhera, Mwenyezi Mungu atamfufua siku ya Kiyama hali ya kuwa ni mwanazuoni msomi”[٥] .[١]

QUR’ANI YAJISIFU YENYEWE

Ama jambo muhimu zaidi kuliko hayo ni kukusomeeni baadhi ya aya ambazo Qur’ani tukufu yajisifu kwazo ili tuitambue, kwani bila shaka yenyewe inajijua zaidi, na iweje isijijue wakati ni maneno ya mbora wa wasemaji? Kutokana na aya hizi hufahamika utukufu na hadhi ya Qur’ani hii, heshima na baraka zake:

[هَذَا بَيَانٌ لِّلنَّاسِ وَهُدًى وَمَوْعِظَةٌ لِّلْمُتَّقِينَ]

١. “Hii ni bayana kwa watu wote, na ni uwongofu, na mawaidha kwa wachamungu.[٥] ”[٢]

[إِنَّا أَنزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ لِتَحْكُمَ بَيْنَ النَّاسِ]

٢. “Hakika sisi tumekuteremshia Kitabu hiki kwa haki ili upate kuhukumu baina ya watu kwa alivyo kuonyesha Mwenyezi Mungu. Wala usiwe mtetezi wa mahaaini”[٥] .[٣]

[يَا أَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَاءكُم بُرْهَانٌ مِّن رَّبِّكُمْ وَأَنزَلْنَا إِلَيْكُمْ نُوراً مُّبِينًا، فَأَمَّا الَّذِينَ آمَنُواْ بِاللّهِ وَاعْتَصَمُواْ بِهِ فَسَيُدْخِلُهُمْ فِي رَحْمَةٍ مِّنْهُ وَفَضْلٍ وَيَهْدِيهِمْ إِلَيْهِ صِرَاطاً مُّسْتَقِيماً]

٣. “Enyi watu! Umekufikieni ushahidi kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Na tumekuteremshieni nuru iliyo wazi. Ama wale walio muamini Mwenyezi Mungu, na wakashikamana naye, basi atawatia katika rehema yake na fadhila, na atawaongoa kwenye njia iliyo nyooka”[٥] .[٤]

---

[٥١] Al-Khisal: 2/542, mlango wa (Al-arbau’n).

[٥٢] Surut Al-Imaran: 138.

[٥٣] Surat An-Nisaa: 105.

[٥٤] Surat An-Nisaa: 174-175.

[قَدْ جَاءكُم مِّنَ اللهِ نُورٌ وَكِتَابٌ مُّبِينٌ، يَهْدِي بِهِ اللهُ مَنِ اتَّبَعَ رِضْوَانَهُ سُبُلَ السَّلاَمِ وَيُخْرِجُهُم مِّنِ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ بِإِذْنِهِ وَيَهْدِيهِمْ إِلَى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ]

٤. "Enyi Watu wa Kitabu! Amekwisha kujieni Mtume wetu anaye kufichulieni mengi mliyo kuwa mkiyaficha katika Kitabu, na anaye samehe mengi. Bila shaka imekujieni kutoka kwa Mwenyezi Mungu Nuru na Kitabu kinacho bainisha. Mwenyezi Mungu huwaongoa wenye kufuata radhi yake katika njia za salama, na huwatoa katika giza kuwapeleka kwenye nuru kwa amri yake, na huwaongoa kwenye njia iliyo nyooka.[٥] "

[وَلَوْ أَنَّهُمْ أَقَامُواْ التَّوْرَاةَ وَالإِنجِيلَ وَمَا أُنزِلَ إِلَيهِم مِّن رَّبِّهِمْ لأَكَلُواْ مِن فَوْقِهِمْ وَمِن تَحْتِ أَرْجُلِهِم]

٥. "Na lau wangeliishika Taurati na Injili na yote waliyo teremshiwa kutokana na Mola wao Mlezi, basi hapana shaka wangelikula vya juu yao na vya chini ya miguu yao. Wapo watu miongoni mwao walio sawa, lakini wengi wao wanayo yafanya ni mabaya mno.[٦] "

[قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ لَسْتُمْ عَلَى شَيْءٍ حَتَّىَ تُقِيمُواْ التَّوْرَاةَ وَالإِنجِيلَ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْكُم مِّن رَّبِّكُمْ]

٦. "Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Hamna lenu jambo mpaka muishike Taurati na Injili na yote mlio teremshiwa kutokana na Mola wenu Mlezi.[٧] "

[مَّا فَرَّطْنَا فِي الكِتَابِ مِن شَيْءٍ]

٧. "Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote.[٨] "

[وَهَذَا كِتَابٌ أَنزَلْنَاهُ مُبَارَكٌ]

٨. "Na hiki ni Kitabu tulicho kiteremsha, kilicho barikiwa.[٩] "

[وَإِذَا قُرِئَ الْقُرْآنُ فَاسْتَمِعُواْ لَهُ وَأَنصِتُواْ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ]

٥: Surat Al-Maidah: 15-16.

٦: Surat Al-Maidah: 66.

٧: Surat Al-Maidah: 68.

٨: Surat Al-An'aam: 38.

٩: Surat Al-An'aam: 92.

٩. “Na isomwapo Qur’ani isikilizeni na mnyamae ili mpate kurehemewa.[٦] ”

[يَا أَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَاءتْكُم مَّوْعِظَةٌ مِّن رَّبِّكُمْ وَشِفَاء لِّمَا فِي الصُّدُورِ وَهُدًى وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ]

١٠. “Enyi watu! Yamekujieni mawaidha kutoka kwa Mola wenu Mlezi, na posa kuponyesha yaliyomo vifuani, na uongofu, na rehema kwa waumini.[٦] ”

[إِنَّ هَذَا الْقُرْآنَ يِهْدِي لِلَّتِي هِيَ أَقْوَمُ وَيُبَشِّرُ الْمُؤْمِنِينَ الَّذِينَ يَعْمَلُونَ الصَّالِحَاتِ]

١١. “Hakika hii Qur'ani inaongoa kwenye yaliyo nyooka kabisa, na inawabashiria waumini ambao wanatenda mema.[٦] ”

[اللَّهُ نَزَّلَ أَحْسَنَ الْحَدِيثِ كِتَابًا مُّتَشَابِهًا مَّثَانِيَ تَقْشَعِرُّ مِنْهُ جُلُودُ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ ثُمَّ تَلِينُ جُلُودُهُمْ وَقُلُوبُهُمْ إِلَى ذِكْرِ اللَّهِ ذَلِكَ هُدَى اللَّهِ يَهْدِي بِهِ مَنْ يَشَاء وَمَن يُضْلِلْ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ هَادٍ]

١٢. “Mwenyezi Mungu ameteremsha hadithi nzuri kabisa, Kitabu chenye kufanana na kukaririwa; husisimua kwacho ngozi za wenye kumkhofu Mola wao Mlezi. Kisha ngozi zao na nyoyo zao hulainika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Huo ndio uwongofu wa Mwenyezi Mungu, na kwa huo humwongoa amtakaye. Na ambaye ameachwa na Mwenyezi Mungu kupotea, basi hapana wa kumwongoa.[٦] ” ٣

[وَإِنَّهُ لَكِتَابٌ عَزِيزٌ، لا يَأْتِيهِ الْبَاطِلُ مِن بَيْنِ يَدَيْهِ وَلا مِنْ خَلْفِهِ تَنزِيلٌ مِّنْ حَكِيمٍ حَمِيدٍ]

١٣. “Kwa hakika wanayo yakataa mawaidha haya yanapo wajia (wataangamia), na haya bila ya shaka ni Kitabu chenye nguvu na utukufu. Hautakifikia upotovu mbele yake wala nyuma yake. Kimeteremshwa na Mwenye hikima, Msifiwa.[٦] ” ٤

[اللَّهُ الَّذِي أَنزَلَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ وَالْمِيزَانَ]

---

٦١ Surat Al-a’araaf: 204.

٦١ Surat Yuunus: 57.

٦٢ Surat Al-Israa: 9.

٦٣ Surat Az-Zumar: 23.

٦٤ Surat Fussilat: 41-42.

١٤. “Mwenyezi Mungu ndiye aliye teremsha Kitabu kwa Haki, na Mizani.[٦٥] ”

[وَإِنَّهُ فِي أُمِّ الْكِتَابِ لَدَيْنَا لَعَلِيٌّ حَكِيمٌ]

١٥. “Na hakika hiyo imo katika Asili ya Maandiko yalioko kwetu, ni tukufu na yenye hikima.[٦٦] ”

[وَمَن يَعْشُ عَن ذِكْرِ الرَّحْمَنِ نُقَيِّضْ لَهُ شَيْطَانًا فَهُوَ لَهُ قَرِينٌ]

١٦. “Anaye yafanyia upofu maneno ya Rahmani tunamwekea Shet'ani kuwa ndiye rafiki yake.[٦٧] ”

[فَاسْتَمْسِكْ بِالَّذِي أُوحِيَ إِلَيْكَ إِنَّكَ عَلَى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ، وَإِنَّهُ لَذِكْرٌ لَّكَ وَلِقَوْمِكَ وَسَوْفَ تُسْأَلُونَ]

١٧. “Basi wewe yashike yaliyo funuliwa kwako. Hakika wewe uko kwenye njia iliyonyooka. Na hakika haya ni ukumbusho kwako na kwa kaumu yako. Na mtakuja ulizwa.[٦٨] ”

[هَذَا بَصَائِرُ لِلنَّاسِ وَهُدًى وَرَحْمَةٌ لِّقَوْمٍ يُوقِنُونَ]

١٨. “Hizi ni dalili zilizo wazi kwa watu wote, na ni uwongofu, na rehema kwa watu wanao yakinisha.[٦٩] ”

[أَفَلا يَتَدَبَّرُونَ الْقُرْآنَ أَمْ عَلَى قُلُوبٍ أَقْفَالُهَا]

١٩. “Je hawaizingatii hii Qur'ani? Au kwenye nyoyo (zao) zipo kufuli?[٧٠] ”

[ق وَالْقُرْآنِ الْمَجِيدِ]

٢٠. “Qaaf. Naapa kwa Qur'ani tukufu![٧١] ”

---

٦٥. Surat Ash-Shura: 17.

٦٦. Surat Az-Zukhruf: 4.

٦٧. Surat Az-Zukhruf: 36.

٦٨. Surat Az-Zukhruf: 43-44.

٦٩. Surat Al-Jaathiyah: 20.

٧٠. Surat Muhammad: 24.

٧١. Surat Qaaf: 1.

[وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْآنَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِن مُّدَّكِرٍ]

٢١. "Na hakika tumeisahilisha Qur'ani kuikumbuka. Lakini yupo anaye kumbuka?[٧] " ٢

[إِنَّهُ لَقُرْآنٌ كَرِيمٌ، فِي كِتَابٍ مَّكْنُونٍ، لا يَمَسُّهُ إِلا الْمُطَهَّرُونَ]

٢٢. "Hakika bila ya shaka hii ni Qur'ani tukufu, katika kitabu kilicho hifadhiwa, hapana akigusaye ila walio takaswa.[٧] " ٣

[أَلَمْ يَأْنِ لِلَّذِينَ آمَنُوا أَن تَخْشَعَ قُلُوبُهُمْ لِذِكْرِ اللَّهِ وَمَا نَزَلَ مِنَ الْحَقِّ وَلا يَكُونُوا كَالَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِن قَبْلُ فَطَالَ عَلَيْهِمُ الأَمَدُ فَقَسَتْ قُلُوبُهُمْ وَكَثِيرٌ مِّنْهُمْ فَاسِقُونَ]

٢٣. "Je! Wakati haujafika bado kwa walio amini zikanyenyekea nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na haki iliyo teremka? Wala wasiwe kama walio pewa Kitabu kabla yao, muda wao ukawa mrefu, kwa hivyo nyoyo zao zikawa ngumu, na wengi wao wakawa wapotovu.[٧] "

[لَوْ أَنزَلْنَا هَذَا الْقُرْآنَ عَلَى جَبَلٍ لَّرَأَيْتَهُ خَاشِعاً مُّتَصَدِّعاً مِّنْ خَشْيَةِ اللَّهِ وَتِلْكَ الأَمْثَالُ نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ]

٢٤. "Lau tumeiteremsha hii Qur'ani juu ya mlima, basi bila ya shaka ungeliuona ukinyenyekea, ukipasuka kwa hofu ya Mwenyezi Mungu. Na hiyo mifano tunawapigia watu ili wafikiri.[٧] " ٥

[وَرَتِّلِ الْقُرْآنَ تَرْتِيلاً، إِنَّا سَنُلْقِي عَلَيْكَ قَوْلاً ثَقِيلاً

٢٥. "Na soma Qur'ani kwa utaratibu na utungo. Kwa hakika sisi tutakuteremshia kauli nzito.[٧] " ٦

[بَلْ هُوَ قُرْآنٌ مَّجِيدٌ، فِي لَوْحٍ مَّحْفُوظٍ]

---

٧ Surat Al-Qamar: 40.

٧ Surat Al-Waaqi'a: 77-79.

٧ Surat Al-Hadid: 16.

٧ Surat Al-Hashri: 21.

٧ Surat Al-Muzammil: 4-5.

٢٦. “Bali hii ni Qur'ani tukufu . Katika ubao ulio hifadhiwa.[٧] ”

[إِنَّهُ لَقَوْلٌ فَصْلٌ، وَمَا هُوَ بِالْهَزْلِ]

٢٧. “Hakika hii ni kauli ya kupambanua, wala si mzaha.[٧] ”

[الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَنزَلَ عَلَى عَبْدِهِ الْكِتَابَ وَلَمْ يَجْعَل لَّهُ عِوَجَا، قَيِّماً لِّيُنذِرَ بَأْساً شَدِيداً مِن لَّدُنْهُ وَيُبَشِّرَ الْمُؤْمِنِينَ]

٢٨. “Kuhimidiwa ni kwa Mwenyezi Mungu, ambaye amemteremshia mja wake kitabu, wala hakukifanya kina upogo. Kimenyooka sawa, ili kitoe onyo kali kutoka kwake, na kiwabashirie Waumini watendao mema kwamba watapata ujira mzuri.[٧] ”

[وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ تِبْيَاناً لِّكُلِّ شَيْءٍ وَهُدىً وَرَحْمَةً وَبُشْرَى لِلْمُسْلِمِينَ]

٢٩. “Na tumekuteremshia kitabu hiki kinacho bainisha kila kitu, na ni uwongofu, na rehema, na bishara kwa waislamu.[٨] ”

[وَمَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِي فإن لَهُ مَعِيشَةً ضَنكاً وَنَحْشُرُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَعْمَى]

٣٠. “Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu.[٨] ”

Hizi ni baadhi ya sifa na athari nzuri ambazo husifika nazo Qur’ani. Qur’ani ni kitabu kilicho barikiwa, kwenye ngvu na utukufu na kilicho tukuzwa. Qur’ani ni bayana, ni uongofu, ni mawaidha, ni rehema, ni tiba, ni ukumbusho, na ni nuru iliyo teremshwa kwa haki, ili kuhukumu baina ya watu na ili kiwaingize waumini katika rehema za Mwenyezi Mungu na fadhila zake, na ili kiwaongoze njia iliyo nyooka. Qur’ani ni kitabu kitukufu na chenye hekima, ni chenye kuwafumbua macho watu, ni kauli nzito, ni kipambanuzi cha haki na batili na wala sio mzaha. Hivyo, ukweli na uhakika wa Qur’ani umewekwa ndani ya matamshi yake, na

---

٧ Surat Al-Buruuj: 21-22.

٧ Surat At-Taariq: 13-14.

٧ Surat Al-Kahf: 1-2.

٨ Surat An-Nahli: 89.

٨ Surat Taha: 124.

matamshi ndio chombo kilicho hifadhi ukweli na uhakika huo. Matamshi ya Qur'ani ndio yanayo isogezea akili uhakika na zile maana za ndani, zile maana zilizo fichikana katika lohi iliyo mahfudhi (hifadhiwa), kiasi kwamba hakuna agusaye wala kufikia maana uhakika huo isipokuwa walio takaswa kutokana na madhambi na maasi, nyoyo zao zikasafika na kila aina ya uchafu kiasi cha kuweza kuakisi kikamilifu ukurasa wa lohi hiyo iliyo hifadhiwa. Ama wasio kuwa hao, hawana uwezo wa kuzifahamu isipokuwa kwa kile kiwango kidogo cha ukamilifu walio pewa. Anasema Mwenyezi Mungu:

[أَنزَلَ مِنَ السَّمَاء مَاء فَسَالَتْ أَوْدِيَةٌ بِقَدَرِهَا]

"Ameteremsha maji kutoka mbingini kisha mabonde yakamiminika maji kwa kadiri na kiwango chake"[٢] .

Watu wameamrishwa kuizingatia Qur'ani, kuisoma kwa mafungu, kushikamana nayo na kunyamanza pindi inaposmwa, na lau ingeli kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu basi wangeli kuta ndani yake hitilafu nyingi. Na lau wangeli ishika Qur'ani na waka ambatana nayo, hapana shaka wangeli kula vya juu yao na vya chini ya miguu yao, na nyoyo zao zingeli nyenyekea na kulainika, na wangeli stahiki kheri nyingi kutoka kwa mola wao mlezi. Lakini ikiwa wataiacha wataishi katika maisha ya dhiki na watavamiwa na mashetani mpaka wawafanye kuwa marafiki wao, na nyoyo zao zitakuwa ngumu hata kufikia kuwa kama mawe au zaidi, kwani kuna mawe yanayo timbuka mito, na kuna mengine yanayo pasuka yakatoka maji ndani yake, na kuna mengine huanguka kwa sababu ya khofu ya Mwenyezi Mungu. Na nyoyo zilizo mbali na Qur'ani na utajo wa Mwenyezi Mungu aliye takasika ni ngumu zaidi kiasi kwamba ndani yake hayawezi kuingia hata tone la maarifa. Mwenyezi Mungu anasema:

[وَتِلْكَ الأَمْثَالُ نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ]

" Na hiyo mifano tunawapigia watu ili wafikiri"[٣] .

---

[٢] Surat Ar-Ra'd: 24.

[٣] Surat Al-Hijr:

UFAFANUZI WA BAADHI YA SIFA ZA QUR'ANI

Lakini maelezo hayo kuhusu sifa za Qur'ani hayatoshezi. Hivyo, ninaona kuna udharura wa kuzitolea ufafanuzi wa ziada baadhi ya sifa hizo, ufafanuzi utakao kuwa na athari chanya kijamii na kimaadili, ama ufafanuzi wa sifa hizo katika nyanja zingine, tumeuacha kwa ajili ya vitabu vya tafsiri, kwenye aya zilizo zitaja. Na sifa hizi sizitaji kwa lengo la kuifahamu Qur'ani pekee, bali ninazifafanua ile huwafahamu Ahlul-bayt (a.s) pia, kwakuwa wao ndio wenza wa Qur'ani na kwa pamoja hutengeneza mihimili miwili isiyo farakana. Hivyo, ikiwa Qur'ani inasema kweli basi Ahlul-bayt nao wapo na haki na haki ipo nao. Qur'ani ni kitabu kisicho fikiwa na batil, na Ahlul-bayt nao ni maasumina walio hifadhiwa na kutenda dhambi. Na ikiwa Qur'ani ni msimamizi na mlinzi, Ahlul-bayt (a.s) nao pia wana usimamizi na mamlaka juu ya watu, kwani wao ndio viongozi wa na ni wabora zaidi kuliko nafsi zao. Na ufuatao ni ufafanuzi wa sifa hizo:

Kitabu Kilicho Barikiwa

Yaani Qur'ani ina baraka tele. Na hivyo ndivyo ulivyo ukweli, na baraka zake zinaweza kuelezewa katika pande kadhaa:

١. Qur'ani ina baraka kwa upande wa chanzo chake na pahali iliko tokea. Kwa sababu aliye iteremsha ni Mwenyezi Mungu aliye tukuka, mtenda wema kwa waja wake mtoa neena sozizo na ukomo wala hesabu.
٢. Ni yenye baraka kwa ilipo teremkia. Imeteremkia kwenye moyo wa bwana mtume mwenye huruma, aliye tumwa kuwa rahma kwa walimwegu.
٣. Qur'ani imebarikiwa pia kwenye athari zake. Ndini yake mna hidaya, heri na furaha ya dunia na akhera. Ndani ya Qur'ani mna mfumo na nidhamu ya maisha ya nwanadamu, mna misingi na ulinzi wa maisha, mna amani na utulivu.
٤. Kadhalika Qur'ani imebarikiwa kwa upande wa hajimu na kiasi chake. Ni kitabu kimoja, lakini wasomi wote hunufaika nacho, kila mmoja huchukua ndani yake ikitakacho. Utamkuta msomi wa Usuli, mwanazuoni wa fikihi,

msomi wa nahau, mwandishi, mwanafikra, mwanasiasa, msomi wa elimu ya jamii, msomi wa uchumi, daktari, mtunga sheria na mtawala, utawaona wote wakinufaika na Qur'ani, na kila mmoja akitoa hoja zake kwa kutumia aya za Qura'ni. Lakini pamoja na yote hayo, bado itabakia ni kitabu cha kudumu na chenye kutoa maafira. Na hii ni dalili ya kuwa iliteremka kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa sababu maarifa yaliyomo ndani ya Qur'ani ni maarifa ambayo hayawezi kukusanya na vitabu kadhaa kama si vyote.

٥. Na mwisho kabisa, Qur'ani ina baraka kwa idadi waliyo ongoka kwayo, nyoyo zao zikanawirika kwayo na akili zao zikapata mwanga kwa baraka zake.

Kitabu Chenye Nguvu (**Al–A'ziz**)

١. Kwa maana kwamba Qur'ani ni kitabu ambacho ni vigumu kufikia uhakika wake. Kwani kitabu ambacho uhakika wake umehifadhiwa kwenye lohi mahfudhi, na matamshi yake chombo tu cha kuziweka maana zake karibu na akili ya kibinadamu iliyo zoea mambo ya kimada, na isiyo weza kuufikia ule uhakika wenyewe kama ulivyo. Ndio, wanao weza kuufikia na kuufahamu uhakika huo, ni wale tu walio takasika na ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na akawasafisha barabara, ambao si wengine bali ni Ahlul-bayt (a.s). Bila shaka umemsikia Amirulmuunina Ali (a.s) akisema: Kwa hakika sisi hatumiliki elimu zaidi ya ufahamu wetu wa Qur'ani.

٢. Nacho ni kitabu chenye nguvu kwa maana ya kwamba, ni nadra kupata mfano wake, kwani ni maneno ya asiye kuwa na mfano.

٣. Ni kitabu chenye nguvu kwa maana kwamba, kaiwezekani kikapwa na jambo baya. Na hivyo maana yake itakuwa ni sawa na aya hii:

[إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ]

"Hakika sisi ndio tulio teremsha ukumbusho huu, na hakika sisi ndio tutakao uhifadhi"٨٤

٨٤ Surat Al-Hijr: 9.

٤. Qur'ani ni yenye nguvu kwa maana kwamba ni kitabu chenye kushinda, kwa sababu ni neno la Mwenyezi Mungu, na neno la Mwenyezi Mungu ndilo lipo juu. Hivyo, Qur'ani ni yenye kushinda na wala haishindwi, nafasi yake ni kuwaongoza na kuwatawala waja kwa kutoa mwelekeo wa mambo yao.

٥. Ni kitabu chenye nguvu kwa maana kwamba ni chenye kutafutwa. Kwani imesemwa kuwa: Kila kilichopo huchokwa na kila kilicho potea hutafutwa. Na Qur'ani hii ni yenye kutafutwa na kila atakae kufika kwa Mwenyezi Mungu aliye tukuka.

Kitabu Kitukufu (**Almajiid**)

Raghibu anasema katika kitabu chake cha *Al-Mufradat:* Neno: "Almajdu": ni upana katika ukarimu na utukufu. Na asili ya neno hilo ni kauli ya warabu: "majadat al-ibilu", pale ngamia anapokutwa kwenye malisho yenye nyasi nyingi na makubwa. Hivyo, Qur'ani imesifiwa kwa sifa hii ya "majiid" kwa sababu ya wingi wa mema ya dunia na akhera iliyo yabeba. Na ni kwa sabubu hiyo hiyo Mwenyezi Mugu akaisifu kwa kusema:

[إِنَّهُ لَقُرْآنٌ كَرِيمٌ]

" Bila shaka hii ni Qur'ni tukufu"[٨٥] kwa sababu ya kheri zake zinazo patikana kwa wingi, na hili tumeliashiria wakati tukifafanua athari tele za sifa "mubaarak".

Mwangalizi (**Qayyim**)

Sifa hii inatokana na neno: "alqaymumah" lenye maana ya uangalizi. Hivyo, Qur'ani ni kitabu kinacho wasimamia waja wa Mwenyezi Mungu, ili kuwaongoza na kuwaonyesha masilahi na heri yao, ikiwa ni pamoja na kuwandaliwa kila aina ya furaha na mafaniko ya dunia na akhera, ni hii ni sawa afanyavyo msimamizi wa familia au jamii. Na njia inayotumiwa na Qur'ani katika usimamizi, ni msimamizi wa njia nyinginezo, sawasawa katika uuga wa itikadi au sheria. Ndio njia inayo ongoza njia zilizo salia, na hizo njia nyengine zinafuata njia ya Qur'ani. Kwa ajili hiyo, ikiwa mwanadamu atataka kheri na furaha hana namna zaidi ya kuuweka

[٨٥] Surat Al-Hadid: 77.

usimamizi wa Qur'ani maishani mwake, na si kama walivyo fanya leo hii kuipa mgongo na kuiacha njia Qur'ani, na badala yake wakazifanya akili za kibinadamu ambazo ni pungufu kuwa ndio hakimu wa maisha yao, akili ambayo mara nyingi hunyenyekea mbele matakwa ya nafsi na masilahi yakupita. Na ndio maana Mwwenyezi Mungu akaisifu Qur'ani kwamba, ndani yake hakuna upogo wala mafungufu, hakuna tatizo wala kasoro, akasema:

[وَلَمْ يَجْعَل لَّهُ عِوَجَا]

"... wala hakukifanya kina upogo (kombo)"[٨٦] Kwani miongoni mwa masharti ya anayetaka kumsimamia mwanadamu na kukamilisha mapungufu yake, yeye mwenye awe ni mkamilifu, kwani kama wasemavyo kuwa: "Asiye na kitu hawezi kutoa kitu". Ni lazima msimamizi wa watu aisiwe na mapungu wala kasoro. Na sifa hii haipatikani isipokuwa kwenye Qur'ani na mwenza wake ambae ni kizito kidogo, yaani Ahlul-bayt (a.s). Na visivyo kuwa hivi viwili, havina haki ya kuongoza jamii na kuisimamia. Na haidithi zenye maana hii ni nyingi sana na zote zinatanguliza Qur'ani na Ahlul-Bayt (a.s).

[وَمَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِي فإن لَهُ مَعِيشَةً ضَنكاً]

"Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa hakika atapata maisha yenye dhiki"[٨٧] yaani maisha aliyo bana. Na hii ni sifa ya kila atakaye puuza ukumbusho na mawaidha ya Mwenyezi Mungu, kiasi kwamba akakata mahusiano yake na Mwenyezi Mungu na kishi mbali na Qur'ani tukufu, kwa hakika mtu huyo atakuwa na dhidi, mahangaiko na machukungu maishani mwake, kwakuwa atakuwa amejiondoa katika rehema za Mwenyezi Mungu zilizo enea kila mahali na atakuwa ni muhanga wa matamanio na tamaa ambavyo havina ukomo. Hivyo, ataishi akiwa na khofu ya mauti na hatimaye kukhasirika dunia ambayo ndio ilikuwa lengo lake na akhera hatakuwa na fungu. Ataishi akipupia kile alicho nacho akihofia kutoweka, ataishi kwa taabu kwakuwa hafuati isipokuwa sarabi (mazigazi), hapati chochote adganiacho mna faraha yake isipokuwa humbainikia kuwa alikosea na hivyo kufanya juhudi kutafuta kingine. Kwa mfano: atadhania kuwa furaha

---

[٨٦] Surat Al-Kahf: 1.

[٨٧] Surat Taha: 124.

ataipata katika mali, atahangaika kukusanya mali hizo mpaka zitafikia mamilioni, lakini haipati ile furaha, atadhani labda furaha ataipata kwenye manyumba ya fahari, ataanza kujenga manyumba ambayo jicho halijawahi kuyaona, lakini pia huko nako hataipa furaha yake, wakati huo atadhani furaha imo kwa wanawake, anastarehe nao kadiri awezavyo, mara anajikuta kafika kwenye njia iliyo fungwa, na hapo ndio kauli yake Mwenyezi Mungu itamhusu: "*Alipo uona mwezi unachomoza alisema: Huyu ndiye Mola mlezi wangu.*", na mwezi hapa ni kinaya ya mali, atadhania mali ndiyo Mola mlezi wake mwenye kumletea furaha, Mwenyezi Mungu anasema: "*Na ilipo tua*" na akafeli kuipata ile furaha, "*akasema: Siwapendi wanao tua*", "Na *alipo liona jua limechomoza*", hapa jua ni kinaya ya mambo mengine ya dunia, "*akasema: Huyu ndiye Mola mlezi wangu. Huyu mkubwa kiliko wote*", huyu ndiye atakaye nipa furaha na utulivu wa moyo kwa kuwa ni mkubwa zaidi ya wote.

Na sehemu muhimu na yenye taathira kubwa ni "Ilipo tua" na Mola huyu mlezi mpya akafeli kuleta furaha "akasema: Siwapendi wanao tua", mamola wapungu wasio miliki heri hata ya nafsi zao achilia mbali kumiliki madhara au manufaa ya wasio kuwa wao. Ifikia hapa, ikiwa mtu atakuwa mwenye moyo safi na nia njema katika kutafuta ukweli, basi hakika mtu huyo ataipata hidaya na uongofu, na atasema maneno ya waumini kwamba:

[قَالَ يَا قَوْمِ إِنِّي بَرِيءٌ مِّمَّا تُشْرِكُونَ، إِنِّي وَجَّهْتُ وَجْهِيَ لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَاوَاتِ وَالأَرْضَ حَنِيفًا وَمَا أَنَاْ مِنَ الْمُشْرِكِينَ]

"*Enyi watu wangu! Mimi simo katika hayo mnayo fanyia ushirikina. Hakika mimi nimeuelekeza uso wangu sawa sawa kwa aliye ziumba mbingu na ardhi, wala mimi si miongoni mwa washirikina*"[٨]. Lakini kama hatakuwa na nia jema na ikhlasi, atandikiwa uovu na wakati huo majibu yake yatakuwa:

[وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَعْمَالُهُمْ كَسَرَابٍ بِقِيعَةٍ يَحْسَبُهُ الظَّمْآنُ مَاء حَتَّى إِذا جَاءهُ لَمْ يَجِدْهُ شَيْئًا وَوَجَدَ اللّهَ عِندَهُ فَوَفَّاهُ حِسَابَهُ واللّهُ سَرِيعُ الْحِسَابِ]

"Na walio kufuru vitendo vyao ni kama sarabi (mazigazi) uwandani. Mwenye kiu huyadhania ni maji. Hata akiyaendea hapati chochote. Na atamkuta Mwenyezi

[٨] Surat Al-An'am:76-77.

Mungu hapo naye amlipe hisabu yake sawa sawa. Na Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu.[٨] ”

Na hivyo atabakia katika uovu akiwa na mikosi na dhiki hali ya kuwa yumo baina nyundo ya kifo ambayo inaweza kummaliza muda wowote, na adhabu ya kupana tamaa: “Na hakika utawaona ni wenye kuwashinda watu kuliko wote kwa pupa ya kuishi”[٩] . Wewe mwenyewe unashuhudia kuwa matukio mengi ya kujinyonga yanatokea katika nchi zilizo endelea kiuchumi na ambazo watu wake huishi kwa kujaza matumbo.

[قَدْ جَاءكُم مِّنَ اللهِ نُورٌ وَكِتَابٌ مُّبِينٌ، يَهْدِي بِهِ اللهُ مَنِ اتَّبَعَ رِضْوَانَهُ سُبُلَ السَّلاَمِ وَيُخْرِجُهُم مِّنِ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ بِإِذْنِهِ وَيَهْدِيهِمْ إِلَى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ]

“Bila shaka imekujieni kutoka kwa Mwenyezi Mungu nuru na kitabu kinacho bainisha. Mwenyezi Mungu huwaongoa wenye kufuata radhi yake katika njia za salama, na huwatoa katika giza kuwapeleka kwenye nuru kwa amri yake, na huwaongoa kwenye njia iliyo nyooka.[٩] ” Basi Qur’ani ni nuru iumurikayo moyo wa muumini kwanza kasha kusafisha na uchafu wa maasi na madhambi, kasha kuuacha ukurasa wake uking’aa ili tayari kuingia haki ambayo ndio nuru ya umma na jamii itakayo iongoza kwenye mfumo utakayo uletea furaha na saada.

Miongoni mwa ibara za Qur’ani ninazo vutia, ni kwamba neno “*nur”* lenye maana ya nuru au mng’o, imelileta likiwa na sura ya umoja, wakati neno giza limekuja kwa sura ya wingi. Na sababu yake ni kuwa njia ya haki ni moja tu hata kama mifano yake ni mingi. Mwenyezi Mungu anasema:

[اهدِنَا الصِّرَاطَ المستَقِيمَ]

“*Tuongoze njia iliyo nyooka*”[٩] , wakati magiza yako mengi kama valiʋyo wengi miungu wanao zuilia na kuziba njia ya Mwenyezi Mungu.

---

[٨] Surat An-Nur: 39.

[٩] Surat Al-Baqarah: 96.

[٩] Surat Al-Maidah: 15-16.

[٩] Surat Al-Fath: 6.

Katika athari na baraka za Qur'ani ni kuwa humuogoza mwenye kufuata radhi za Mwenyezi Mungu kwenye njia za amani. Na amani ya kwanza anayo neemeka nayo ni amani ya nafsi, utulivyo wa moyo na utakaso wa akili:

[أَلاَ بِذِكْرِ اللهِ تَطْمَئِنُّ الْقُلُوبُ]

"Kwa hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mumgu ndio moyo hutua"[٩] . Kisha inafuatia amani ndani ya familia iliyo simamia misingi ya Uislamu na mafuzo ya Qur'ani:

[وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُم مِّنْ أَنفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِّتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُم مَّوَدَّةً وَرَحْمَةً إِنَّ فِي ذَلِكَ لآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ]

"Na katika Ishara zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao fikiri"[٩] . Na baadae ni amani baina ya wanajamii, pale yanapo tawala mafunzo na adabu za Kiislamu:

[فَأَصْبَحْتُم بِنِعْمَتِهِ إِخْوَاناً]

"Kisha kwa neema yake mkawa ndugu"[٩] , ٥

[مُّحَمَّدٌ رَّسُولُ اللَّهِ وَالَّذِينَ مَعَهُ أَشِدَّاء عَلَى الْكُفَّارِ رُحَمَاء بَيْنَهُمْ]

"Muhammad ni mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walio pamoja naye wana nguvu mbele makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao"[٩] na ٦

[وَيُؤْثِرُونَ عَلَى أَنفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ]

"Bali wanapendelea kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji"[٩] .

Qur'ani Ni Kauli Nzito

Uzito ambao unabebwa na kauli au neno. Na Qur'ani ni nzito kwenye nafsi, kwa sababu huyazuwia matakwa ya nafsi na haiiachi uhuru, bali huiadabisha, huijenga na kuongoza. Qur'ani ni nzito kenye akili kutokana na siri na mambo kina ambao huwa vigumu kwa akili za watu wenye kiburi kuyavumilia na kuyabeba.

---

[٩٢] Surat Ar-Ra'd: 28.

[٩٤] Surat Ar-Rum: 21.

[٩٩] Surat Al-Imran: 103.

[٩٦] Surat Al-Fath: 29.

[٩٧] Surat Al-Hashr: 9.

Vilevile Qur'ani ni nzito kwenye roho ya mwanadamu, kwani ndani yake kuna sheria nzito na malezi ya aina tofauti tofauti. Bwana mtu (s.a.w.w) ameliashiria hilo pia alipo sema: "Surat Al-Hud na Al-Waqi'ah zimenizeesha. Kwa sababu yake kuna: "*Simama sawa sawa kama ulivyo amrishwa*". Bila shaka alikuwa anajua uzito wa jambo hili ndio akasema hayo.

Na chanzo cha uzito wa Qur'ani ni kwakuwa inatokea kwa Mwenyezi Mungu mtukufu. Na hili linaweza kuthibitishwa na nukuu za wanahistoria juu ya hali ya bwana mtume (s.a.w.w) pindi akiteremshiwa wahai (ufunuo). Sehemu nyingine uzito wa Qur'ani umesifiwa namna hii:

[لَوْ أَنزَلْنَا هَذَا الْقُرْآنَ عَلَى جَبَلٍ لَّرَأَيْتَهُ خَاشِعًا مُّتَصَدِّعًا مِّنْ خَشْيَةِ اللَّهِ وَتِلْكَ الأَمْثَالُ نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ]

"*Lau kuwa tumeiteremsha hii Qur'ani juu ya mlima, basi bila ya shaka ungeli uona ukinyenyekea, ukipasuka kwa khofu ya Mwenyezi Mungu. Na hiyo mifano tunawapigia watu ili wafikiri*"[٨] .

Qur'ani ni nzito pia kutokana na mabalaa na matatizo yanayo msibu aliye ibeba (mtume) na yeyote anaye fanya juhudi za kuisimamisha katika jamii. Mwenyezi Mungu amesema:

[المص، كِتَابٌ أُنزِلَ إِلَيْكَ فَلاَ يَكُن فِي صَدْرِكَ حَرَجٌ مِّنْهُ لِتُنذِرَ بِهِ وَذِكْرَى لِلْمُؤْمِنِينَ]

"Alif Lam Mym 'Saad, Kitabu kilicho teremshwa kwako – basi isiwe dhiki kifuani kwako kwa ajili yake, upate kuonya kwacho, na kiwe ni ukumbusho kwa waumini"[٩] . Na ndio sababu ya bwana mtume (s.a.w.w) kuamrishwa kusimama usiku kwa ajili sala na ili kuwa karibu na Mwenyezi Mungu na kujenga mahusiano ya karibu kabisa na Mola mlezi wake mtukufu, kwa lengo kufanya maandalizi ya kuipokea kauli hiyo nzito na majukumu makubwa. Na Mwenyezi Mungu alimuahidi kuyapata matunda hayo kwa kusema:

[وَمِنَ اللَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهِ نَافِلَةً لَّكَ عَسَى أَن يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُوداً]

[٨] Surat Al-H'ashri: 21.

[٩] Surat Al-A'araaf: 2.

“Na amka usiku kwa ibada; ni ziada ya sunna khasa kwako wewe. Huenda Mola wako mlezi akakunyanyua cheo kinacho sifika”[١] .

Qur’ani Ni Mawaidha, Tiba, Uongofu Na Rehema

Hapa nitafupisha maneno aliyo yataja Sayyed Tabatabai katika tafsiri ya aya ya 138 katika surat Al-Imran[١] :

Raghibu anasema katika kitabu chake cha *Al-Mufradat:* “Neno *alwa’dh*, maana yake ni kukemea kunako ambatana na kuhofisha”. Na Khalili anasema: “Neno *alwa’dh,* maana yake ni ukumbusho wa jambo la kheri kiasi cha moyo kulainika”. Ama “Poza yay ale yaliyomo vifuani” ni kinaya cha kwamba Qur’ani inaondosha sifa mbaya za kiroho ambazo humsababishia mwanadamu uovu, humharibia maisha yake ya furaha na kumzuilia kheri ya dunia na akhera. Ama ni kwanini Mwenyezi Mungu ametumia neno vifua? Jibu ni kwamba: kwa kuwa watu wanajua moyo upo kifuani na wanajua kuwa mwanadamu hufahamu na kudiriki mambo kwa moyo wake na kuyatia akilini, hupenda na hukasirika kwa moyo wake, kama ambavyo hutaka, huchukia, hutaraji na hutamani kwao, ndo maana wakakihesabu kifua kuwa ni sanduku la yaliyo moyoni miongoni mwa siri na sifa za nzuri na mbaya kiroho zilizo ndani ya mwanadamu.

Ninasema kuwa: hadithi zinonyesha kuwa Qur’ani ni poza na shifaa ya baradhi ya mwili pia. Baadi ya hadithi zinaeleza kuwa, surat Al-Fatiha lau itasomwa kwa maiti mara sabini kisha akafufuka lingekuwa ni jambo la kushangaza.

Rehema ni hisia ya moyo inayo patika kwa kuona madhara au mapungufu kwa mtu mwingine, zikamsukuma kutaka kumuondoshea madhara au upungufu ule. Lakini sifa hii inahusishwa na Mwenyezi Mungu aliye takasika, huwa na maana ya kuhurumia mojo kwa moja bila kuanza kuhisia, kwa sababu Mwenyezi Mungu ameepukana na hisia, na hivyo hutumika sifa ya huruma kwake ikimanisha utoaji wake na unemeshaji wake kwa viumbe vila ulazima kuwa hisia.

---

[١] Surat Al-Israa: 79.

[١] Al-Mizan: jz: 10, katika tafsir ya aya 70-75 za surat Yuunus. Aya iliyo ikusudiwa na mwandishi ni ya 57 isemayo: “Enyi watu! Yamekufikieni mawaidha kutoka kwa Mola wenu, na poza ya ale yaliyomo vifuani, na uongozo na rehema kwa wenye kuamini”.

Huu ni upande mmoja tu katika kuyafafanua majina matukufu ambayo hayawezi huhusishwa na Mwenyezi Mungu kama yanavyo nasibishwa kwa viumbe.

Unapo zichukua sifa hizi nne za Qur'ani ambazo zimetajwa na Mwenyezi Mungu, namanisha sifa ya kuwa Qur'ani ni: mawaidha, pozo ya yale yaliyomo vifuani, uongofu na rehema, kisha ukazipima baadhi yake kwa baadhi, halafu ukazihusisha na Qur'ani, aya hiyo itatoa ubainifu unao kushanya athari zote nzuri na matendo yake masafi inayoyaweka katika nafsi za waumini tangu kuanzia inaposikika masikioni mwao hadi inapojikita ndani ya nyoyo zao.

Kwa hakika Qur'ani jambo la kwanza kabisa ilifanyalo kwa waumini baada kughafilika, na kuzingirwa na sintofahamu kiasi cha uwepo wao kuzungukwa na giza la mashaka, na pale nyoyo zao zinapo patwa na maradhi yatokanayo na kila aina ya sifa mbaya au hali mbaya, Qur'ani huwawaidhi kwa mawaidha mazuri, huwazindua na kuwatabahisha waamke kutoka katika usingizi huo wa kughafilika, kama ambavyo huwakemea waachane na tabia mbovu na matendo mabaya, na hatimae kuwahimiza kuiendea kheri na furaha na dunia na akhera. Kisha huanza kuhizisafisha nyoyo zao na kila sifa mbaya, na itaendelea kuondoa maafa ya akili na maradhi ya nyoyo moja baada jingine mpaka zimelizike.

Kisha Qur'ani huwaonyesha waumini hao mafunzo ya haki na maadili mazuri na matendo mema kwa upole na kuwainua daraja moja baada jingine na huwazogeza kwenye cheo baada ya kingine mpaka huwafikisha kwenye kituo cha walijikarisha kwa Mwenyezi Mungu, na hapo watafauli ufaulu wa watu wenye nia safi.

Qur'ani haishii hapo, bali huwavisha vazi la rehema na huwakaribisha kwenye nyumba ya utukufu na huwakalisha kwenye masofa ya furaha na itawakutanisha na manabii, na masiddiki,na mashahidi na watu wema, na hao ndio marafiki wema. Kisha itawaingiza katika kundi la waja walio karibu na Mwenyezi Mungu katika pepo za juu kabisa.

Hivyo, Qur'ani ni muwaidhi, na tatibu wa yale yaliyomo vifuani, yenye kuongoza kwenye njia iliyo nyooka na yenye kutoa rehema kwa idhini ya Mwenyezi Mungu aliye takasika. Bali tunaweza kusema kuwa inawaidhi, na kuponya yaliyomo vifuani, na inaongoza na kutoa rehema yenyewe na sio kwa amri ya yeyote, kwa sababu yenyewe ndio sababu kiunganisha kati ya Mwenyezi Mungu

na viumbe wake. Hivyo, Qur'ani ni mawaidha, na poza ya yaliyomo vifuani, na uongofu na rehema kwa waumini.

MAISHA KATIKA HIMAYA YA QUR'ANI

Kwa hakika nimeyapitia maisha nikiwa katika himaya ya Qur'ani na kiashi katika ulinzi wake kwa miaka kadhaa. Ujanani mwangu nilikuwa nikihitimisha Qur'ani mara ishirini mpaka mara ishini na moja kwa mwaka. Mpaka ilifikia hatua nyama yangu, na damu yangu, na fikra zangu, ulimi wangu na moyo wangu vikachanganyikana na Qur'ani. Lakini pia, pamoja na kuisoma, nilikuwa nikisoma kwa umakini tafsiri mbili za Qur'ani, ambazo mwenyewe ninakiri wazi kwamba, zilikuwa na mchango mkubwa katika kujenga shakhsia yangu kielemu na kifikra, tafsiri hizo ni *Al-Mizan* na *Fii dhilaalil Qur'an,* nilizisoma hadi nikazimaliza na nikaandika muhtasari wa vichwa vya habari vya fikra zilizomo ndani ya tafsiri hizo ili kuzirejea kila mara, na hivyo zile fikra hujapika akilini mwangu kama zilivyo kuwa nikinijia zile nyakati zenye kufurahisha.

Lakini kipi nilicho kipata katika himaya ya Qur'ani? na kipi atakacho kipata atakaye ishi katika ulinzi wake? Bila shaka atauona ukubwa na utukufu wa Mwenyezi Mungu aliye tukuka ukidhihiri katika aya zake, na katika sheria zake, na katika miongozo yake na uwezo wake juu ya kila kitu, kwani ardhi yote iko mikononi mwake, mbingu zitakunjwa katika mkono wake wa kulia, na utukufu wote ni wake, na ufalme ni wake peke yake, yeye ndiye anaye irithi ardhi na walio juu yake na kwake ndiko watarejeshwa waja, naye yuko karibu nao kuliko mshipa wa shingoni mwao, naye huingia kati ya mtu na moyo wake, na hakuna anaye miliki manufaa wala madhara kwa ajili ya kitu chochote isipokuwa kwa idhini yake. Basi kila kitu hudogeka mbele ya mbeba Qur'ani. Kila kisicho kuwa Mwenyezi Mungu hata kama dhahi yake itafikia adhama gani, au watawala na wafuasi wake wakamkuza na kumtukuza kiasi gani, lakini uwezo wa Mwenyezi Mungu utavimeza vyote walivyo vibuni, si Iram wenye majumba marefu, wala Firauni mwenye vigingi, wala watu wenye mahazina ambayo funguo zake hubebwa na watu wenye nguvu. Ama mtu wa Qur'ani nguvu yake imeunganika na nguvu ya Mwenyezi Mungu, hivyo hamuogopi asiye kuwa yeye. Mwenyezi Mungu anasema:

[مَثَلُ الَّذِينَ اتَّخَذُوا مِن دُونِ اللَّهِ أَوْلِيَاء كَمَثَلِ الْعَنكَبُوتِ اتَّخَذَتْ بَيْتًا وَإِنَّ أَوْهَنَ الْبُيُوتِ لَبَيْتُ الْعَنكَبُوتِ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ]

“Mfano wa wale waliofanya waungu asiyekuwa Mwenyezi Mungu, kama mfano wa buibui ajitandiaye nyumba, na bila shaka nyumba iliyo mbovu kuliko zote ni nyumba ya buibui, laiti wangelijua”[1] , na “mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu basi Mwenyezi Mungu atakifanya kila kitu kumuogopa”[1] .

na hapo ndipo utayaona hayo madola yenye nguvu ambayo: “zikaoenekana mbele yake, kwa uchawi wao zikienda mbio”[1] , na kuwa yanaweza kufanya kila yakitacho, yakiporomoka na kuyeyuka kama chumvi ndani ya maji, bila ya vita wala adui kudhihiri. Lakini Mwenyezi Mungu anakueleza sababu ya kuteketea kwao kwa kusema:

[فَأَتَى اللّهُ بُنْيَانَهُم مِّنَ الْقَوَاعِدِ فَخَرَّ عَلَيْهِمُ السَّقْفُ مِن فَوْقِهِمْ وَأَتَاهُمُ الْعَذَابُ مِنْ حَيْثُ لاَ يَشْعُرُونَ، ثُمَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ يُخْزِيهِمْ وَيَقُولُ أَيْنَ شُرَكَآئِيَ الَّذِينَ كُنتُمْ تُشَاقُّونَ فِيهِمْ قَالَ الَّذِينَ أُوتُواْ الْعِلْمَ إِنَّ الْخِزْيَ الْيَوْمَ وَالْسُّوءَ عَلَى الْكَافِرِينَ]

“Walifanya vitimbi wale walio kuwa kabla yao, basi Mwenyezi Mungu akayasukua majengo yao kwenye misingi, ndipo dari zikawaangukia kutoka juu yao na ikawafikia adhabu kutoka wasiko kujua. Kisha siku ya Kiyama atawahizi na atasema: Wako wapi hao washirika wangu kwa ajili yao mlikuwa mkigombana (na manabii?) Watasema wale walio pewa elimu: Hakika hizaya na msiba mkubwa leo vitawafikia makafiri”[1] .

Na ataiona ahadi ya Mwenyezi Mungu na utulivu wake kwa waumini kwamba mwisho mwema utakuwa wao, lakini hiyo ni baada ya:

[مَّسَّتْهُمُ الْبَأْسَاء وَالضَّرَّاء وَزُلْزِلُواْ حَتَّى يَقُولَ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ آمَنُواْ مَعَهُ مَتَى نَصْرُ اللّهِ أَلا إِنَّ نَصْرَ اللّهِ قَرِيبٌ]

“iliwapata shida na madhara na wakatikiswa hata mtume na wale walio amini pamaoja naye wakasema: Lini nusura ya Mwenyezi Mungu itakuja? Jueni kuwa

---

[1] Surat Al-ankabuut: 41.

[1] Man layhdhuruhu Alfaqiih: 4/410.

[1] Surat Taha: 66.

[1] Surat An-Nahli: 26-27.

nusura ya Mwenyezi Mungu ipo karibu."[١٠٣] , na ni lazima wapatwe na fitina na majaribu ili Mwenyezi Mungu awasafishe wale walio amini:

[ألم، أَحَسِبَ النَّاسُ أَن يُتْرَكُوا أَن يَقُولُوا آمَنَّا وَ هُمْ لا يُفْتَنُونَ، وَلَقَدْ فَتَنَّا الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ فَلَيَعْلَمَنَّ اللهُ الَّذِينَ صَدَقُوا وَلَيَعْلَمَنَّ الْكَاذِبِينَ]

"Alif Lam Mim,Je! Wanadhani watu wataachwa kwa kuwa wanasema: Tumeamini. Nao wasijaribiwe? Hakika tuliwajaribu walio kuwa kabla yao, na kwa yakini Mwenyezi Mungu atawatambulisha walio wa kweli na atawatambulisha walio waongo"[١٠٤] Hapo ndipo hali ya muumini hutulia, hata kama atawajihi ugumu na shida, kwani hiyo ndio kanuni ya Mwenyezi Mungu kwa waja wake, kwamba lazima muumini asimame imara katika matati na athibitishe ukweli na Imani yake, na Mwenyezi Mungu huwalipa wakweli, na atamrahisishia muumini yale yanayo msibu, kwa sababu muumini huwa katika ulinzi wa Mwenyezi Mungu aliye takasika. Mwenyezi Mungu anasema:

[فَإِنَّكَ بِأَعْيُنِنَا]

"Hakika wewe uko mbele ya macho yetu"[١٠٥] na:

[ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ لاَ يُصِيبُهُمْ ظَمَأٌ وَلاَ نَصَبٌ وَلاَ مَخْمَصَةٌ فِي سَبِيلِ اللهِ وَلاَ يَطَؤُونَ مَوْطِئًا يَغِيظُ الْكُفَّارَ وَلاَ يَنَالُونَ مِنْ عَدُوٍّ نَّيْلاً إِلاَّ كُتِبَ لَهُم بِهِ عَمَلٌ صَالِحٌ إِنَّ اللهَ لاَ يُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ]

"Hayo ni kwa sababu hawafikii kiu wala taabu wala njaa katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawakanyagi njia iwachukizayo makafiri, wala hawapati taabu yoyote kwa adui, ila huandikiwa kitendo chema. Hakika Mwenyezi Mungu haupotezi malipo ya watendao mema"[١٠٩]

Ataona ukubwa wa imani ambayo huujenga moyo na atayaona mafunzo ya juu ambayo inayabeba kwa wanadamu walio potea, wale ambao wanafuata sarabi

---

[١٠٣] Surat Al-Baqarah: 214.

[١٠٤] Surat Al-An'kabut: 1-3.

[١٠٥] Surat Tur: 48.

[١٠٩] Surat Tawba: 120.

(mazigazi) na kuishi kwa malengo mabaya, huku wakizitamisha nafsi zao kwa matamanio ya batili yanayo pendezeshwa kwao na wafuasi shetani, kama vile: mali, na vyeo na mambo ya anasa, wakivishindania na kupigana kwa vitu ambavyo havitadumu kwa ajili yao, na badala yake vitakuwa ni mzigo juu yao. Wanajifanyia waungu kasha huanza kuwaabudu na kuwatii na wanawapa mamlaka, basi huwafanyia waungu hao minasaba, na sherehe na makongamano, huwatolea makafara, sio tu ya wanyama bali hata ya binadamu na hutumia kwa waungu hao mabilioni ya fedha.

Kisha ataona kuwa hayupo peke yake kiasi cha kuhisi udhaifu, na udhalili, na kunyenyekea na kusalimu amri. Wala hatahisi kuwa matukio yanayo msibu, na anayo yashudia na kuyaishi ni kirojo na kwamba yeye ni wapekee. Mwenyezi Mungu anasema:

[قُلْ مَا كُنتُ بِدْعاً مِّنْ الرُّسُلِ وَمَا أَدْرِي مَا يُفْعَلُ بِي وَلا بِكُمْ إِنْ أَتَّبِعُ إِلا مَا يُوحَى إِلَيَّ وَمَا أَنَا إِلا نَذِيرٌ مُّبِينٌ]

"Mimi si kiroja miongoni mwa mitume. Wala sijui nitakavyo fanywa wala nyinyi. Mimi sifuati ila yaliyo funuliwa kwangu, wala mimi siye ila ni muonyaji dhahiri"[١] . Hivyo mitume wakubwa na mawalii wema wamekwisha mtangulia kwenye njia hii, hali kadhalika wabeba ujumbe wa Mwenyezi Mungu, na wasuluhishi na waja wema, wote walikabiliwa na haya yanayo mkabili, wakafanya subira kubwa, na wakakabiliwa na jamii zao kwa makubwa kuliko, lakini radiamali yao ilikuwa kama anavyo iakisi Mwenyezi Mungu katika aya hii:

[فَمِنْهُم مُّهْتَدٍ وَكَثِيرٌ مِّنْهُمْ فَاسِقُونَ]

"Basi wengi wao ni waongofu na wengi wao ni waasi"[١] . Kisha akasema:

[يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ عَلَيْكُمْ أَنفُسَكُمْ لاَ يَضُرُّكُم مَّن ضَلَّ إِذا اهْتَدَيْتُمْ]

"Enyi mlio amini! Lililo lazima juu yenu ni nafsi zenu. Hawakudhuruni walio potoka ikiwa nyinyi mmeongoka"[١] .

[١] Surat Al-Ah'qaaf: 9.

[١] Surat Al-Hadid: 26.

[١] Surat Al-Maidah: 105.

Ndani ya Qur'ani ataona namna Mwenyezi Mungu alivyo mtukuza mwanadamu pindi alipo wazungumzisha yeye mwenyewe na akawaelekezea maneno yake moja kwa moja. Mwenyezi Mungu aliye tukuka ndiye muumba wa mbingu na ardhi, mwenye majina mazuri, ndiye anaye upeleka ujumbe kwao na kuwapa ahadi yake. Ni utukuzaji upi ulio bora kuliko huu ambao Mweneyzi Mungu anasema:

[وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَرَزَقْنَاهُم مِّنَ الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَى كَثِيرٍ مِّمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلاً]

"Na hakika tumewatukuza wanadamu na tumewabeba nchi kavu na baharini, na tumewaruzuku katika vitu vizuri, na tumewatukuza kuliko wengi wa wale tulio waumba, kwa utukufu mkubwa"[١١٣] . Unadhani ni nini zitakuwa hisia[١١٤] za mwanadamu hali ya kuwa akiusoma ujumbe wa mpendwa wake, tena mpendwa asiye na ukomo, "hakika Qura'ni ni agano la Mwenyezi Mungu kwa viumbe wake, hivyo inafaa kwa kila muumini kuingalia kilichoko ndani ya ahahi hiyo"[١١٥] .

Vile vile atakiona kila katika ulimwengu huu ikikiwa kwa kiwango maalumu na hesabu makini, Mwenyezi Mungu: "Kwa hakika sisi tumekiumba kila kitu kwa kipimo"[١١٦] , "wala sisi hatukiteremshi isipokuwa kwa kipimo maalumu"[١١٧] , " Nasi tumeweka mizani ya uadilifu"[١١٨] , na viumbe vyote kikiwa pekee au kwa makundi hufuata kanuni madhubuti za Mwenyezi Mungu: "nyendo wa wale walio kuwa kabla yenu"[١١٩] na:

[وَمَا مِن دَآبَّةٍ فِي الأَرْضِ وَلاَ طَائِرٍ يَطِيرُ بِجَنَاحَيْهِ إِلاَّ أُمَمٌ أَمْثَالُكُم مَّا فَرَّطْنَا فِي الكِتَابِ مِن شَيْءٍ ثُمَّ إِلَى رَبِّهِمْ يُحْشَرُونَ]

[١١٣] Surat Al-Isaraa: 70.

[١١٤] Al-Kafii: 2/609, mlango wa fii qiraatihi, hadithi: 1.

[١١٥] Surat Al-Qamar: 49.

[١١٦] Surat Al-Hij'ri: 21.

[١١٧] Surat Al-Anbiyaa: 47.

[١١٨] Surat An-Nisaa: 26.

“Na hapana mnyama katika ardhi, wala ndege anaye ruka kwa mbawa zake mbili, ila ni umma kama nyinyi. Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote. Kisha watakusanywa kwa Mola wao Mlezi”[١١٨] .

Hivyo, hakuna awezaye kutoka nje ya kanuni hii madhubuti ya Mwenyezi Mungu: “Basi hutapatamabadiliko katika kawaida ya Mwenyezi Mungu, wala hautakuta mageuko katika kawaida (mwendo) ya Mwenyezi Mungu”[١١٩] . Basi ni vipi mwanadamu amwabudu asiye kuwa Mwenyezi Mungu wakati hawezi kutoka mkono wa kawaida na kanuni zake! Hapa si sehemu ya kufanya mchezo wala upuzi: “Ewe Mola wetu mlezi! Hakika hukuviumba hivi bure, utukufu ni wako”[١٢٠] , “Na sikuumba majini na watu ila wapate kuniabudu”[١٢١] , “Kama tungali taka kufanya mchezo, hakika tungeufanya Sisi wenyewe, lau tungeli kuwa ni wafanyao mchezo”[١٢٢] . Wala hakuna nafasi ya kusema kwamba vitu vilijitokeza tu bila ya kuwepo aliye vifanya vitokee, jambo ambalo walilishikilia mulhidina (wasio amini uwepo wa Mwenyezi Mungu) dhidi ya kanuni za Mwenyezi Mungu, na wakazicheka kwalo akili za watu kwa muda mrefu, na wakawapotosha wengi, hakaki ameangamia mpotoshaji na mpotoshwaji. Kwani kuumbwa kwa mwanadamu kuna lengo ambalo ndio mwanadamu huyo anapaswa kuishi kwalo na kutumia kipawa na nguvu zake ili kulifanikisha lengo hilo. Na lengo si lingine ila Mwenyezi Mungu aliye tukuka.

Mwenye kuiweka Qur’ani maishani mwake, atakuta ndani yake ahadi ya Mwenyezi Mungu kumsaidia kwa nguvu ya ghaibu katika kila tukio, na katika shida na katika mtengo na vita dhidi ya nafsi yenye kuamrisha maovu au dhidi ya shetani, na atamkuta Mwenyezi Mungu akiwa naye, na Mwenyezi Mungu

---

١١٨. Surat Al-An’aam: 38.

١١٩. Surat Al-Faatir: 43.

١٢٠. Surat Al-Imraan: 191.

١٢١. Surat Adh-Adhariyaat: 56.

١٢٢. Surat Al-Anbiyaa: 17.

anatosha kuwa mtetezi wake bora kabisa madaamu atakuwa na naye. Anasema Mwenyezi Mungu:

[إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللهُ ثُمَّ اسْتَقَامُوا تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ الْمَلائِكَةُ أَلا تَخَافُوا وَلا تَحْزَنُوا وَأَبْشِرُوا بِالْجَنَّةِ الَّتِي كُنتُمْ تُوعَدُونَ، نَحْنُ أَوْلِيَاؤُكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الآخِرَةِ وَلَكُمْ فِيهَا مَا تَشْتَهِي أَنفُسُكُمْ وَلَكُمْ فِيهَا مَا تَدَّعُونَ، نُزُلا مِّنْ غَفُورٍ رَّحِيمٍ، وَمَنْ أَحْسَنُ قَوْلاً مِّمَّن دَعَا إِلَى اللهِ وَعَمِلَ صَالِحاً وَقَالَ إِنَّنِي مِنَ الْمُسْلِمِينَ]

“Hakika wale wanosema: Mola wetu mlezi ni Mwenyezi Mungu! Kisha wakanyooka sawa, hao huwateremkia Malaika wakawaambia: Msiogope, wala msihuzunike; na furahieni Pepo mliyo kuwa mkiahidiwa. Sisi ni walinzi wenu katika maisha ya dunia na katika Akhera, na humo mtapata kinacho tamaniwa na nafsi zenu, na humo mtapata mtakavyo vitaka. Ni takrima itokayo kwa Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu. Na ni nani asemaye kauli bora zaidi kuliko aitaye kwa Mwenyezi Mungu na kufanya vitendo vizuri na akasema: Hakika mimi ni miongoni watii (waislamu)?”[۱۲۶] , na aya ziko nyingi zinazo elezea kuٹeremkiwa nyoyo za waumini na utulivu, na kushuka msaada wa malaika wenye kushambulia kwa nguvu nk.

Lakini pia mwenye kuishi katika himaya ya Qur’ani atapata utulivu. Mwenyezi Mungu anasema: “Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu, nyoyo hutulia”. Atapata poza ya yale yaliyomo katika vifua, na muongozo, na baraka na kila kheri ambayo Qur’ani imejifu nayo.

Hivyo, msomaji wa Qur’ani na mwenye kuiweka maishani mwake, akishayapata yote, azma yake huimarika, na moyo wake hupata nguvu, na nafsi yake husafika, na wakti huo huo hima yake huzidi na hekima yake hudhihirika. Akishafikia hapo, huwa ni chanzo na chemchem ya kheri kwake na kwa jamii nzima kama ilivyo sifa ya wasuluhishi wakubwa, wakiongozwa na bwana mtume (s.a.w.w) na Amirul muuminina (a.s).

UDHARURA WA KURUDI KWENYE QUR’ANI

Sidhani kama baada ya ufafanuzi huo tutakuwa na haja ya kuendelea kutaja sababu za ziada zinazo tusukuma kurudi kwenye Qur’ani na kuishi katika himaya

[۱۲۶] Surat Fussilat: 30-33.

yake. Kwani sidhani kama yupo ambaye hajatambua hasara mbaya iliyo tupata kwa sababu ya kuipa mgongo Qur'ani. Hivyo, sote kwa pamoja na turejee kwenye Qur'ani, tutubie na jukutia na tuiombe ili nayo ikubali kurudi kutuongoza kuelekea kwa Mwenyezi Mungu aliye tukuka. Ni juu yetu tufikirie njia itakayo kitoa kitabu hiki kwenye hali ya kutegwa tuliyo isababisha sisi wenyewe na hatimaye tuirejeshee nafasi yake katika maishani na katika jamii.

Unaweza ukasema: Mbona jambo hilo ulisemalo limeshatekelezeka! Kwani tunashuhudia vipindi mbali mbali vya kufundisha Qur'ani, kuhifadhi, kusoma tajuwidi, hata kubainisha hukumu zake na uandishi wake.

Niseme kuwa: pamoja na kuyaheshimu hayo yote, ila huko ni kuyapa umuhimu maganda wakati jambo muhimu ni kilicho ndani ya maganda hayo. Kwa sababu kama ilivyo tangulia huko nyumba kwamba, matamshi ni chombo na zana ya kufikishia maana, na ni ganda linalo hifadhi maana ambayo ndio kiini na lengo, lakini pia neno ni ala ya kuhamishia maana kwenda akilini. Sasa je tutosheke na maganda na tuache kilicho ndani yake? Kinacho tafutwa ni kuirejesha Qur'ani kwa uhalisia wake, na kwa madhumuni yake, na kwa maana zake, na fikra zake na mafunzo yake. Ndio, ni kweli kwamba hatua ya kwanza ya kuliendea hilo, ni kuisoma Qur'ani, na kufahamu maana za maneno yake na kuzitumia kanuni za lugha ya Kiarabu kwenye matokeo ya herufi zake.

MAJUKUMU YA VYUO VYA DINI KATIKA KUIRESHA QUR'ANI MAISHANI

Ninaamini kuwa kundi la kwanza kabisa katika jamii lenye majukumu hayo ni hauza tukufu (vyuo vya kidini), wanafunzi wake, na wasomi wake na wakhatibu wake, kwa sababu kusalika na kuimarika kwa jamii kutategema kusalimika na kuimarika kwa hauza, na kuharibika kwa jamii kunategemea kuharibika kwa hauza pia -Mwenyezi Mungu apishe mbali-. Imekuja katika hadithi kutoka kwa bwana mtume (s.a.w.w) kwamba: "Makundi mawili katika umma wangu akiimarika umeimarika umma wangu, na yakiharibika umeharibika umma wangu". Akaulizwa: Ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ni akina nani hao? Akasema(s.a.w.w): "Ni wanazuoni na watawala"[١] .

[١] Al-Khisal: milango y ail-ithnain, hadithi: 12.

Hakika nimesema katika baadhi ya maandiko yangu[١] kuwa: Inahuzunisha sana kuona Qur'ani inakosa uwepo wake katika mitaala ya masomo ya hauza, kwani zimetungwa kwa namna ambayo mwanafuzi hahitaji kubobea katika Qura'ni tangu mwanzo wa masomo yake hadi anamaliza, na haipitii Qur'ani ipokuwa baadhi ishara kidogo pindi inapothibitishwa moja ya kanuni za Kinahau, au katika bahathi ya Kiusuli au katika masiala ya Kifikihi. Hivyo, mwanafunzi amekuwa ni mhanga wa mambo yanayo hitaji akili sana wakati hajapata chakula cha moyo, na roho na hajapata poza na tiba ya nafsi. Bali imefikia hatua mwanahauza anafikia kiwango cha juu katika Fikihi na Usuli hali ya kuwa hajawahi kuyaishi maisha ya Qur'ani wala hajawahi kupata tajiriba ya namna ya kuamiliana nayo na akaifahamu kama ujumbe wa isilahi na kurekebisha. Masiku, hata mawiki yanaweza kupita bila kumuona mwanafunzi akichukua Msahafu asome aya zake na kutafakari maana zake kwa sababu ya kukosekana mahusiano ya kina ya kiroho baina yake na Qur'ani, ambapo kama angelipata ndani yake chakula inayo mtosheleza kuliko kitu kingine, bila shaka asingeli iacha. Na huu ndio msiba mkubwa wa hauza (vyuo vya dini) na jamii, kiasi kwamba imefikia hata ukawaona baadhi yao hawawezi hata kuisoma vizuri Qur'ani licha kuwa na shakli zake.

Hivyo basi, kwa kuwa majukumu yanayo bebwa na hauza ni kurekebisha jamii na kuiweka karibu na Mwenyezi Mungu, kuifahamu Qur'ani na kupigania kuiweka katika maisha ya jamii ndio wajubu wake nambari moja. Kwani kheri ya umma haitapatikana ila kwa kushikamana na Qur'ani, na kuongoka kwa uongofu wake na kuangaza kwa nuru yake, kama ilivyo sema hadhithi mashuhuri ya Thaqalayni:

(إني تارك فيكم الثقلين كتاب الله وعترتي أهل بيتي ما إن تمسكتم بهما لن تضلوا بعدي أبداً)

"Hakika Mimi nimekuachieni viziti viwili: kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu, Ahlul-bayt wangu. Iwapo mtashikamana navyo, kamwe hamtapotea baada yangu"[١] .

UJAHILIA WA KILEO

[١٣٦] Wasia na nasaha kwa makhatibu na wanafunzi wa hauza (yamekwisha tangulia ndani ya juzuu hii)

[١٣٧] Tumekwishaitaja huko nyumba.

Wanadamu leo hii wanauishi ujahilia mpya –hata kama baadhi yao watajiiata waislamu– kwa mujibu wa maana ya ujahilia inayo tolewa na Qur'ani. Kwa sababu Qur'ani haiuhesabu ujahilia kuwa ni kipindi maalumu kilicho malizika kwa kudhihiri Uislamu, bali ujahilia kwa mtazamo wa Qur'ani, ni hali ya kijamii inayo ukumba umma na jamii ikabadilika na kusifika kwa sifa ile, kwa sababu ya kuupa na kuacha sheria ya Mwenyezi Mungu aliye takasika:

[أَفَحُكْمَ الْجَاهِلِيَّةِ يَبْغُونَ وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ اللهِ حُكْماً لِّقَوْمٍ يُوقِنُونَ]

"Je wanataka hukumu ya kijahili? Na nani aliye mwema kuliko Mwenyezi Mungu katika hukumu kwa watu wenye yakini?"[١] . Hali kadhalika Qur'ani imeeleza [٢] uwepo wa ujahahilia pale iliso sema:

[وَلا تَبَرَّجْنَ تَبَرُّجَ الْجَاهِلِيَّةِ الأُولَى]

"*Wala msijishauwe kwa mishauwo ya kijahilia ya kizamani*"[١] , kana kwamba ilikuwa ni ishara ya uwepo wa ujahilia mpya, ambao ndio huu wanao ishi wanadamu leo hii katika shari yake, na maangamizi yake na uovu wake.

Bali ujahilia wa leo umekusa mabaya yote ya ujahilia wa nyuma, mwenye nguvu amekuwa akimnyonya mnyonge, na ushoga umekuwa unatungiwa kanuni zinazo uruhusu na kujuzisha kuowana wanaume, na uzinzi unaenea kila mahali, wakati maradhi yake yaangamizayo kama vile: ukimwi na mfano wake yamesambaa ulimenguni kote, na upunjaji katika vipimo na vizani umezagaa kwa aina zake mbali mbali, kwa kiwango cha mtu mmoja mmoja bali hata kwa kiwango mataifa. Kumekuwa hakuna uadilifu katika mahusiano kati ya jamii ya kibinadamu, hadi wanafikia kuyaita mahusiano hayo kuwa ni: 'Kibaba kwa vibaba viwili'. Na makasisi, na wamonaki na viongozi wengine wa upotovu katika mashetani, na wanadamu na majini baadhi yao wakiwafundisha wengine maneno ya kupambapamba kwa udanganyifu, wamefanywa kuwa waungu badala ya Mwenyezi Mungu, wamekuwa wakiharamisha yale yaliyo halalishwa na wakihalalisha yale yaliyo haramishwa. Na sasa miungu ambao huabudiwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu aliye takasika imekuwa haina idadi tena, imekuwa

---

[١] Surat Al-Maidah: 50.

[٢] Surat Al-Ahzaab: 33.

haishii kwenye ya mawe tu, bali kila kukicha akili za kishetani zimeendelea kuafikiana kuongeza miungu wengine. Huku mashetani watu na majini nao wakuiendelea kufundishana wao kwa wao maneno ya kupambapamba na wakizuwia njia ya Mwenyezi Mwenyezi iliyo nyooka:

[لأَقْعُدَنَّ لَهُمْ صِرَاطَكَ الْمُسْتَقِيمَ، ثُمَّ لآتِيَنَّهُم مِّن بَيْنِ أَيْدِيهِمْ وَمِنْ خَلْفِهِمْ وَعَنْ أَيْمَانِهِمْ وَعَن شَمَآئِلِهِمْ وَلاَ تَجِدُ أَكْثَرَهُمْ شَاكِرِينَ]

"Akasema: Kwa sababu umenihukumu mpotofu, basi nitawavizia (waja wako) katika njia yako iliyo nyooka. Kisha nitawafikia kwa mbele yao na nyuma yao na kuliani kwao na kushotoni kwao, na wengi katika wao hutawakuta ni wenye shukuru"[١٣] na:

[وَلاَ تَقْعُدُواْ بِكُلِّ صِرَاطٍ تُوعِدُونَ وَتَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللهِ مَنْ آمَنَ بِهِ وَتَبْغُونَهَا عِوَجاً](الأعراف:٨٦)،

" *Wala msikae katika kila njia kuogopesha watu, na kuwazuilia na njia ya Mwenyezi Mungu wale wenye kumuamini, na mkataka kuipotosha*"[١٤] . Na wingi ulioje wa watu hawa wanao ziwilia na njia ya Mwenyezi Mungu wale walio amini na wanataka kuipotosha kutoka na maumbile salama, kuanzia kwa machangudoa walio tega mitego ya fitina na udanganyifu, ukija kwenye hisa za kiuchumi ambazo hadi huudondosha udenda, kisha uje kwa wasanii ambao hawana kazi zaidi ya kuharibu tabia na maadili ya kijamii nk.

Yote hayo ni katika sifa na alama za ujahili wa leo na ujahili wa kila zama na kila sehemu. Hii ni moja ya maana za Qur'ani ambazo ni lazima zifahamike na kutambuliwa.

Na hili kulifafanua hili ipasavyo, ninafanya ulinganishaji baina ya itikadi na matendo ya ujahilia wa kizamani na ujahilia wa kileo ambao tunauishi, na hapa nitabainisha mambo yafuatayo:

١. Kuchambua maana na misamiti ya Kiqur'ani na kunyambua maana zake ambazo Qur'ani ilizitaka, na kuondoa utando ulio zizunguka kwa sababu ya kughafilika na Qur'ani, na kutumia akili zetu kabla ya kuirejea.
٢. Kuidiriki haja ya Qur'ani pindi tunapo fahamu kuwa wanadamu wamerudi kwenye ujahilia wao wa zamani, na hivyo wana haja ya kwenye Qur'ani ili

[١٣] Surat Al-A'araaf: 16-17.

[١٤] Surat Al-A'araaf: 86.

itekeleze jukumu lake kwa mara nyingine katika kuwaleta kwenye Uislamu halisia.

٣. Kukomaza fikra ya Imamu Al-Mahdi (a.s) na ili kujenga hoja ya kielemu kwenye fikra hiyo, kwa kuwa baada ya wanadamu kurudi kwenye ujahilia wao wa zamani, Qur'ani pekee ndiyo yenye uwezo wa kuwaokoa kwa kutekeleza jukumu lake. Pia ni lazima awepo masimamizi atakaye isimamia katika utekelezaji wa majukumu yake, kama vile mtume (s.a.w.w). ama katika kipindi hiki ambacho hakuna mtume, kwa sabau utume ulishia kwake (s.a.w.w), na hatuna mtu ambaye amekusanya sifa hizo isipokuwa Alhoja bin Alhasani (a.s), na sasa hizi ni alama za kudhihiri kwake na siku iliyo ahidiwa inakaribia[١] . Maelezo zaidi kumhusu Imanu Al-Mahdi (a.s) yana sehemu yake maalumu.

SIFA ZA JAMII YA KIJAHILIA KWA MUJIBU WA QUR'ANI

Sifa ya kwanza miongoni mwa sifa za kijahilia ni kuwaabudu watu badala ya Mwenyezi Mungu aliye tukuka. Na ibada maana yake ni kutii na kutawalisha kama ilivyo pokelewa kutoka kwa Ahlul-bayt (a.s) katika tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu:

[اتَّخَذُواْ أَحْبَارَهُمْ وَرُهْبَانَهُمْ أَرْبَاباً مِّن دُونِ اللهِ وَالْمَسِيحَ ابْنَ مَرْيَمَ وَمَا أُمِرُواْ إِلاَّ لِيَعْبُدُواْ إِلَهاً وَاحِداً لاَّ إِلَهَ إِلاَّ هُوَ سُبْحَانَهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ]

"Wamewafanya makuhani wao na wamonaki wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu, na Masihi mwana wa Mariam. hali hawakuamrishwa isipokuwa wamuabudu Mwenyezi Mungu Mmoja, hapana mungu ila Yeye. Ametakasika na hayo wanayo mshirikisha nayo"[٢] . Alisema (a.s): [٣]

---

[١] Ndio maana katika hadithi imekuja kwamba Imamu Al-Mahdi (a.s) natakuja a Uislamu mpya na Qur'ani mpya. Na hii haina maana kwamba atakuja na mafunzo yaliyo nje na Uislamu au na Qur'ani ya babu yake bwana mtume (s.a.w.w), bali kinacho kusudiwa ni kwamba ataondoa utando uliopo kwenye Qur'ani hii na kuirudisha kwenye maishani kwa mara nyingine.

[٢] Surat At-Tawbah: 31.

(أما والله ما دعوهم إلى عبادة أنفسهم، ولو دعوهم ما أجابوهم، ولكن أحلوا لهم حراما، وحرموا عليهم حلالا فعبدوهم من حيث لا يشعرون)

"Wallah! Hawakuwaita wawaabudu wenyewe, na laiti wangeli waita kwa hilo wasingeli wakubalia, lakini waliwahalalishia haramu, na wakawaharamishia halali, wakawaabudu bila ya wenyewe kujua"[١] . Hii ni aina ya ibada ya asiyekuwa[٣] Mwenyezi Mungu iliyokuwa katika jamii ile ya kijahilia, na ndio sababu sura ya kwanza ya Qur'ani iliyo teremka ilikuja kuwataka kuuacha kumtii asiyekuwa Mwenyezi Mungu: "Akome! Usimtii"[١] . Wakati ule kulikuwa na utii wa miungu wengi:

[مَا نَعْبُدُهُمْ – أي الأصنام – إلا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى اللَّهِ زُلْفَى]

"Hatuwaabudu –masanamu– isipokuwa wapate kutujongeza kwa Mwenyezi Mungu"[١] , [٣] [٦]

[وَلاَ يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضاً أَرْبَاباً مِّن دُونِ اللهِ]

"Wala baadhi yetu wasiwafanye baadhi kuwa waungu badala ya Mwenyezi Mungu"[١] , [٣] [٧]

[إِنَّا أَطَعْنَا سَادَتَنَا وَكُبَرَاءنَا فَأَضَلُّونَا السَّبِيلا]

"Mola wetu! Hakika tumewatii mabwana wetu na wakubwa wetu, nao ndio walio tupoteza njia"[١] , [٣]

[فَاتَّبَعُواْ أَمْرَ فِرْعَوْنَ وَمَا أَمْرُ فِرْعَوْنَ بِرَشِيدٍ]

"Wao wakafuata amri ya Firauni, na amri ya Firauni haikuwa yenye uongofu"[١] ,

[فَخَلَفَ مِن بَعْدِهِمْ خَلْفٌ أَضَاعُوا الصَّلَاةَ وَاتَّبَعُوا الشَّهَوَاتِ فَسَوْفَ يَلْقَوْنَ غَيّاً]

---

[١٣٤] Al-Kafii" 1/53, mango wa At-Taqliid, hadithi: 1.

Msamiati huu muhimu wa Qur'ani, yaani: (ibada) unahitaji kufafaniliwa vizuri, kwa sababu haufahamiki vyema katika vichwa vya jamii. Wamekuwa wakidhani kuwa maana ya ibada ni kusali au kusujudu tu, na sio kutii. Ndio utawakuta hawaoni kuwa ni tatizo katika dini yao kusali na kufungu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wakati huo huo miamala na matendo yao wanavifanya kinyume na yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu. Na huu ni ufahamu hatari sana, ambapo hatuna budi kuuondoa utata huu katika jamii. Imekuja katika hadithi kutoka kwa Imamu Jawad (a.s) kwamba alisema: "Yeyote atakaye msikiliza msemaji, basi atakuwa amemuabudu, ikiwa msemaji huyo ataongea katoka kwa Mwenyezi Mungu, basi atakuwa amemuabudu Mwenyezi Mungu, na ikiwa msemaji huyo atasema kutoka kwa Ibilisi…". Tuhaful U'quul, Uk: 336.

[١٣٥] Surat Al-A'laq: 19.

[١٣٦] Surat Az-Zumar: 3.

[١٣٧] Surat Al-Imran: 64.

[١٣٨] Surat Al-Ahzab: 67.

[١٣٩] Surat Hud: 97.

“Lakini wakaja baada yao walio wabaya, wakaacha sala, na wakafuata matamanio. Basi watakuja kuta malipo ya ubaya”[١٤٤] ,

[وَإِذَا قِيلَ لَهُمُ اتَّبِعُوا مَا أَنزَلَ اللهُ قَالُواْ بَلْ نَتَّبِعُ مَا أَلْفَيْنَا عَلَيْهِ آبَاءنَا أَوَلَوْ كَانَ آبَاؤُهُمْ لاَ يَعْقِلُونَ شَيْئاً وَلاَ يَهْتَدُونَ]

“Na wanapo ambiwa: Fuateni aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu; wao husema: Bali tutafuata tuliyo wakuta nayo baba zetu. Je, hata ikiwa baba zao walikuwa hawaelewi kitu, wala hawakuongoka?”[١٤٥] ,

[وَمِنَ النَّاسِ مَن يُجَادِلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَيَتَّبِعُ كُلَّ شَيْطَانٍ مَّرِيدٍ، كُتِبَ عَلَيْهِ أَنَّهُ مَن تَوَلاهُ فإنه يُضِلُّهُ وَيَهْدِيهِ إِلَى عَذَابِ السَّعِيرِ]

“Na miongoni mwa watu wapo wanao bishana juu ya Mwenyezi Mungu bila ya ilimu, na wanamfuata kila shet'ani aliye asi. Ameandikiwa kwamba anaye mfanya kuwa rafiki, basi huyo hakika atampoteza na atamwongoza kwenye adhabu ya Moto mkali”[١٤٦] ,

[إِذْ جَعَلَ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي قُلُوبِهِمُ الْحَمِيَّةَ حَمِيَّةَ الْجَاهِلِيَّةِ]

“Wale walio kufuru walipotia nyoyoni mwao hasira, hasira za kijinga (za kijahilia)”[١٤٧] .

Hawa ni baadhi ya miungu wa enzi za ujahilia wa zamani waliokuwa wakiabudiwa badala ya Mwenyezi Mungu aliye tukuka. Miungu ambao walikuwa ni: masanamu, wasomi wasio na nyoyo safi, watawala, matamanio ya nafsi iamrishayo maovu, Ibilisi, hasira na ada walizo zirithi kutoka kwa mababa zao. Lakini msingi wa yote hayo ulikuwa ni kufuata matamanio:

[فَإِن لَّمْ يَسْتَجِيبُوا لَكَ فَاعْلَمْ أَنَّمَا يَتَّبِعُونَ أَهْوَاءهُمْ وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّنِ اتَّبَعَ هَوَاهُ بِغَيْرِ هُدًى مِّنَ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ لا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ]

“Na ikiwa hawakukujibu, basi jua kuwa wanajifuatia tu matamanio yao. Na nani aliyepotea zaidi kuliko yule anayefuatia matamanio yake pasipo muongozo utokao kwa Mwenyezi Mungu? Bila shaka Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhalimu”[١٤٨] .

---

[١٤٤] Surat Maryam: 59.

[١٤٥] Surat Al-Baqarah: 170.

[١٤٦] Surat Al-Hajj: 3-4.

[١٤٧] Surat Al-Fat’hi: 26.

[١٤٨] Surat Al-Qasas:50.

Lakini je hali ya watu wa leo hii imebadilika? Na hapa sikusudii wale watu wanaojiita kuwa wameendelea, kwani ni wazi kuwa wao wamezama zaidi katika dimbwi la ujahilia kuanzia kichwani kadi miguuni, bali ninakusudia wale wajiitao waislamu hali ya kuwa wamepanda jahazi la hao hao makafiri. Waislamu ambao wamezama katika kuyatii matamanio na kila kinacho amrishwa na miungu wao wapya kama vile: michezo, Sanaa na baadhi ya nadharia na kanuni zenye kupotosha. Leo hii bado amri za mabwana na wakubwa kama vile: kiongozi wa ukoo au watu wenye vyeo umekuwa unatekelezwa bila hata kuchunga mipaka ya sharia ya Mwenyezi Mungu, wamekuwa akihalalisha yale yaliyo haramishwa na Mwenyezi Munngu na kuharamisha yale aliyo yaharamisha. Hali kadhilika mila na ada za mababa na mababu zimeendelea kuheshimiwa kuliko sheria za Mwenyezi Mungu, kiasi kwamba jamii iko radhi kumuasi Mwenyezi Mungu kuliko kuachana na mila na desturi hizo. Kana kwamba ndimi zao zinasema: "Moto ni mora kuliko udhalili", kunyume kabisa na Uislamu alioudhirisha Imamu Hussein (a.s) katika ardhi ya Karbala, pindi aliposema:

الموت أولى من ركوب العار والعار أولى من دخول النار

Kufa ni bora kuliko kuukubali udhalili***na udhalili ni bora kuliko kuingia motoni

Jambo hili la kufadhilisha mida na desturi za mababa na mababu niko wazi katika mwenendo wa watu wanaoshi kimakoo na wengineo. Ama mwanamke amekuwa ni wakutii mapenzi, na kwenda kwenye maduka ya mavazi na kufuata usasa na kila kinacholetwa wamagharibi, mfano: mavazi na vipodozi hata kama vitakuwa vinaenda kinyume na sheria ya Mwenyezi Mungu. Sasa ikiwa hali ndio hii, je kuna aina yoyote ile ya ibada na utii vilivyosalia na havifanyi na jamii ya kileo? Hii ni kwa kiwango cha shirki ya wazi wazi. Na Qur'ani inatujulisha kwa miungu wote siku ya Kiyama watawakana waliowaabudu. Lakini siku hiyo majuto yao hayatawanufaisha kitu:

[وَمِنَ النَّاسِ مَن يَتَّخِذُ مِن دُونِ اللهِ أَندَاداً يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ اللهِ وَالَّذِينَ آمَنُواْ أَشَدُّ حُبّاً لِّلهِ وَلَوْ يَرَى الَّذِينَ ظَلَمُواْ إِذْ يَرَوْنَ الْعَذَابَ أَنَّ الْقُوَّةَ لِلهِ جَمِيعاً وَأَنَّ اللهَ شَدِيدُ الْعَذَابِ، إِذْ تَبَرَّأَ الَّذِينَ اتُّبِعُواْ مِنَ الَّذِينَ اتَّبَعُواْ وَرَأَوُاْ الْعَذَابَ وَتَقَطَّعَتْ بِهِمُ الأَسْبَابُ، وَقَالَ الَّذِينَ اتَّبَعُواْ لَوْ أَنَّ لَنَا كَرَّةً فَنَتَبَرَّأَ مِنْهُمْ كَمَا تَبَرَّؤُواْ مِنَّا كَذَلِكَ يُرِيهِمُ اللهُ أَعْمَالَهُمْ حَسَرَاتٍ عَلَيْهِمْ وَمَا هُم بِخَارِجِينَ مِنَ النَّارِ]

“Na miongoni mwa wako wanaowafanya miugu wasiokuwa Mwenyezi Mungu Wanawapenda kama kumpenda Mwenyezi Mungu kuwa ni washirika na wakiwapenda kama kumpenda Mwenyezi Mungu. Lakini walio amini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi. Na walio dhulumu wangelijua watakapo iona adhabu kuwa nguvu zote ni za Mwenyezi Mungu na kuwa Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu. Walio fuatwa watakapo wakataa wale walio wafuata, na hali ya kuwa wamekwisha iona adhabu; na yatakatika mafungamano yao”[١٤٥] .

Sehemu nyingine Qur’ani inawaelezea miungu hawa ambao huabudiwa na wanadamu kwa kuwapa mamlaka na utiifu badala ya Mwenyezi Mungu kwa musema:

[مَثَلُ الَّذِينَ اتَّخَذُوا مِن دُونِ اللهِ أَوْلِيَاء كَمَثَلِ الْعَنكَبُوتِ اتَّخَذَتْ بَيْتًا وَإِنَّ أَوْهَنَ الْبُيُوتِ لَبَيْتُ الْعَنكَبُوتِ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ]

“Mfano wa wale walio waliowafanya waungu asiyekuwa Mwenyezi Mungu, ni mfano wa buibui ajitandiaye nyumba. Na hakika nyumba dhaifu mno kuliko zote ni jumba la buibui, laiti wangelijua”[١٤٦] na inasema sehemu nyingine:

[وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَعْمَالُهُمْ كَسَرَابٍ بِقِيعَةٍ يَحْسَبُهُ الظَّمْآنُ مَاءً حَتَّى إِذا جَاءهُ لَمْ يَجِدْهُ شَيْئاً وَوَجَدَ اللَّهَ عِندَهُ فَوَفَّاهُ حِسَابَهُ وَاللَّهُ سَرِيعُ الْحِسَابِ]

“Na wale waliokufuru vitendo vyao ni kama mazigazi uwandani. Mwenye kiu huyadhania ni maji, hata akiyaendea hapati chochote. Na humkuta Mwenyezi Mungu hapo, naye humpa hisabu yake sawa sawa. Na Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhesabu”[١٤٧]

---

[١٤٥] Surat Al-Baqarah: 165-166.

[١٤٦] Surat Al-A’nkabut: 41.

[١٤٧] Surat An-Nur: 39.

Kimsingi hii bahathi inayofaa umuhimu, kwani huwazindua wanadamu wauone upungufu wa imani na itikadi zao na kwamba waone ni namna gani walivyojitenga na tauhidi (kumpwekesha Mwenyezi Mungu) ya kweli na kwamba utiifu wako kwa Mwenyezi Mungu umeshuka kuliko wa wanavyo watii waungu hawa mbali mbali. Bahathi hii inafaa hata tukaiita kwa jina "Masanamu ya ujahilia wa kileo", masanamu ambayo hatari imefichikana hadi kwa waumini achilia mbali wasiokuwa wao.

Ama tukija kwa kile kijulikanacho kama shirki iliyojificha, hapa msiba unakuwa mkubwa zaidi, kwani mara chache unaweza kuona kitendo kifanywacho kwa ikhlasi na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu pekee hata mwenye kufanya kitendo hicho anaweza kudhania kuwa kweli kakifanya kwa ikhlasi. Kwa mfano, ni kwanini mtu aandike jina lake kwenye bango kubwa pindi anapojenga msikiti ikiwa kweli kafanya hivyo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu? Ikiwa mtu na ikhlasi kweli ni kwanini anasimanga na kuzungumza kwa kile alichokitoa?

Sifa ya pili miongoni mwa sifa za kijahilia ni kwamba sheria zinanadhimu mambo yao na kutatua magomvi yao siko mbali na sheria za Mwenyezi Mungu: "Je wanataka hukumu za kijahili?"[١] Kwa mujibu wa Qur'ani ni kuwa kila hukumu isiyokuwa ile aliyo iteremsha Mwenyeze Mungu basi hiyo ni hukumu ya kijahilia. Lakini kwa bahati leo tunaziona jamii nyingi ziishizo kwa mfumo wa makabila huhukumiwa na mila na desturi ambazo Mwenyezi Mungu hakuziletea uthibitisho, bali zimewekwa na watu wasijua na walioko mbali kabisa na Mwenyezi Mungu. Hilo ni kama mfano tu, lakini nawe pia unaweza kutazama makundi mengine ya kijamii ukapata mifano ya namna zinavyoishi kwa kufuata sheria isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu. Bila shaka mwenyewe unajione ni namna gani mataifa ya ulimwengu yanavyo ongozwa na kanuni na sheria zilitungwa na mwanadamu mwenye mapungu, asiye miliki kheri ya nafsi yake wala shari, na asiywezea kuona zaidi ya ncha ya pua lake. Utamuona kila siku akibadili kifungu cha sheria kwa kuongeza kupengele au kukifuta, na hugundua mapungufu mengineo kila mara na hivyo hurekebisha kasoro zake. Tukirejea kwenye hadithi tunakuta zao zikieleza kuwa kila upingaji wa sheria ya Mwenyezi Mungu au

[١] Surat Al-Maidah: 50.

kutotenda kwa mujibu wake kuwa ni ujahilia na ujinga. Imekuja katika hadithi kuwa: "Yeyote atakaye kufa bila kutoa wasia, basi atakuwa amekufa kifo cha kijahilia"[١٤٥].

Kwa mfano, Firauni anasema: "Sikupeni ushauri ila ile niliyoiona"[١٥٠], hali hii sio maalumu kwa ajili ya Firauni bali hali inayojirudia daima na kwa watu wengi ambao hujipa mamlaka ya kutunga sheria badala ya Mwenyezi Mungu.

Sifa nyingine ya ujahilia ni upotovu wa imani, kama ilivyo ashiriwa katika kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo: "wanamdhania Mwenyezi Mungu dhana isiyokuwa ya haki, dhana ya kijahilia (kijinga/kikafiri)"[١٥١], kwa mfano, walikuwa wakiamini kwamba vyovyote mwanadamu atakavyo tenda madhambi anaweza kuokaka na adhabu iwapo tu atatoa kafara kwa miungu! Hali hii pia unaweza kuishuhudia katika jamii yetu kutokana na makhatibu wa mimbari ya Imamu Hussein (a.s) alivyo wakaririsha watu kwamba tone moja la machozi atakalolidondosha muumini kwa ajili ya Imam Husseini (a.s) basi linamtosha kuingia peponi hata kama atakuwa katenda maovu na madhambi makubwa! Haya wameyasema kufatia hadithi isemayo:

(من بكى على الحسين ولو مقدار جناح بعوضة وجبت له الجنة)

"Yeyote atakaye mlilia Imamu Hussein walau (chozi lake likawa) kwa kiwango cha bawa la mbu, basi Pepo itakuwa wajubu kwake"[١٥٢], lakini pia wakatumia ubeti huu wa mshairi kuwa ni hoja:

فإنَّ النار ليس تمس جسماً عليه غبار زوار الحسينِ

Na hakika moto hautaugusa mwili *** wenye vumbi la mazuwari wa Hussein (a.s).

Ni kweli kwamba hatukanush utukufu wa Imamu Hussein (a.s) kwa Mwenyezi Mungu. Bila shaka anastahiki kutukuzwa kwa namna hii, bali hata

---

[١٤٥] Ar-Rasaailul A'sharah cha sheikh Tusi, Uk: 317.

[١٥٠] Surat Ghaafir: 29.

[١٥١] Surat Al-Imran: 154.

[١٥٢] Kamil Az-Ziyarat: Uk: 201.

zaidi ya hivo. Lakini kutukuzwa huko inabidi kuwe ni sehemu ya sababu ambayo itakamilishwa na sehemu nyingine ambayo ni katika masharti ya kuingia peponi, ambapo sababu ya kwanza kabisa ni kumtii Mwenyezi Mungu katika maamrisho yake na makatazo yake. Qur'ani yenyewe inaeleza bayana kwamba: "Wala hawamuombei yeyote ila yule anayemridhia Mwenyezi Mungu"[١٠٥] , na hadithi kutoka kwa Imamu Swadiq (a.s) inasema: "Mwenye kupuuza sala hataupata uombezi wetu"[١٠٦] , hali kadhali madai hayo hayakinzana na aya ifuatayo:

[فَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْراً يَرَهُ، وَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرّاً يَرَهُ]

"Basi anayetenda chembe ya wema atauona, na atakayetenda chembe ya uovu atauona"[١٠٧] , isipokuwa ayadiriki matendo yake kwa kufanya toba yakweli.

Upotovu huu wa imani madhara yake ni makubwa mno, kwani huwaweka watu mbali na dini na hupunguza ufahamu wao baada kulewa na idikadi hizi zilizo mbali kabisa na Qur'ani na wakaacha kuifanyia kazi Qur'ani.

Katika alama za ujahilia pia ni kutojistiri, na kujishaua, na kuonyesha viongo vya uzuri, na kutojiheshimu na kuenea ausherati, anasema Mwenyezi Mungu: "Wala msijishauwe kwa mishauwo ya kijahilia ya kizamani"[١٠٨] . Na bila shaka jamii ya kileo imezipita nyumati zilizopita katika ufaiki na uovu, halikadhali katika mitindo ya ushawishi, na kupotosha, na kuwaingiza watu kwenye uchafu, na kurahisisha nyenzo za kisasa ili kueneza uchafu huo, kama ulivyokuwa ujahilia wa zamani nao pia ulikuwa ukivumbua njia na kuweka kanuni mbalimbali zinazokidhi hisia zao za kinjisia kwa mitindo mbalimbali ya kishetani. Kwa mfano: Makuraishi walipasisha kanuni ya kuharamisha kufanya tawafu kwenye nyumba ya Mwenyezi Mungu Makka mtu akiwa amevaa nguo yake ya zamani, kwa hoja kuwa inawezekana mwenye nayo akawa aliwahi kumuasi Mwenyezi Mungu akiwa ameivaa na kafanya madhambi, hivyo ikawa ni lazima afanye tawafu ndani ya nguo ya watu Makka, au nguo mpya au atufu akiwa uchi.

---

١٠٥. Surat Al-Anbiyaa: 28.

١٠٦. Biharul Anwar: 76/136.

١٠٧. Surat Az-Zalzalah: 7-8.

١٠٨. Surat Al-Ahzab: 33.

Na wafuasi wa shetani leo hii zaidi ya kumbi za ouvu, wameanzisha njia mbali mbali za kueneza uchafu kwa jina michezo. Michezo ambayo yafanyikayo ndani yake si madogo kuliko ya yale yatendekayo kwenye kumbi za ouvu. Bali makumbi zina nafuu kuliko michezo hiyo, kwa sababu zipo ufichoni na watu wengi hawayapendi kwani huogopa kupoteza hishima zao. Lakini katika michezo maovu hufanyika hadharani na mbaya zaidi ni kuwa mwenyekufanya uovu huo hujifaharisha kwao na wote humpongeza! Bila shaka utakuwa umeona ni namna gani watu walivyofanywa midoli mikononi mwa shetani, naye huwatumia atakavyo. Hali ipo hivyo hivyo katika anuwani na majina mwengine, ukiangalia kwa mfano: matamasha kumsaka mrembo, au mauonyesho ya navazi, au sanaa nyinginezo, vyote ni ouvu, lakini kwa kutumia majina na anuwani zinazokubalika kwenye jamii kiasi kwamba haponi mtu isipokuwa yule aliyehifadhiwa na Mwenyezi Mungu. Na malengo ya hayo yote ili wanadamu waishi kinyama na katika vurugu za kijinsia huku moto wa matamanio ukiendelea kuwaka kiasi kwamba hauishi wala hausazi.

Na miongoni mwa sifa za kijahilia ni upotovu wa fikra na mitazamo ya maisha. Kwa mfano: baadhi wa watu enzi za ujahilia wa kale, walikuwa wanakataa kuwaoza mabinti zao kwa watu wasiokuwa katika ukoo au kabila lao, kwakuwa walikuwa wakijiona kuwa wao ni wabora kuliko wengine na walijulikana kwa la 'Humus' ambao ni Makuraishi. Leo pia katika ujahilia wa kileo hali hiyo ipo. Kuna kundi la watu wengi, na mfano ulio wazi zaidi ni baadhi ya masayyidi (mashifu) ambao nasaba yao inanasibishwa kwa bwana mtume (s.a.w.w), wao hawawaozeshi mabinti zao isipokuwa kwa ambaye ni sayyidi kama wao, mpaka babinti hao wakuwa wakikaa mda mrefu manyumbani mwao na mwisho hukoza ndoa na kwa njia hiyo wanapoteza haki yao ya kisheria ya kufurahia familia na wao wakapata furaha ya umama. Haya yote sababu yake ni mitazo mibovo ya kijahilia. Ni mitazo duni zana unapo iangalia misingi ya Qur'ani, kwa Mwenyezi Mungu anasema:

[خَلَقَكُم مِّن نَّفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالاً كَثِيراً وَنِسَاء]

"Amekuumbeni kutokana na nafsi moja, na akauumba kutokana na nafsi hiyo wapili wake (mkewe). Na akaeneza kutokana na wawili hao wanaume na

wanawake wengi"[١٥٧] , vilevile ukiangalia mafunzo ya bwaña Mtume (a.s.w.w) aliposema:

(إذا جاءكم من ترضون خلقه ودينه فزوجوه)

"Atakapo kufikieni mtu ambaye mnairidhia dini tabia yake na dini yake, basi muozesheni"[١٥٨] . Hivyo ikiwa utukufu wao ni kwa sabaٌbu ya nasaba yao kwa bwana mtume (s.a.w.w), bila shaka utukufu wa bwana mtume ni kwa sababu ya Uislamu na kuiifu wake kwa Mwenyezi Mungu, na si kwa kuwa yeye ni Muhammad mwana wa Abdallah, anasema Mwenyezi Mungu:

[لَئِنْ أَشْرَكْتَ لَيَحْبَطَنَّ عَمَلُكَ وَلَتَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ]

"Bila shaka ukimshirikisha Mwenyezi Mungu vitendo vyako zitaharibika na lazima utakuwa miongoni mwa wenye khasara"[١٥٩] , na: ٥

[وَلَوْ تَقَوَّلَ عَلَيْنَا بَعْضَ الأَقَاوِيلِ، لأَخَذْنَا مِنْهُ بِالْيَمِينِ، ثُمَّ لَقَطَعْنَا مِنْهُ الْوَتِينَ، فَمَا مِنكُم مِّنْ أَحَدٍ عَنْهُ حَاجِزِينَ]

"Na lau kama angelituzulia baadhi ya maneno tu, bila ya shaka tungelimshika kwa mkono wa kulia, kisha kwa hakika tungelimkata mshipa mkubwa wa moyo. Na hapana yeyote katika nyinyi ambaye angeliweza kutuzuia naye"[١٦٠] , na bwana mtume (a.s) anasema: "Lau ningeliasi bila shaka ningeliporomoka"[١٦١] . Basi wana hadhi gani hao ambao hufanya biashara kwa jina lake (s.a.w.w) ilihali wanakhalifu sheria yake?

Vilevile katika alama za ujahilia wa kileo ni kuhitalifiana maadili na mizani ambavyo kipitia hiyo wanadamu hutofautiana kati ya ile kimungu na ile shetani. Qur'ani inaeleza wazi kwamba:

[إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِندَ اللَّهِ أَتْقَاكُمْ]

"Hakika mbora wenu kwa Mwenyezi Mungu ni yule amchaye zaidi"[١٦٢] , na:

---

[١٥٧] Surat An-Nisaa: 1.

[١٥٨] Wasailush- Shia: kitabun-Nikaah: abwabu muqaddimaatin-Nikaah wa aadaabihi, mlango: 28, hadithi: 1.

[١٥٩] Surat Az-Zumar: 65.

[١٦٠] Surat Al-Haaqah: 44-47.

[١٦١] Biharul Anwar: 22/467.

[١٦٢] Surat Al-Hujuraat: 13.

[قُلْ بِفَضْلِ اللهِ وَبِرَحْمَتِهِ فَبِذَلِكَ فَلْيَفْرَحُواْ هُوَ خَيْرٌ مِّمَّا يَجْمَعُونَ]

“Sema: Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na kwa rehema zake, basi wafurahi, hiyo ni bora kuliko wanavyo vikusanya[١] ”, wakati uhajilia ni kujifakharisha kwa mali, na vyeo na wingi wa watoto:

[أَلْهَاكُمُ التَّكَاثُرُ، حَتَّى زُرْتُمُ الْمَقَابِرَ]

“Kumewashughulisheni mno kutaka wingi wa mali, mpaka mmeingia makaburini”[١] , na:

[وَقَالُوا نَحْنُ أكثر أَمْوَالاً وَأَوْلاداً وَمَا نَحْنُ بِمُعَذَّبِينَ]

“Na wakasema: Sisi tuna mali nyingi na watoto wengi na wala sisi hatukuwa wenyekuadhibiwa”[١] , na mambo haya wako wazi kiasi kwamba sina haja ya kutaja mifano, na aya hizi zifuatazo zinauweka wazi ulingano huu baina ya maadili ya kimungu nay ale ya kijahilia:

[زُيِّنَ لِلنَّاسِ حُبُّ الشَّهَوَاتِ مِنَ النِّسَاء وَالْبَنِينَ وَالْقَنَاطِيرِ الْمُقَنطَرَةِ مِنَ الذَّهَبِ وَالْفِضَّةِ وَالْخَيْلِ الْمُسَوَّمَةِ وَالأَنْعَامِ وَالْحَرْثِ ذَلِكَ مَتَاعُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَاللهُ عِندَهُ حُسْنُ الْمَآبِ، قُلْ أَؤُنَبِّئُكُم بِخَيْرٍ مِّن ذَلِكُمْ لِلَّذِينَ اتَّقَوْا عِندَ رَبِّهِمْ جَنَّاتٌ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا وَأَزْوَاجٌ مُّطَهَّرَةٌ وَرِضْوَانٌ مِّنَ اللهِ وَاللهُ بَصِيرٌ بِالْعِبَادِ]

“Watu wamepambiwa kupenda matamanio ya wanawake, na vijana wa kiume, na mirundi ya dhahabu na fedha, na farasi wazuri wazuri, na wanyama, na mashamba. Hayo ni starehe ya maisha ya duniani; na kwa Mwenyezi Mungu ndio kwenye marejeo mema. Sema: Je, nikwambieni yaliyo bora kuliko hayo? Kwa wacha Mungu ziko Bustani kwa Mola wao zipitazo mito chini yake. Watakaa humo milele na wake waliotakaswa, na wanazo radhi za Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaona waja wake”[١] , pia anasema:

[وَمَا أَمْوَالُكُمْ وَلا أَوْلادُكُم بِالَّتِي تُقَرِّبُكُمْ عِندَنَا زُلْفَى إِلا مَنْ آمَنَ وَعَمِلَ صَالِحاً فَأُوْلَئِكَ لَهُمْ جَزَاء الضِّعْفِ بِمَا عَمِلُوا وَهُمْ فِي الْغُرُفَاتِ آمِنُونَ]

---

[١٦٣] Surat Yunus: 58.

[١٦٤] Surat At-Takathur: 1-2.

[١٦٥] Surat As-Sabai: 35.

[١٦٦] Surat Al-Imran: 14-15.

“Na si mali zenu wala watoto wenu watakao kukaribisheni kwetu katika daraja, isipokuwa aliyeamini na kutenda mema. Basi hao watapata malipo mardufu kwa walioyafanya. Nao watakuwa salama katika maghorofa”[١٦٧] .

Na sifa zizazoshirikisha ujahilia wa kale na wa kileo ni kuenea maadili mabaya. Mifano iliyowazi ni kama vile: kunywa pombe, na kupunja katika mizani, na kudanganya na ushoga. Mwenyezi Mungu anasema:

[وَتَأْتُونَ فِي نَادِيكُمُ الْمُنكَرَ]

“Na manafanya maovu katika mikusanyiko yenu?[١٦٨] , ٦

[وَلاَ تَبْخَسُواْ النَّاسَ أَشْيَاءهُمْ]

“Wala msiwapunje watu vitu vyao”[١٦٩] , ٦

[وَيْلٌ لِّلْمُطَفِّفِينَ، الَّذِينَ إذا اكْتَالُواْ عَلَى النَّاسِ يَسْتَوْفُونَ، وَإِذَا كَالُوهُمْ أَو وَّزَنُوهُمْ يُخْسِرُونَ]

“Ole wao wapunjao! Ambao wanapojipimia kwa watu hupokea kamili. Na wanapowapimia watu kwa kipimo au kwa mizani wao hupunguza”[١٧٠] , wamefikia hadi wanamdhihaki watu wema:

[وَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِ إِلاَّ أَن قَالُواْ أَخْرِجُوهُم مِّن قَرْيَتِكُمْ إِنَّهُمْ أُنَاسٌ يَتَطَهَّرُونَ]

“Na hayakuwa majibu ya kaumu yake isipokuwa kusema: Wafukuzeni katika mji wenu, kwa sababu wao ni watu wanaojitakasa”[١٧١] , kiasi kwamba Ja’far mwana wa ٧ Abu Talib historia imesajili jina lake kuwa ni miongoni mwa watu waliojiharamishia kunywa pombe na kufanya uzinzi enzi za ujahilia. Na miongoni mwa maadili mabaya waliyokuwa nayo kipindi cha ujahilia wa kale ni mwenye nguvu kumnyonya dhaifu, na kutokuwa na tabia hata za kiubinadamu achilia mbali zile za kimungu, kwani jambo muhimu kwao yalikuwa ni manufaa binafsi. Na leo maendeleo ya yamekuwa ni kumaliza mataifa na kuteketeza mimea na viumbe kwa ajili ya masilahi ambayo kwao ndio kila kitu. Ama lengo halisi na la kweli, ambalo

---

١٦٧ Surat As-Sabaa: 37.

١٦٨ Surat Al-Ankabut: 29.

١٦٩ Surat Al-A’raaf: 85.

١٧٠ Surat Al-Mutafifiin: 1-3.

١٧١ Surat Al-A’raaf: 82.

ni radhi za Mwenyezi Mungu na kufaulu huko Akhera, limekuwa likionekana kuwa ni kurudi nyuma na kukosa maendeleo! Anasema Mwenyezi Mungu:

[وَطَآئِفَةٌ قَدْ أَهَمَّتْهُمْ أَنفُسُهُمْ يَظُنُّونَ بِاللهِ غَيْرَ الْحَقِّ ظَنَّ الْجَاهِلِيَّةِ يَقُولُونَ هَل لَّنَا مِنَ الأَمْرِ مِن شَيْءٍ قُلْ إِنَّ الأَمْرَ كُلَّهُ لِلَّهِ يُخْفُونَ فِي أَنفُسِهِم مَّا لاَ يُبْدُونَ لَكَ يَقُولُونَ لَوْ كَانَ لَنَا مِنَ الأَمْرِ شَيْءٌ]

“Na kundi jingine limeshughulishwa na nafsi zao, hata wakamdhania Mwenyezi Mungu dhana isiyokuwa ya haki, dhana ya kijinga (kijahili na kikafiri). Wakisema: Hivyo tuna lolote sisi katika jambo hili? Wambie: Mambo yote ni ya Mwenyezi Mungu. Wanaficha katika nafsi zao wasiyo kudhihirishia. Wanasema: Tungekuwa na lolote katika jambo hili tusingeuliwa hapa”[١] , haya ndio malengo yao ambayo wanaishi kwa ajili yake kuwa: Tuna lolote katika jambo hili? ٧

Na katika sifa muhimu za kijahilia ambayo ndio sababu ya kubatikana kwake, ni kuacha kuamrisha mema na kukataza maovu. Na hili ni alilolohatahadharisha bwana mtume (s.a.w.w) aliposema:

(كيف بكم إذا فسدت نساؤكم وفسق شبابكم ولم تأمروا بالمعروف ولم تنهوا عن المنكر؟ فقيل له: ويكون ذلك يا رسول الله؟ فقال: نعم، وشر من ذلك، كيف بكم إذا أمرتم بالمنكر ونهيتم عن المعروف؟ فقيل له يا رسول الله ويكون ذلك؟ فقال (صلى الله عليه وآله): وشر من ذلك، كيف بكم إذا رأيتم المعروف منكراً والمنكر معروفاً)

“Mtakuwaje nyinyi pindi wanawake zenu watakapo haribika, na vijana wenu wakawa na tabia mbaya, na mema yasiamrishwe na maovu kukatazwa? Wakamuuliza: Je hilo litakuja kutokea? Akasema: Ndio, na mbaya kuliko hayo, mtakuwaje pindi mtakapo amrisha maovu na mkataza mema? Je hilo litakuja kutokea? Wakamuuliza. Akasema: Ndio, na mbaya kuliko hilo, mtakuwaje pindi mtakapo liona jambo jema kuwa uovu na ouvu kuwa ni wema”[١] . Na huku ndiko jamii za kileo zilikofikia. Na kwa mujibu wa Qur’ani ni kwamba tatizo linaanzia kwa wasomi wa dini au wanazuoni kwa sababu ya kupuuzia na kuchelewa kutekeleza wadhifa wao, na mfano mzuri wa wanazuoni ni nyinyi enyi wanafunzi na wakubwa vyuo vya kidini. Mwenyezi Mungu anasema:

[وَتَرَى كَثِيراً مِّنْهُمْ يُسَارِعُونَ فِي الإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ وَأَكْلِهِمُ السُّحْتَ لَبِئْسَ مَا كَانُواْ يَعْمَلُونَ، لَوْلاَ يَنْهَاهُمُ الرَّبَّانِيُّونَ وَالأَحْبَارُ عَن قَوْلِهِمُ الإِثْمَ وَأَكْلِهِمُ السُّحْتَ لَبِئْسَ مَا كَانُواْ يَصْنَعُونَ]

---

[١] Surat Al-Imran: 154.

[١] Al-Kafii: 5/59, mlango wa: kuamrisha mwema na kukataza maovu.

“Na utawaona wengi katika wao wanakimbilia kwenye dhambi, na uadui, na ulaji wao vya haramu. Bila shaka wayafanyayo hayo ni maovu mno. Mbona hao wanazuoni na makohani wao hawawakatazi maneno yao ya dhambi, na ulaji wao vya haramu? Bila shaka wayafanyayo ni maovu mno”[۱۷۵] ,

[كَانُواْ لاَ يَتَنَاهَوْنَ عَن مُّنكَرٍ فَعَلُوهُ لَبِئْسَ مَا كَانُواْ يَفْعَلُونَ، تَرَى كَثِيراً مِّنْهُمْ يَتَوَلَّوْنَ الَّذِينَ كَفَرُواْ لَبِئْسَ مَا قَدَّمَتْ لَهُمْ أَنفُسُهُمْ أَن سَخِطَ اللّهُ عَلَيْهِمْ وَفِي الْعَذَابِ هُمْ خَالِدُونَ]

“Hawakuwa wenye kukataza maovu waliyokuwa wakiyafanya, bila shaka ni maovu mambo waliyokuwa wakiyafanya. Utawaona wengi wao wanafanya urafiki na makafiri. Hakika ni maovu yaliyotangulizwa na nafsi zao hata Mwenyezi Mungu amewakasirikia, nao watadumu katika adhabu”[۱۷۶] .

Na hii ni sifa nyingine ya jamii iliyojiweka mbali na Uislamu, yaani kuwafanya makafiri marafiki. Kuhusiana na ubaya huu anasema Amirulmuunina Ali Bin Abi Talib (a.s):

(أما بعد فإنه إنما هلك من كان قبلكم حيثما عملوا من المعاصي ولم ينههم الربانيون والأحبار عن ذلك، وأنهم لما تمادوا في المعاصي نزلت بهم العقوبات فأمروا بالمعروف ونهوا عن المنكر واعملوا أن الأمر بالمعروف والنهي عن المنكر لن يقربا أجلاً ولن يقطعا رزقاً)

“Ama baada ya hayo, hakika waliokuwa kabla yenu waliangamia pindi walipotenda maasi na wanazuoni na makohani wao hawakuwakataza hayo, nao walipokithirisha maasi, basi adhabu ziliwateremkia. Basi amrisheni mema na katazeni maovu, na mtambue kuwa kuamrisha mema na kukataza maovu hakuharakishi kifo wala hakupunguzi riziki”[۱۷۷] .

Ukweli ni kwamba pasina kuisimamia faradhi hii hakutabia hadhi yoyote ile kwa waumini, si kwa Mwenyezi Mungu na mtume wake (s.a.w.w) tu, bali hata kwa maadui wao, kwani baina ya Makuraishi walikuwepo waumini wanaompwekesha Mwenyezi Mungu waliojulikana maah’nafi, yaani wale

---

۱۷۵. Surat Al-Maidah: 62-63.

۱۷۶. Surat Al-Maidah: 79-80.

۱۷۷. Nahjul-Balaghah: khutba: 27.

walioacha kuyaabudia masanamu na wakajishughulisha na kumuabudu Mwenyezi Mungualiyetukuka, lakini hata hivyo hawakuwa na thamani mbele ya Mushirikiana, wala hawakujali uwepo wao; kwa sababu wao waliacha faradhi hii adhimu.

Ndio maana kutekeleza wadhifa na faradhi hii ni moja ya sifa za jamii ya Kiislamu:

[كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللهِ]

"Nyinyi mmekuwa bora ya umma walio tolewa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu. Na lau kuwa Watu wa Kitabu nao wameamini ingeli kuwa bora kwao. Wapo miongoni mwao waumini, lakini wengi wao wapotovu"[١٧٧] , na:

[وَلَيَنصُرَنَّ اللَّهُ مَن يَنصُرُهُ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ، الَّذِينَ إِن مَّكَّنَّاهُمْ فِي الأَرْضِ أَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ وَأَمَرُوا بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَوْا عَنِ الْمُنكَرِ وَلِلَّهِ عَاقِبَةُ الأُمُورِ]

"Na bila ya shaka Mwenyezi Mungu humsaidia yule anaye msaidia Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mtukufu. Wale ambao tukiwapa madaraka katika nchi husimamisha Sala, na wakatoa Zaka, na wakaamrisha mema, na wakakataza mabaya. Na kwa Mwenyezi Mungu ndio marejeo ya mambo yote"[١٧٨] ,

[وَلْتَكُن مِّنكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنكَرِ]

"Na uwe kutokana na nyinyi umma unao lingania kheri na unao amrisha mema na unakataza maovu."[١٧٩] ,

[وَالْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاء بَعْضٍ يَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنكَرِ وَيُقِيمُونَ الصَّلاَةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَيُطِيعُونَ اللهَ وَرَسُولَهُ أُوْلَئِكَ سَيَرْحَمُهُمُ اللهُ إِنَّ اللهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ]

"Na Waumini wanaume na Waumini wanawake wao kwa wao ni marafiki walinzi. Huamrisha mema na hukataza maovu, na hushika Sala, na hutoa Zaka, na humtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao Mwenyezi Mungu atawarehemu.

---

[١٧٧] Surat Al-Imran: 110.

[١٧٨] Surat Al-Hajj: 40-41.

[١٧٩] Surat Al-Imran: 104.

Hakika Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye nguvu, Mwenye hikima"[١] , na aya nyingizo nyingi, hapa hatuwezi kuziorodhesha zote, kwani bahathi hii malengo yake ni kutoa ishara tu na kufungua mlango wa fikra katika masuala haya, kwa sababu kila mlango ukiufungua hufunguka milango elfu moja kwa ujuzi wa Mwenyezi Mungu na wingi wa rehema zake.

Kutawaliwa na hadithi za kubuni na mabo yasiyo na uhakika ni moja ya alama za ujahilia. Kwa mfano, Warabu walikuwa wakiichulia sauti ya kunguru na bundi kuwa ni nuksi, na sasa leo hii Wamagharibi na bila sababu yoyote ile nao wanaichukuli namba (13) kuwa ni nuksi. Wakati huo watabiri na makohani walienea kila mahala na wakawa na soko nzuri. Leo hii pia tunaona mwitikio mkubwa wa watu kwenda kwa wapiga ramli na wanajimu na mfano wa hivyo vinavyo fanywa na watu wasiojua na wakawaida.

Sifa nyingine ya kijahilia ni kuwazuwia watu na Qur'ani na kuwatenga nayo mbali kwa njia mbalimbali. Hakika Nadhri ibin Al-Harith ambaye ni miongoni mwa watu waliokwenda katika miji ya Farsi na akajifunza habari za wafalme wao, na akawa akimfuata bwana mtume (s.a.w.w) kwa nyuma, mtume anapo nyanyuka kutoka kwenye kikao, basi Nadhri naye anakaa baina yao kisha anawasimulia visa vya wafalme wa Farsi, kisha anawauliza: Ni kati yetu mwenyekusimilia vizuri kuliko mwenzake, Mimi au Muhammad? Hivyo wakawa wanaisifia Qur'ani kuwa ni viza vya kale alivyo viandikisha, anavyosomewa asubuhi na jioni, au wakisema kuwa: hadithi za kuzua, au wakati mwingine walikuwa wakipiga makofi kwa sauti ya juu pindi mtume anaposoma ili kuzuwia isisikilizike. Qur'ani inasimulia matendo yao kwa kusema:

[وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لا تَسْمَعُوا لِهَذَا الْقُرْآنِ وَالْغَوْا فِيهِ لَعَلَّكُمْ تَغْلِبُونَ]

"Na walio kufuru walisema: Msiisikilize Qur'ani hii, na timueni zogo, huenda mkashinda"[٢] , inasema pia:

[١] Surat At-Tawbah: 71.

[٢] Surat Fussilat: 26.

[وَإِن يَرَوْا آيَةً يُعْرِضُوا وَيَقُولُوا سِحْرٌ مُّسْتَمِرٌّ]

"Na wakiona ishara hugeuka upande na husema: Hu uchawi tu unazidi uendelea"[١٧] . Na sasa ujahilia wa kisasa pia umekuwa ukiisifu Qur'ani kwa sifa zilezile za ujahilia wa kale, kwamba Qur'ani ni maneno ya Muhammad yatokanayo na fikra za kibinadamu wala sio ufunuo na wahai utokao kwa Mwenyezi Mungu. Wamejaribu kuandika vitabu kuhusu aya walizodhania kuwa zinakinzana, lakini waliposhindwa na Qur'ani ikaendelea kuthibitisha uwepo wake waliamua -kwa kila ukhabithi, vijanja na udanganyifu- kuifanya ipoteze maana yake kivitendo, na wakaiweka mbali na maisha halisia na wakaibadili ikiwa ni mfano wa kaswida na nyimbo ambazo huibwa na wasanii na wasikilizaji wake wakawa wakionyesha furaha zao sauti za juu wakisema: Allah! Allah! Ewe shaikh! Wameifanya Qur'ani kuwa ni kinga huivaa vifuani mwao au huitundika majumbani mwazo na si vinginevyo. Njia hii kama uonavyo ni hatari kuliko ile ya Nadhiri bin Al-Harith na mfano wake, kama ambavyo ni ujanja mbaya na matokeo yake ni hatari mno. [٢]

Katika matendo yaliyowazi ambayo husifika nayo majahili ni kung'ang'ania mila walizo zirithi kutoka walikuwa kabila yao, na kujilazimisha kuzifanyia kazi, na kutokuwa tayari kuachana nazo hata kama ziko kinyume na haki iliyothibiti kwa hoja na dalili. Bila shaka matendo haya ni tija itokanayo na ugumu wa moyo, kutokuwa na fikra salama na kuzitawaza hisia kwamba kitu kilichofanywa na vizazi vya mababa na mababu hujipatia utukufu ambao huwa vigumu kuuvunja. Kwa hakika Qur'ani tukufu imeikariri maana hii kwa wingi kiasi kwamba tunaweza kufahamu kuwa huu ni mtihani ambao manabii wote walikabiliana nao. Anasema Mwenyezi Mungu:

[وَإِذَا قِيلَ لَهُمُ اتَّبِعُوا مَا أَنزَلَ اللهُ قَالُواْ بَلْ نَتَّبِعُ مَا أَلْفَيْنَا عَلَيْهِ آبَاءنَا أَوَلَوْ كَانَ آبَاؤُهُمْ لاَ يَعْقِلُونَ شَيْئاً وَلاَ يَهْتَدُونَ]

"Na wanapo ambiwa: Fuateni aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu; wao husema: Bali tutafuata tuliyo wakuta nayo baba zetu. Je, hata ikiwa baba zao walikuwa hawaelewi kitu, wala hawakuongoka?"[١٨] , [٨]

[إِنَّهُمْ أَلْفَوْا آبَاءهُمْ ضَالِّينَ، فَهُمْ عَلَى آثَارِهِمْ يُهْرَعُونَ]

---

[١٧] Surat Al-Qamar: 2.

[١٨] Surat Al-Baqarah: 170.

“Hakika waliwakuta baba zao wamepotea, na wao wakafanya haraka kufuata nyayo zao”[١٧٤] ,

[قَالُواْ أَجِئْتَنَا لِنَعْبُدَ اللهَ وَحْدَهُ وَنَذَرَ مَا كَانَ يَعْبُدُ آبَاؤُنَا فَأْتِنَا بِمَا تَعِدُنَا إِن كُنتَ مِنَ الصَّادِقِينَ]

“Wakasema: Je! Umetujia ili tumuabudu Mwenyezi Mungu peke yake, na tuyaache waliyo kuwa wakiyaabudu baba zetu? Basi tuletee hayo unayo tuahidi, ukiwa miongoni mwa wasemao kweli”[١٧٥] ,

[بَلْ قَالُوا إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءنَا عَلَى أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَى آثَارِهِم مُّهْتَدُونَ، وَكَذَلِكَ مَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ فِي قَرْيَةٍ مِّن نَّذِيرٍ إِلا قَالَ مُتْرَفُوهَا إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءنَا عَلَى أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَى آثَارِهِم مُّقْتَدُونَ، قَالَ أَوَلَوْ جِئْتُكُم بِأَهْدَى مِمَّا وَجَدتُّمْ عَلَيْهِ آبَاءكُمْ قَالُوا إِنَّا بِمَا أُرْسِلْتُم بِهِ كَافِرُونَ]

“Bali wanasema: Hakika sisi tuliwakuta baba zetu wanashika dini makhsusi, basi na sisi tunaongoza nyayo zao. Na kadhaalika hatukumtuma mwonyaji kwenye mji wowote isipokuwa watu wake waliodeka kwa starehe walisema: Hakika sisi tuliwakuta baba zetu wanashika dini makhsusi, na sisi tunafuata nyayo zao. Akasema (Mwonyaji): Hata nikikuleteeni yenye uwongofu bora kuliko mlio wakuta nao baba zenu? Wakasema: Sisi tunayakataa tu hayo mliyo tumwa”[١٧٦] . Na aya mbili za mwisho zinaonyesha kwamba mtihani huu mkubwa kumkabili na kumkuta kila anayetaka kuiokoa jamii yake na akafanya juhudi za kuiimarisha, kwa sababu Mwenyezi Mungu amesema: “Na kadhaalika hatukumtuma mwonyaji kabla yako isipokuwa…”, na hali hii sio maalumu kwa mitume peke yao.

Ujahilia wa kisasa hautofautiani na ule wa kale katika hili, kwani ushahidi wa hilo ni mwingi sana. Na kwa hika jamii zetu bado zinakabiliwa na ugonjwa wa kufuata ya kale kama asemavyo mwanafikra mmoja wa kihauza.

Kutomjua Imam na kiongozi wa kweli nayo ni alama ya ujagilia na ujinga:

(من مات ولم يعرف إمام زمانه مات ميتة جاهلية)

“Yeyoye yule atakayekufa bila kumtambua na kumjua Imam wa zama zake, basi mtu huyo atakufa mauti ya kijahili (yaani atakufa kifo cha ukafiri)”[١٧٧] .

---

[١٧٤] Surat As-Saffat: 69-70.

[١٧٥] Surat Al-A’raaf:70.

[١٧٦] Surat Az-Zukhruf: 22-24.

[١٧٧] Kamalud Diini wa Tamamun Ni’mah:409.

Na malengo ya kumtambua sio kulijua jina lake pekee, bali ni kuyajua kikamilifu majukumu yetu kwa Imam na kuyatekeleza ipasavyo. Na bila shaka upumgufu huu kwa Imam wetu wa zama (a.s) uko wazi. Lakini pia dua iliyopokelewa inaiuelezea ujahilia huu kwa kusema:

(اللهم عرفني نفسك فإنك إن لم تعرفني نفسك لم أعرف نبيك اللهم عرفني رسولك فإنك إن لم تعرفني رسولك لم أعرف حجتك اللهم عرّفني حجّتك فإنك إن لم تعرفني حجتك ضللت عن ديني)

"Ewe Mwenyezi Mungu! Nifanye nikujue wewe, kwani iwapo hautanifanya nikakujua wewe bila shaka sitaweza kumjua mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu! Nifanye nimjue mtume wako, kwani iwapo hautanifanya nikamjua mtume wako, bila shaka sitaweza kumjua hoja wako. Ewe Mwenyezi Mungu! Nifanye nimjue hoja wako, kwani iwapo hautanifanya kumjua hoja wake bila shaka nitapotea katika dini yako"[١٨] , kwa sababu upotevu katika dini ndio ujahilia na ujinga wenyewe. ٨

Na jambo hili linahitaji kudurusiwa kwa kina na kubainisha kwanini ni lazima kuwepo Imam na Hoja wa Mwenyezi Mungu kwa kila zama, lakini pia ni nini takilifu yetu katika kipindi hiki cha ghaiba na kufichikana Imam, na upi wadhifa wetu kwa Imam wakati huu, na majibu ya viulizo vingi vya maswali na mishkeli ya kifikra inayolizunguka jambo hili la Imam, mambo amabyo yamefichikana kwa waumini wengi ukiachilia mbali waiokuwa waumini, hali ya kuwa: "maimam ndio mlango wa Mwenyezi Mungu ambao hawezi kufikiwa isipokuwa kupitia mlango huo"[١٩] . Ni vipi atakwenda kwa Mwenyezi Mungu yule asiyeujua mlango wa kwenda kwake? Na kipi baada ya Mwenyezi Mungu isipokuwa upotovu uliyowazi. ٩

Sifa nyingine ya ujahilia ni kuyakubali mambo ya kimada pekee na kuyakanusha mambo ya ghaibu na yale yasiyo ya kimada. Anasema Mwenyezi Mungu:

[وَقَالُواْ إِنْ هِيَ إِلاَّ حَيَاتُنَا الدُّنْيَا وَمَا نَحْنُ بِمَبْعُوثِينَ]

"Sema: Mola Mlezi wangu ameamrisha uadilifu, na mumuelekeze nyuso zenu kila mnapo sujudu, na muombeni Yeye kwa kumsafia Dini. Kama alivyo kuumbeni mwanzo ndivyo mtavyo rudi"[١٩] , ٩

---

١٨. Al-Kafii: 1/337.

١٨. Al-Kafii: 1/196.

١٩. Surat Al-An'aam: 29.

[وَقَالُوا مَا هِيَ إِلا حَيَاتُنَا الدُّنْيَا نَمُوتُ وَنَحْيَا وَمَا يُهْلِكُنَا إِلا الدَّهْرُ وَمَا لَهُم بِذَلِكَ مِنْ عِلْمٍ إِنْ هُمْ إِلا يَظُنُّونَ]

“Na walisema: Hapana ila huu uhai wetu wa duniani – twafa na twaishi, na hapana kinacho tuhiliki isipo kuwa dahari. Lakini wao hawana ilimu ya hayo, ila wao wanadhani tu” [١٩٤]. Na hapa Qur’ani huja kuwaazisha malengo watukufu watakayoishi kwa ajili yake:

[وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالإِنسَ إِلا لِيَعْبُدُونِ]

“Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi” [١٩٥],

[قَالَ يَا قَوْمِ اعْبُدُواْ اللّهَ مَا لَكُم مِّنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ هُوَ أَنشَأَكُم مِّنَ الأَرْضِ وَاسْتَعْمَرَكُمْ فِيهَا فَاسْتَغْفِرُوهُ ثُمَّ تُوبُواْ إِلَيْهِ إِنَّ رَبِّي قَرِيبٌ مُّجِيبٌ]

“Na kina Thamud tuliwapelekea ndugu yao Saleh. Akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna Mungu ila Yeye. Yeye ndiye aliye kuumbeni katika ardhi, na akakuwekeni humo. Basi mwombeni msamaha, kisha mtubu kwake. Hakika Mola wangu Mlezi yupo karibu, anaitikia maombi” [١٩٦],

[ثُمَّ جَعَلْنَاكُمْ خَلاَئِفَ فِي الأَرْضِ مِن بَعْدِهِم لِنَنظُرَ كَيْفَ تَعْمَلُونَ]

“Kisha tukakufanyeni nyiye ndio wenye kushika mahala pao baada yao katika ardhi ili tuone jinsi mtakavyotenda” [١٩٧].

Hivyo, mwanadamu hakuumbwa kwenye huu dunia ili aje kujishughulisha na matamanio yake, bali amefanywa kuwa ni khalifa na kiongozi ardhini ili aijenge na kuifanya iwe shamba kwa ajili ya akhera yake, na Muumba wake humhesabia matendo yake ili aone ni vipi atafanya. Na Mwenyezi Mungu humkemea mwanadamu anayezama katika mambo ya kimada kwa kusema:

[أَيَحْسَبُ الإنسان أَن يُتْرَكَ سُدىً، أَلَمْ يَكُ نُطْفَةً مِّن مَّنِيٍّ يُمْنَى، ثُمَّ كَانَ عَلَقَةً فَخَلَقَ فَسَوَّى، فَجَعَلَ مِنْهُ الزَّوْجَيْنِ الذَّكَرَ وَالأُنثَى، أَلَيْسَ ذَلِكَ بِقَادِرٍ عَلَى أَن يُحْيِيَ الْمَوْتَى]

“Ati binaadamu anadhani kuwa ataachwa bure? Kwani yeye hakuwa ni tone ya manii lilioshushwa? Kisha akawa kidonge cha damu, tena Mwenyezi Mungu akamuumba na akamtengeneza vilivyo. Kisha akamfanya namna mbili,

---

[١٩٤] Surat Al-Jaathiyah: 24.

[١٩٥] Surat Ath-Thaariyaat: 56.

[١٩٦] Surat Hud: 61.

[١٩٧] Surat Yunus: 14.

mwanamume na mwanamke. Je, huyo hakuwa ni Muweza wa kufufua wafu?"[١٩٥] . Ndio, umetakasika ewe Mwenyezi Mungu. Wewe ni muweza hilo na ni muweza wa kila jambo. Ni kweli kuwa hii haimanishi kumzuwia mwanadamu kuwa na fungu lake hapa duniani maadamu hajalifanya kuwa ndio lengo lake la mwisho. Bali anaweza kuwa na fungu na akalitumia kwa ajili ya lengo lake halisi, ambalo ni radhi ya Mwenyezi Mungu aliyetukuka:

[وَابْتَغِ فِيمَا آتَاكَ اللَّهُ الدَّارَ الآخِرَةَ وَلا تَنسَ نَصِيبَكَ مِنَ الدُّنْيَا وَأَحْسِن كَمَا أَحْسَنَ اللَّهُ إِلَيْكَ وَلا تَبْغِ الْفَسَادَ فِي الأَرْضِ إِنَّ اللَّهَ لا يُحِبُّ الْمُفْسِدِينَ]

"Na utafute, kwa aliyokupa Mwenyezi Mungu makaazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyokufanyia wema wewe. Wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi mafisadi"[١٩٦] , hivyo upungufu na kasoro haviko kwenye kuipata dunia, kwani imesemwa kuwa: "Dunia ni shamba la Akhera"[١٩٧] na katika hadithi nyingine imekuja kwamba: "Dunia ni sehemu ya chumo kwa mawalii wa Mwenyezi Mungu"[١٩٨] . Wao hufanya biashara isiyobwaga na Mwenyezi Mungu.

Sifa nyingine ya kijahilia ni kugawanyika na kufarakana. Anasema Mwenyezi Mungu:

[وَلا تَكُونُوا مِنَ الْمُشْرِكِينَ، مِنَ الَّذِينَ فَرَّقُوا دِينَهُمْ وَكَانُوا شِيَعًا كُلُّ حِزْبٍ بِمَا لَدَيْهِمْ فَرِحُونَ]

"Muwe wenye kutubia kwake, na mcheni Yeye, na shikeni Sala, na wala msiwe katika washirikina. Katika wale ambao kwamba wameigawanya dini yao, na wakawa makundi makundi, kila kikundi kinafurahia kilicho nacho"[١٩٩] . Yote hayo ni kwa sababu ya kupoteza kwao mhimili wa msingi ambao walipaswa kuushikilia, mhimili ambao ni kumpekesha Mwenyezi Mungu aliyetukuka na Kaaba ikafanywa kuwa ni alama yake. Ama jamii iliyo mbali na Mwenyezi Mungu kwanza: hugawangika mataifa kwa miji, kiasi leo hii idadi ya mataifa duniani imefikia zaidi

---

[١٩٥] Surat Al-Qiyaamah: 36-40.

[١٩٦] Surat Al-qasas: 77.

[١٩٧] A'waalil Aalaali: 1/267.

[١٩٨] Minhaajul Baraa'h fii Sharhin Nahjul Balaghah: 15/203.

[١٩٩] Surat Ar-Rum: 31-32.

ya 180. Lakini pia hugawanyika kwa jinsia na matabaka mbalimbali ndani ya nchi moja, kisha hugawanyika kifikra, utamkuta huyu ana mlengo wa kikomunisti na mwengine mlengo wake ni wakibepari hali ya kuwa wote wana utaifa mmoja na dini moja. Wanatofautiana katika mawazo hata wakiwa dini moja, bali hata ndani ya madhehebu moja, na kila kundi utaliona likiwanyika makundi tofauti tofauti na kuendelea: "kila kikundi kinafurahia kilicho nacho" [٢] . Na Qur'ani imekwishaelezea kuwa mgawanyiko huu ni moja ya adhabu za kujiweka mbali na njia ya Mwenyezi Mungu na dini yake, Qur'ani inaasema:

[قُلْ هُوَ الْقَادِرُ عَلَى أَن يَبْعَثَ عَلَيْكُمْ عَذَابًا مِّن فَوْقِكُمْ أَوْ مِن تَحْتِ أَرْجُلِكُمْ أَوْ يَلْبِسَكُمْ شِيَعاً وَيُذِيقَ بَعْضَكُم بَأْسَ بَعْضٍ انظُرْ كَيْفَ نُصَرِّفُ الآيَاتِ لَعَلَّهُمْ يَفْقَهُونَ]

"Sema: Yeye ndiye Muweza wa kukuleteeni adhabu kutoka juu yenu au kutoka chini ya miguu yenu, au kukuleteeni fujo la mfarakano, na kuwaonjesha baadhi yenu jeuri ya wenzao. Tazama vipi tunavyo zieleza aya ili wapate kufahamu" [٢] , kisha Uislamu ukaja kuwakusanya na kuwaweka pamoja kwa Qur'ani hii, amesma Mwenyezi Mungu:

[وَاعْتَصِمُواْ بِحَبْلِ اللهِ جَمِيعًا وَلاَ تَفَرَّقُواْ وَاذْكُرُواْ نِعْمَةَ اللهِ عَلَيْكُمْ إِذْ كُنتُمْ أَعْدَاء فَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُم بِنِعْمَتِهِ إِخْوَانًا وَكُنتُمْ عَلَى شَفَا حُفْرَةٍ مِّنَ النَّارِ فَأَنقَذَكُم مِّنْهَا كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللهُ لَكُمْ آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ]

"Na shikamaneni kwa Kamba ya Mwenyezi Mungu nyote pamoja, wala msifarikiane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu: vile mlivyo kuwa nyinyi kwa nyinyi maadui naye akaziunganisha nyoyo zenu; kwa neema yake mkawa ndugu. Na mlikuwa ukingoni mwa shimo la Moto, naye akakuokoeni nalo. Namna hivi Mwenyezi Mungu anakubainishieni Ishara zake ili mpate kuongoka" [٢] , na katika aya nyingine anasema:

[وَإِن يُرِيدُواْ أَن يَخْدَعُوكَ فإن حَسْبَكَ اللهُ هُوَ الَّذِيَ أَيَّدَكَ بِنَصْرِهِ وَبِالْمُؤْمِنِينَ، وَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ لَوْ أَنفَقْتَ مَا فِي الأَرْضِ جَمِيعاً مَّا أَلَّفْتَ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ وَلَكِنَّ اللهَ أَلَّفَ بَيْنَهُمْ إِنَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ]

"Na akaziunga nyoyo zao. Na lau wewe ungeli toa vyote viliomo duniani usingeli weza kuziunga nyoyo zao, lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliye waunganisha.

---

[٢] Surat Al-Muuniin: 53.

[٢] Surat Al-An'aam: 65.

[٢] Surat Al-Imran: 103.

Hakika Yeye ndiye Mtukufu Mwenye nguvu na Mwenye hikima. Ewe Nabii! Mwenyezi Mungu anakutoshelezea wewe na waumini waliokufuata"[٢] .

Katika sifa zilizowazi za kijahilia pia ni kuogopa kifo na kukiogopa kila kinacho ashiria suala la umauti. Sababu ya hilo ni kwakuwa wapeipoteza Akhera na wakayafanya malengo yao kuwa kuzishibisha hisia zao na mahitaji yao:

[قُلْ إِن كَانَتْ لَكُمُ الدَّارُ الآخِرَةُ عِندَ اللهِ خَالِصَةً مِّن دُونِ النَّاسِ فَتَمَنَّوُاْ الْمَوْتَ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ، وَلَن يَتَمَنَّوْهُ أَبَداً بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ وَاللهُ عَلِيمٌ بِالظَّالِمِينَ، وَلَتَجِدَنَّهُمْ أَحْرَصَ النَّاسِ عَلَى حَيَاةٍ وَمِنَ الَّذِينَ أَشْرَكُواْ يَوَدُّ أَحَدُهُمْ لَوْ يُعَمَّرُ أَلْفَ سَنَةٍ وَمَا هُوَ بِمُزَحْزِحِهِ مِنَ الْعَذَابِ أَن يُعَمَّرَ وَاللهُ بَصِيرٌ بِمَا يَعْمَلُونَ]

"Sema: Ikiwa nyumba ya Akhera iliyoko kwa Mwenyezi Mungu ni yenu tu bila ya watu wengine, basi tamanini mauti kama nyinyi mnasema kweli. Wala hawatayatamani kamwe kwa sababu ya yale yaliyo tangulizwa na mikono yao; na Mwenyezi Mungu ni mwenye kuwajua vyema wanao dhulumu. Na hakika utawaona ni wenye kuwashinda watu wote kwa pupa ya kuishi, na kuliko washirikina. Kila mmoja wao anatamani lau angeli pewa umri wa miaka elfu. Wala hayo ya kuzidishiwa umri hayamuondoshei adhabu; na Mwenyezi Mungu anayaona wanayo yatenda"[٢] ,

[قُلْ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ هَادُوا إِن زَعَمْتُمْ أَنَّكُمْ أَوْلِيَاء لِلَّهِ مِن دُونِ النَّاسِ فَتَمَنَّوُا الْمَوْتَ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ، وَلا يَتَمَنَّوْنَهُ أَبَدًا بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالظَّالِمِينَ]

"Sema: Enyi mlio Mayahudi! Ikiwa nyinyi mnadai kuwa ni vipenzi vya Mwenyezi Mungu pasipo kuwa watu wengine, basi yatamanini mauti, ikiwa mnasema kweli. Wala hawatayatamani kabisa, kwa sababu ya iliyo kwisha yatanguliza mikono yao. Na Mwenyezi Mungu anawajua walio dhulumu"[٢]

[فَإِذَا جَاء الْخَوْفُ رَأَيْتَهُمْ يَنظُرُونَ إِلَيْكَ تَدُورُ أَعْيُنُهُمْ كَالَّذِي يُغْشَى عَلَيْهِ مِنَ الْمَوْتِ]

[٢٣] Surat Al-Anfaal: 62-63.

[٢٤] Surat Al-Baqarah: 94-96.

[٢٥] Surat Al-Jumu'a: 6-7.

“Ikifika khofu utawaona wanakutazama na macho yao yanazunguka, kama yule ambaye aliye zimia kwa kukaribia mauti”[٢٠] , lakini Qur’ani inazidi kuwahakikishia ukweli huu usio kuwa na makwepeo:

[قُلْ إِنَّ الْمَوْتَ الَّذِي تَفِرُّونَ مِنْهُ فإنه مُلاقِيكُمْ ثُمَّ تُرَدُّونَ إِلَى عَالِمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَيُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ]

“Sema: Hayo mauti mnayo yakimbia, bila ya shaka yatakukuteni. Kisha mtarudishwa kwa Mwenye kuyajua yaliyo fichikana na yanayo onekana. Hapo atakwambieni mliyo kuwa mkiyatenda”[٢١] ,

[قُل لَّن يَنفَعَكُمُ الْفِرَارُ إِن فَرَرْتُم مِّنَ الْمَوْتِ أَوِ الْقَتْلِ وَإِذًا لا تُمَتَّعُونَ إِلا قَلِيلاً]

“Sema: Kukimbia hakukufaeni kitu ikiwa mnakimbia mauti au kuuwawa, na hata hivyo hamtastareheshwa ila kidogo tu”[٢٢] ,

[أَيْنَمَا تَكُونُواْ يُدْرِككُّمُ الْمَوْتُ وَلَوْ كُنتُمْ فِي بُرُوجٍ مُّشَيَّدَةٍ]

“Popote mlipo mauti yatakufikieni, na hata mkiwa katika ngome zilizo na nguvu”[٢٣] ,

[قُل لَّوْ كُنتُمْ فِي بُيُوتِكُمْ لَبَرَزَ الَّذِينَ كُتِبَ عَلَيْهِمُ الْقَتْلُ إِلَى مَضَاجِعِهِمْ]

“Seme hata mngelikuwa majumbani mwenu, basi wangetoka walioandikiwa kufa, wakenda mahali pao pa kuangukia wafe”[٢٤] . Hivyo khofu ya kifo haitoweki isipokuwa kwa kujiandaa na imamni na matendo mema na kuijenga Akhera kwa yale anayo yaridhia Mwenyezi Mungu na kwa kujikaribisha kwake.

Ninadhani mpaka kufikia hapa nitakuwa nimetoa ishara yenye kutosha na ninatakuwa nimefungua mlango wa fikra kwa kiwango cha kutosha kuhusiana na upande, kwa sababu hatua ya kwanza katika kuyatibu maradhi yetu ya kijamii ni kuainisha ugonjwa na maradhi kwa umakini kisha kuutolea matibabu yanayo endana na ugonjwa huo.

---

[٢٠] Surat Al-Ahzab: 19.

[٢١] Surat Al-Jumu’a: 8.

[٢٢] Surat Al-Ahzab: 16.

[٢٣] Surat An-Nisaa: 78.

[٢٤] Surat Al-Imran: 154.

Na kwa maelezo hayo, mambo kadhaa yanayo ikamilisha anuwani ya Ujahilia kwa wanadamu wa leo hii yatakuwa yamebainika. Lakini pia tumeutambua upole endelevu wa Mwenyezi Mungu kwa waja wake, upole ambao hauchagui baina ya kaumu na nyingine. Hivyo ujahilia wa jana hauna ubora ukilinganishwa na huu wa kisasa wala hauna sifa maalumu ambazo kwa ajili yake Mwenyezi Mungu ameiteremsha Qur'ani na akamtuma mtume, halafu akaucha ujahilia wa kisasa bure bure. Ujahilia wa kisasa ni kiwango gani hunahitajia msuluhishi ambaye ni Alhoja bin Al-Hasani (a.s), Imam Al-Mahdi. Na ni kiasi gani amabavyo tunaihitajia Qur'ani ili ituokoe kutokana na shimo hili la Ujahilia wa kisasa na kutufikisha kwenye kilele cha Uislamu.

QUR'ANI NI TIBA YA MARADHI YETU YAKIJAMII

Sasa umefika wakati tutumie nguvu na juhudi zetu katika kufaidika na uwezo wa Qur'ani wa kuyatibu maradhi ya kibinadamu na tunufaike na nguvu ya Qur'ani kwenye kuufikisha ubinadamu kwenye kilele cha ukamilifu, kwani Qur'ani ni ufunuo, ni yenyekudumu, na yenye kutoa muongozo mpaka siku ya Kiyama. Kudumu chwake ndio nguvu yake ya kubaini maeradhi na ndio nguvu yake ya kutoa tiba na dawa kwa kila jamii, kila zama na kila sehemu. Hivyo hatuna budi kuishaurisha Qur'ani na kuitaka itupe tiba ya mangojwa na maradhi yetu yakijamii nay a mtu mmoja mmoja.

Jamii ikikumbwa na mfarakano na mparaganyiko, basi tiba yake ni kauli yake Mwenyezi Mungu:

[وَاعْتَصِمُواْ بِحَبْلِ اللهِ جَمِيعاً وَلاَ تَفَرَّقُواْ]

"Shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu kwa pamoja wala msifarakane"[٢١١] baada ya kutambua kuwa kamba ya Mwenyezi Mungu ni Qur'ani na Ahlul-bayt (a.s) kwa mujibu wa hadithi tukufu.

Umma ukisibiwa na woga na hofu ya kifo, basi tiba yake ni maneno ya Mwenyezi Mungu:

---

[٢١١] Surat Al-Imran: 103.

[أَيْنَمَا تَكُونُواْ يُدْرِككُّمُ الْمَوْتُ وَلَوْ كُنتُمْ فِي بُرُوجٍ مُّشَيَّدَةٍ]

“Popote mlipo mauti yatakufikieni, na hata mkiwa katika ngome zilizo na nguvu”[٢١٢] , na kauli yake:

[قُلْ إِنَّ الْمَوْتَ الَّذِي تَفِرُّونَ مِنْهُ فإنه مُلاقِيكُمْ]

“Sema: Hayo mauti mnayoyakimbia, bila ya shaka yatakukuteni”[٢١٣] .

Na ikiwa jamii itapatwa na mabalaa na misiba, basi posa na tiba yake ni aya Mwenyezi Mungu:

[أَمْ حَسِبْتُمْ أَن تَدْخُلُواْ الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَأْتِكُم مَّثَلُ الَّذِينَ خَلَوْاْ مِن قَبْلِكُم مَّسَّتْهُمُ الْبَأْسَاء وَالضَّرَّاء وَزُلْزِلُواْ حَتَّى يَقُولَ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ آمَنُواْ مَعَهُ مَتَى نَصْرُ اللهِ أَلا إِنَّ نَصْرَ اللهِ قَرِيبٌ]

“Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, bila ya kukujieni kama yaliyo wajia wale walio pita kabla yenu? Iliwapata shida na madhara na wakatikiswa hata Mtume na walio amini pamoja naye wakasema: Lini nusura ya Mwenyezi Mungu itakuja? Jueni kuwa nusura ya Mwenyezi Mungu ipo karibu”[٢١٤]

Pindi jamii inapohisi hali ya kukata tamaa, basi itambue kuwa tiba yake ni kauli ya Mwenyezi Mungu:

[وَلاَ تَيْأَسُواْ مِن رَّوْحِ اللهِ إِنَّهُ لاَ يَيْأَسُ مِن رَّوْحِ اللهِ إِلاَّ الْقَوْمُ الْكَافِرُونَ]

“Hakika hawakati tamaa na faraji ya Mwenyezi Mungu isipo kuwa watu makafiri”[٢١٥]

[وَمَن يَقْنَطُ مِن رَّحْمَةِ رَبِّهِ إِلاَّ الضَّآلُّونَ]

“Akasema: Na nani anaye kata tamaa na rehema ya Mola wake Mlezi ila wale walio potea?”[٢١٦]

[إِنَّا لَنَنصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ آمَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الأَشْهَادُ]

---

[٢١٢] Surat An-Nisaa: 78.

[٢١٣] Surat Al-Jumu’a: 8.

[٢١٤] Surat Al-Baqarah: 214.

[٢١٥] Surat Yusuf: 87.

[٢١٦] Surat Al-Hijr: 56.

“Hakika bila ya shaka Sisi tunawanusuru Mitume wetu na walioamini katika uhai wa duniani na siku wataposimama Mashahidi”[٢١٧]

Na ikiwa majukumu ya kupotea na dhulma tutawabebesha wengine au tukazibebesha zama, basi natusome maneno ya Mwenyezi Mungu yasemayo:

[وَمَا أَصَابَكَ مِن سَيِّئَةٍ فَمِن نَّفْسِكَ]

“Na ovu liliokusibu linatokana na nafsi yako”[٢١٨]

[إِنَّ اللهَ لاَ يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّى يُغَيِّرُواْ مَا بِأَنْفُسِهِمْ]

“Mwenyezi Mungu habadili yaliyoko kwa watu mpaka wao wabadili yaliyomo nafsini mwao”[٢١٩]

[وَمَا ظَلَمَهُمُ اللهُ وَلَكِنْ أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ]

“Na Mwenyezi Mungu hakuwadhulumu, bali wao wenyewe walidhulumu nafsi zao”[٢٢٠]

Na pindi watu watakapo rejea kwenye kupenda wingi (mali na watoto) hali yao ikiwa ni sawa na msemo huu kwamba: “Kukusanyika na watu ni iddi” bila kutafakari na kufahamu, majibu ya Qur’ani kwao yatakuwa kama ifuatavyo:

[وَمَا أكثر النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ]

“Na wengi wa watu si wenye kuamini hata ukijitahidi”[٢٢١]

[وَإِن تُطِعْ أكثر مَن فِي الأَرْضِ يُضِلُّوكَ عَن سَبِيلِ اللهِ إِن يَتَّبِعُونَ إِلاَّ الظَّنَّ وَإِنْ هُمْ إِلاَّ يَخْرُصُونَ]

“Na ukiwatii wengi katika hawa waliomo duniani watakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu. Hawa hawafuati ila dhana tu, na hawakuwa ila ni wenye kusema uwongo tu”[٢٢٢]

[وَمَا يُؤْمِنُ أَكْثَرُهُمْ بِاللهِ إِلاَّ وَهُم مُّشْرِكُونَ]

---

٢١٧. Surat Al-Ghaafir: 51.

٢١٨. Surat An-Nisaa: 79.

٢١٩. Surat Ar-Ra’d: 11.

٢٢٠. Surat Al-Imran: 117.

٢٢١. Surat Yusuf: 103.

٢٢٢. Surat Al-an’aam: 116.

“Na wengi katika wao hawamuamini Mwenyezi Mungu pasina kuwa ni washirikina”[٢٢٣]

Na miongoni mwa maradhi ya kijamii ambayo Qur’ani imeyatolea tiba ni suala kueneza uvumi[٢٢٤] . Na huu ni ugonjwa hatari sana unao isambaratisha jamii na kukutikisa uwepo wake na kuzigonganisha fikra zake. Katika kulitibu tatizo hili Qur'an’ inasema:

[وَإِذَا جَاءهُمْ أَمْرٌ مِّنَ الأَمْنِ أَوِ الْخَوْفِ أَذَاعُواْ بِهِ وَلَوْ رَدُّوهُ إِلَى الرَّسُولِ وَإِلَى أُوْلِي الأَمْرِ مِنْهُمْ لَعَلِمَهُ الَّذِينَ يَسْتَنبِطُونَهُ مِنْهُمْ وَلَوْلاَ فَضْلُ اللهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ لاَتَّبَعْتُمُ الشَّيْطَانَ إِلاَّ قَلِيلاً]

“Na linapowafikia jambo lolote liliohusu amani au la kitisho wao hulitangaza. Na lau kuwa wangeli lipeleka kwa Mtume na kwa wenye mamlaka kati yao, wale wanao chunguza wangeli lijua. Na lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema yake mngeli mfuata Shet'ani ila wachache wenu tu”[٢٢٥] , na aya zingine nyingi ambazo hutoa tiba ya maradhi yetu ya muda mrefu.

MASOMO TUJIFUNZAYO KUTOKANA NA NAMNA QUR’ANI INAVYOJENGA JAMII

Hapa inatubidi kuashiria baadhi ya masomo tunayoweza kujifunza kutokana na namna Qur’ani inavyojenga na kuongoza jamii:

١. Umakinifu katika kutambua sababu na chanzo kuliko kujua athari wakati kutoa utatuzi wa hali maalumu, n jambo ambalo ni muhumu na ladharura. Mgonjwa aendapo kwa daktari na kumueleza hali anayo jisikia, bila shaka jambo la muhimu alifanyalo daktari huwa ni kuainisha na kugundua sababu kisha ndio hutoa matibabu yake. Ama kutosheka na matibabu ya athari za maradhi husika, kama vile: maumivu ya kichwa, au tumbo kuuma, au kupanda kiwango cha choto la mwili bila kubainisha sababu na chanzo hasa cha hizo athari, ni fikra mbovu kabisa. Ikiwa mtu atataka kutibu hali ya

---

٢٢٣. Surat Yusuf: 106.

٢٢٤. Baadae kilichapwa kijitabu kuhusiana mada hii, katika mfululizo ujulikanao kwa jina la: (Kuilekea Jamii Iliyosafi)

٢٢٥. Surat An-Nisaa: 83.

kutojistiri kwa akina mama, au hali ya vijana kuiga mila za kimagharibi, au watu kutotoa Khumsi au kutotekeleza ibada ya sala, au kufanya kwao machafu mfano wa kunywa pombe na kufanya ushoga, au kwa umla sema: watu kutotekeleza sheria za Mwenyezi Mungu na kufanya kwao makusudi kwenda kinyume na sheria hizo, haitoshi kuwaambia kuwa: jambo ni wajibu hivyo litekelezeni na hili ni haramu liacheni, kwa sababu wao ni Waislamu na yote haya wanayajua, hivyo ni lazima kwanza kutambua sababu ya udhaifu wa msukumo wao wa kidini, msukumo ambao ndio chachu ya kutekeleza na kutii sheria, kisha baada ya hapo ndio kutolewe tiba na suluhisho lake. Hapa utaona kwamba udhaifu wa msukumo wa kidini, chanzo chake ni udhaifu wa kimaadili na kiimani kwa jamii, ndio maana Qur'ani katika mji wa Makka –wakati ikianza kuteremka kwake– ilijikita kwenye mambo haya mawili. Qur'ani ilifafanua imani na ikaitetea kwa hoja na dalili mbalimbali, na ikatoa majibu ishikali na maswali yaliyokuwa yakielekezwa kwenye imani hiyo, na mara nyingi ilikuwa ikiyaamsha maumbile ya watu, kwa sababu maumbile salama ni hoja na dalili ya ndani kwa ndani iliyomo ndani mwa kila mwanadamu kiasi cha kutoweza kuikanusha na kuikataa. Lakini pia kwa upande wa pili, Qur'ani ililipa umuhimu suala la kuelezea matukio ya siku Kiyama, na kutaja desturi na kanuni za Mwenyezi Mungu kwa umati zilizopita, na kusimulia matukio mengi yenye mazingatio na somo, ili kuziamsha akili zao na kuzisafisha nyoyo zao, baada ya hayo ndio ikawalazimisha kutekeleza sheria nao wakakakubali kwa hiyari. Na tunatambua kuwa kipindi cha malezi ndani ya Makka kilikuwa ni kirefu kuliko kile cha sheria ndani ya Madina. Na kutokana na hayo tunafahamu ni namna gani inavyotakiwa kulipa umuhimu jambo la kuzingatia sababu kuliko athari.

٢. Kutokana na nukta ya kwanza tunahamu pia udharura wa kuijenga shakhsia ya Muislamu kimaadili na kiimani. Na Qur'ani katika hili ilitumia njia kadhaa nilizo zitaja katika masomo yaliyojulikana kwa jina la: (Na turejee kwa Mwenyezi Mungu), kiasi kwamba nilisema huko: Qur'ani ilitumia njia ya ulimwengu tatu anazo ziishi mwanadamu (akili, moyo na roho). Kwa mfano: inahusiha baina ya mbingu kuzuia baraka zake, na ardhi kutotoa kheri zake na watu waovu kutawala na kutopokelewa dua, inataja kuwa sababu na

chanzo cha vyote hivyo ni mwanadamu kujinga mbali na sheria ya Mwenyezi Mungu na kuacha kutekeleza faradhi ya kuamrisha mema na kukataza maovu, na kwamba mwenyekutaka kuepukana na matokeo haya mabaya, basi na atekeleze faradhi hii. Imekuja katika hadithi kwamba:

(إذا تركتم الأمر بالمعروف والنهي عن المنكر نزعت عنكم البركات ونزلت عليكم البليّات وسلطت عليكم شراركم ثم تدعون فلا يستجاب لكم)

"Mtakapoacha kuamrisha mema na kukataza maovu, basi zitaondolewa kwenu baraka, na mtateremkiwa na mabalaa, na watakuwaleni waovu wenu, kisha mtaomba hamtajibiwa"[٢٢٦] .

Njia muhimu zaidi katika hizo tuliiashiria hapo kabla, ambayo ni kuelezea hali nzito ya umauti na yale yaliko baada yake, na yale yatakayo kuwa siku Kiyama, na majibizano ya makafiri na waovu motoni pamoja na mashetani wao, halikadhalika kukumbusha ada ya Mwenyezi Mungu kwa wenyekuacha kumtii. Mwenyezi Mungu anasema:

[دَمَّرَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ وَلِلْكَافِرِينَ أَمْثَالُهَا]

"Mwenyezi Mungu aliwaangamiza, na kwa makafiri hawa itakuwa mfano wa hayo"[٢٢٧] ,

[فَأَخَذَهُمُ اللَّهُ بِذُنُوبِهِمْ وَاللَّهُ شَدِيدُ الْعِقَابِ]

"Basi Mwenyezi Mungu aliwashika kwa sababu ya madhabi yao, na Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu"[٢٢٨] , na kwa kutaja neema zake zisizo hisabika wala kudhibitiwa kwa waja wake, nao wakiwa nwenye kuukubali ukweli huu utokanao na maumbile yao kwaba:

[هَلْ جَزَاء الإِحْسَانِ إِلا الإِحْسَانُ]

---

[٢٢٦] Tah'dhiibul Ahkaam: 6/176.

[٢٢٧] Surat Muhammad: 10.

[٢٢٨] Surat Al-Imran: 11.

“Hakuna malipo ya ihsani ila ni ihsani”[٢٤] kisha ikabainishwa furaha ambayo hujenga na kuimarisha moyo wa mwanadamu, na maisha yake na jamii yake, iwapo atatekeleza sheria ya Mwenyezi Mungu. Anasema Mwenyezi Mungu mtukufu:

[وَلَوْ أَنَّ أَهْلَ الْقُرَى آمَنُواْ وَاتَّقَواْ لَفَتَحْنَا عَلَيْهِم بَرَكَاتٍ مِّنَ السَّمَاء وَالأَرْضِ]

“Na lau watu wa miji wangeliamani na wakamchamugu, kwa yakini tungeliwafungulia baraka kutoka mbinguni na katika ardhi “[٢٥].

Hakika Imani na maadili wema ndivyo ambavyo huweka malengo ambayo atayaishi wanadamu, kama ambvyo kuaisha mwelekeo wake. Kwa mfano: inapotakiwa kujitolea kwa ajili jambo la kheri au kumsaidia mtu mwenye uhitaji, ni nani ambaye atakae harakia kuliendea hilo: muumini au ambaye anatafura radhi ya Mwenyezi Mungu aliyetakasika na kawa anahitaji badala kutoka kwake au yule aliye mbali na dini ambaye hima yake kubwa ni kujikusanyia vya duniani na miongoni mwa wale:

[قَدْ يَئِسُوا مِنَ الآخِرَةِ كَمَا يَئِسَ الْكُفَّارُ مِنْ أَصْحَابِ الْقُبُورِ]

“Walikwisha kata tamaa ya Akhera, kama makafiri walivyowakatia tamaa watu wa makaburini”[٢٦]

Bila shaka wakwanza ndiye atakayeharakia jambo hilo. Hii ndio athari ya imani na maadili mema katika kumsukuma mwanadamu kwenye utekelezaji wa sheria, kwani lengo la muumini ni Mwenyezi Mungu aliyetukuka. Basi kuweni wana wa Akhera wa msiwe katika wana wa dunia, kwa sababu kuporomoka na kupotea kwa kila umma kulitokana na kupoteza kwake lengo ambalo ulipaswa uliishi, na hivyo, njia nyingie zikawatenga na njia ya Mwenyezi Mungu kama ilivyokuja katika Qur’ani:

[وَأَنَّ هَذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيماً فَاتَّبِعُوهُ وَلاَ تَتَّبِعُواْ السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِ ذَلِكُمْ وَصَّاكُم بِهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ]

[٢٤] Surat Ar-Rahman: 60.

[٢٥] Surat Al-A’araaf: 96.

[٢٦] Surat Al-Mumtahana:

“Na kwa hakika hii ndiyo njia yangu iliyonyooka. Basi ifuatani, wala msifuate njia nyingine, zikakutengeni na njia yake. Haya amekuusieni ili mpate kumchamungu”[٢٣٢].

Hivyo hatuna namna zaidi ya kulijaza pengo hili katika akili na nyoyo za jamii ili mwelekeo wake inyooke na maisha yake yafuate nidhamu aliyoitaka Mwenyezi Mungu, lakini pia tunapaswa kuichukua njia ya Qur’ani katika kuzihuisha nyoyo na kuzilanisha, na katika kuzilea nafsi na kuzimezesha imani ya haki ambao ndio chimbuko la maadili mema. Mwenyezi Mungu anasema:

[أَلَمْ يَأْنِ لِلَّذِينَ آمَنُوا أَن تَخْشَعَ قُلُوبُهُمْ لِذِكْرِ اللَّهِ وَمَا نَزَلَ مِنَ الْحَقِّ وَلا يَكُونُوا كَالَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِن قَبْلُ فَطَالَ عَلَيْهِمُ الأَمَدُ فَقَسَتْ قُلُوبُهُمْ وَكَثِيرٌ مِّنْهُمْ فَاسِقُونَ]

“Je, wakati haujafika kwa wale walioamini kwamba nyoyo zao zinyenyekee kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kwa mambo ya haki yaliyoteremka? Wala wasiwe kama wale waliopewa Kitabu kabla yao na muda wao ukawa mrefu, kwa hivyo nyoyo zao zikawa ngumu, na wengi wao wakawa wapotovu”[٢٣٣].

Na huu ni mlengo unapaswa kuingiwa na kila mwanafikra na mwana malezi, kwani ndio njia ya Qur’ani katika kuwaidhi na kuhuisha nyoyo, na aya zote za Qur’ani kama mwenye akili angelizichunguza bila shaka angelisahihisha mfumo wa maisha yake kama asemavyo Mwenyezi Mungu katika surat Ad-Dukhan:

[كَمْ تَرَكُوا مِن جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ، وَزُرُوعٍ وَمَقَامٍ كَرِيمٍ، وَنَعْمَةٍ كَانُوا فِيهَا فَاكِهِينَ، كَذَلِكَ وَأَوْرَثْنَاهَا قَوْماً آخَرِينَ، فَمَا بَكَتْ عَلَيْهِمُ السَّمَاء وَالأَرْضُ وَمَا كَانُوا مُنظَرِينَ]

“Mabustani mangapi, na chemchem ngapi waliziacha! Na mimea na vyeo vitukufu! Na neema walizo kuwa wakijistareheshea! Ndio hivyo! Na tukawarithisha haya watu wenginewe. La mbingu wala ardhi hazikuwalilia, wala hawakupewa muhula”[٢٣٤].

[٢٣٢] Surat Al-An’aam: 153.

[٢٣٣] Surat Al-Hadiid: 16.

[٢٣٤] Surat Ad-Dukhan: 25-29.

Nami ninakunasihini kusoma kitabu cha Al-Qalbu As-Saliim ambacho kina juzuu mbili, juzuu ya kwanza inahusu imani na nyingine inahusu maadili ambazo zimetoka katika moyo wenye nia safi na uliotakasika.

٣. Kufuata mpangilio katika kutoa hidaya, na kusuluhisha na kuwaongoa watu kwa upole. Na mfano uliyo wazi wa hilo ni: uharamishwaji wa pombe – ikizingatiwa kuwa ilikuwa ni ada na kawaida iliyo jikita katika jamii na zikanyweshwa nyoyo zao na akili zao- ambao ulifuata hatua zifuatazo:

[يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ قُلْ فِيهِمَا إِثْمٌ كَبِيرٌ وَمَنَافِعُ لِلنَّاسِ و إِثْمُهُمآ أَكْبَرُ مِنْ نَفْعِهِمَا]

“Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari. Waambie: katika hayo mna uovu mkubwa na manufaa (kidogo) kwa watu, na uovu wake ni mkubwa zaidi kuliko manufaa yake”[٢٣٦] .

Baadhi ya waislamu ilipoteremka aya hiyo waliesema: Hatutakunywa pombe; kwa sababu ni uovu na Mwenyezi Mungu ameharamisha mambo machafu yaonekanayo na yale yaliyofichikana na uovu, wakati wengine walisema: Tutakunywa kiasi chenye manufaa ndani yake, hapo ndipo Mwenyezi Mungu akateremsha kauli yake isemayo:

[لاَ تَقْرَبُواْ الصَّلاَةَ وَأَنتُمْ سُكَارَى حَتَّىَ تَعْلَمُواْ مَا تَقُولُونَ]

“Msikaribie swala hali ya kuwa mmelewa mpaka mjue mnayo yasema”[٢٣٧] Baadhi yao wakajiziwia kunywa pombe, wakasema: Hatuwezi kutumia kitu kinachokwenda kinyume na swala, wakatu huu ndio ikateremka aya ya surat Al-Maidah ambayo ililipa mkazo zuwio hilo kwa kusema:

[يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ إِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالأَنصَابُ وَالأَزْلاَمُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ فَاجْتَنِبُوهُ]

“Enyi mlio amini! Hakika pombe na kamari na kupiga ramli ni uchafu wa kazi ya shetani, basi jiepusheni nayo”[٢٣٨] .

Na lengo ya kushuka Qur’ani kwa utaratibu kwa kipindi cha miaka (23) ilikuwa ni kutatua matatizo ya jamii hapo kwa hapo kwa kuzingatia zama,

---

[٢٣٦] Surat Al-Baqarah: 219.

[٢٣٧] Surat An-Nisaa: 43.

[٢٣٨] Surat Al-Maidah: 90.

sehemu, na mazingira ya tukio. Halikadhali zilizingatiwa tofauti za kiwango cha watu na uwezo wao wa upokeaji na utekelezaji wa maamrisho na makatazo.

Na inawezekana mpangilio wa kuremka aya ukawa katika namna mbalimbali. Kwa mfano, tunapotaka kutatua hali fulani ya kijamii iliyokita mizizi -kama vile ada za kikabila-, kwanza tunatakiwa tuanze kuweka alama za viulizo juu ya usahihi wake, malengo yake na kuitilia mashaka, kisha ndio tuanze kutoa njia mbadala na uchaguzi mwingine utakaokuwa mkabala wa ile hali. Tukiweza kuzitia mashakini nyoyo juu ile hali, na watu wakaanza kuelekea mbadala ulio bora, basi hali ya kuridhika kuibadili ile ya mwanzo itaanza, wakati huo ndio inawezekana kuishambulia ile hali ili kuiondoa, lakini kuanza kuikabili bila kufanya maandalizi maana yake ni kufeli na kushindwa vibaya, kwani maadamu bado hali hiyo imejikita na mamumbile ya watu yameumbwa ni wenye kupenda kuheshimu mila na desturi walizorithi na kuzinyenyekea, hivyo wenye mila zao wote watakuwa tayari kukabiliani na kila jaribio lenye lengo la kubadilisha ada na kawaida yao hiyo ya kijamii.

Kwa mfano bwana mtume (s.a.w.w) alopopewa utume hakuyashambulia masanamu moja kwa moja, bali alianza kumuambudu Mwenyezi Mungu akiwa na Ali (a.s) na Bi Khadija (a.s) mbele ya Makuraishi bila kuyazungumzia masanamu yao kwa ubaya. Lakini bwana mtume (s.a.w.w) kwa kitendo hiki alifungua mlango wa maswali na viulizo vingi: kwamba watatu hawa wananya nini? Ni nani wanayemuabudu? Na ni kwanini wameamua kuachana na mila za watu wao? Lakini pia watu wana ujasiri kiasi gani na wana imani madhubuti kiasi gani katika nyoyo zao mpaka wakaweza kusimama dhidi ya watu wote kwa amani bila woga?.... Hivi viulizo vilipelekea kundi la watu kuingia kwenye Uislamu – rejea kisa cha Abdullah Bin Masoud katika vitabu vya historia- bila kushambuliwa na Makuraishi, kwa sababu bwana mtume (s.a.w.w) hakuamsha hisia zao tofauti na angeliyataja masanadu kwa ubaya mojo kwa moja.

٤. Kuyapa umuhimu na kuuelekeza umma wa Kiislamu kwenye yele mambo ya msingi ambayo ndio yanauhifadhi, hasahasa yale ambayo yanafahamika

kuwa yaliachwa na kupuuzwa baada ya mtume (s.a.w.w) na ambayo alikuwa akiyahimiza sana, kama vile: kuamrisha mema na kukataza mabaya, uimamu na uongozi kwa ajili waumini, na kuwapinga makarifi na kuwapenda ndugu wa karibu, na kushikamana na Qur'ani na kizazi cha mtume (s.a.w.w), na kuchunga miskiti, na swala za jamaa na Ijuamaa, mambo ambayo baada ya kufariki kwake (s.a.w.w) Umma wa Kiislamu uliipuuzia misingi hii madhubuti yenye lengo la kuulinda Umma, na hapo ndio kasi ya kupotea ikaanza kwa haraka, hivyo kureje kwenye wema na kuerebishaji wa jamii kunategemea kuifanikisha misingi hii na kuirejesha kwenye maisha ya jamii.

٥. Kumpunguza matatizo na taabu anazokabiliana nazo yule mtu ambaye hufanya hujudi ya kurekebisha jamii na kuongoa au kama tulivyomwita huko nyuma: mbeba Qur'ani ikiwa ni ujmbe wa islahi na kurekebishaji wa jamii. Mwenyezi Mungu anasema:

[المص، كِتَابٌ أُنزِلَ إِلَيْكَ فَلاَ يَكُن فِي صَدْرِكَ حَرَجٌ مِّنْهُ لِتُنذِرَ بِهِ وَذِكْرَى لِلْمُؤْمِنِينَ]

"Alif Lam Mym 'Saad. Kitabu kilicho teremshwa kwako – basi isiwe dhiki kifuani kwako kwa ajili yake, upate kuonya kwacho, na kiwe ni ukumbusho kwa Waumini"[٢٣٨] ,

[فَلَعَلَّكَ تَارِكٌ بَعْضَ مَا يُوحَى إِلَيْكَ وَضَآئِقٌ بِهِ صَدْرُكَ أَن يَقُولُواْ لَوْلاَ أُنزِلَ عَلَيْهِ كَنزٌ أَوْ جَاء مَعَهُ مَلَكٌ]

"Basi labda utaacha baadhi ya yale yaliyo funuliwa kwako, na kifua kitaona dhiki kwa hayo, kwa sababu wanasema: Mbona hakuteremshiwa khazina, au wakaja naye Malaika? Wewe ni mwonyaji tu, na Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi wa kila kitu"[٢٣٩] ,

[وَاصْبِرْ وَمَا صَبْرُكَ إِلاَّ بِاللهِ وَلاَ تَحْزَنْ عَلَيْهِمْ وَلاَ تَكُ فِي ضَيْقٍ مِّمَّا يَمْكُرُونَ، إِنَّ اللهَ مَعَ الَّذِينَ اتَّقَواْ وَّالَّذِينَ هُم مُّحْسِنُونَ]

"Na subiri. Na kusubiri kwako kusiwe ila kwa sababu ya MwenyeziMungu tu. Wala usiwahuzunikie; wala usiwe katika dhiki kwa hila wanazozifanya. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wenye kumcha, na watendao mema"[٢٤٠] ,

---

٢٣٨. Surat Al-A'raaf: 1-2.

٢٣٩. Surat Hud: 12.

٢٤٠. Surat An-Nahl: 127-128.

[لَتُبْلَوُنَّ فِي أَمْوَالِكُمْ وَأَنفُسِكُمْ وَلَتَسْمَعُنَّ مِنَ الَّذِينَ أُوتُواْ الْكِتَابَ مِن قَبْلِكُمْ وَمِنَ الَّذِينَ أَشْرَكُواْ أَذىً كَثِيراً وَإِن تَصْبِرُواْ وَتَتَّقُواْ فإن ذَلِكَ مِنْ عَزْمِ الأُمُورِ]

“Hapana shaka yoyote mtapata misukosuko katika mali zenu na nafsi zenu, na bila ya shaka yoyote mtasikia udhia mwingi kutokana na walio pewa Kitabu kabla yenu na wale walio shiriki. Na ikiwa mtasubiri na mkamchamngu basi hakika hayo ni katika mambo ya kuazimia”[٢٤] . Na ibara yenye upole zaidi ni kaule yake Mwenyezi Mungu:

[وَاصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ فَإِنَّكَ بِأَعْيُنِنَا]

“Na ingojee hukumu ya Mola wako Mlezi. Kwani wewe hakika uko mbele ya macho yetu”[٢٥] , macho ya uangalizi, macho ya upole, rehema, ulinzi, muongozo, muono nk.

Na utaona sura kamili imeteremka kwa ajili ya lengo hili hili, kama vile: surat Yusuf ambao unahisi kabisa kwamba iliteremka katika kipindi kigumu alichokiishi mtume (s.a.w.w) ndani ya Makka na kabla kuhamia Madina, ambapo alimkosa msaidizi kwa kufariki dunia Abu Talib na Bi Khadija (a.s), akawa amekata tamaa ya Makuraishi kuingia katika Uislamu, lakini pia akawa amejaribu kutafuta kimbilio lingine tofauti Makka kama vile Taif, hakufanikiwa, dunia ikawa ni dhiki kwa waumini, katika kipindi hicho ndipo iliteremka surat Yusuf ikiwasimulia namna ndugu zake na Yusuf walivyopanga njama dhidi ya ndugu yao mdogo, wakamtupa kisimani, jambo ambalo kwa mazingira ya kawaida maana yake ni kifo, lakini Mwenyezi Mugu akamtumia msafara uliomuokoa, kisha akauzwa kwenye nyumba ya mfalme wa Misri, akaingia kwenye mtihani wa mke wa muheshimiwa na wanawake wengine, akafungwa miaka kadhaa, lakini Mwenyezi Mungu aliyetukuka akamuokoa na kifungo, na akamfundisha tafsiri ya ndoto, na kwa baraka za Mwenyezi Mungu akapata kile cheo cha kuaminiwa kusimamia hazina ya Misri, kisha akawa mfalme wa Misri baada ya kuzimiliki nyonyo za watu kwa maadili yake mema na usimamizi wake mzuri. Hapa ndipo walipokuja wale ndugu wapanga njama mbele yake wakiwa ni dhalili, lakini yeye kwa moyo wake wenye huruma akawasamehe huku akisema:

---

٢٤. Surat Al-Imran: 186.

٢٥. Surat At-Tur: 48.

[لاَ تَثْرِيبَ عَلَيْكُمُ الْيَوْمَ يَغْفِرُ اللهُ لَكُمْ وَهُوَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ]

“Leo hapana lawama juu yenu. Mwenyezi Mungu atakusameheni, naye ni Mwingi wa kurehemu kuliko wote wanao rehemu”[٢٤٣] , na hatima yake Mwenyezi Mungu akamkutanisha kwa mara nyingine na baba yake na kaka yake. Na bwana mtume (s.a.w.w) pia alilitumia neno lile lile lililotumiwa na Yusuf pindi Makuraishi walipofanyia kitendo kile kile cha kumfanyia njama na kutaka kumuuwa, kisha Mwenyezi Mungu akamnusuru dhidi yao na akamuwezesha juu yao ndani mji wao wa Makka, hapo ndipo bwana mtume (s.a.w.w) aliwakariria neno lile la ndugu yake Yusuf mkarimu (a.s) akasema (s.a.w.w): “Leo hakuna lawama juu. Nendeni nyinyi mpo huru”. Hayo aliyasema baada ya kuwauliza: Mnadhani nitanyaje dhidi yenu? Wakasema: “Wewe ni ndugu mwema na mwana wa ami mwema”[٢٤٤] , na huku ni kukiri kwa juu ya utukufu wa dhati ya bwana mtume (s.a.w.w). ٤

٦. Kuhimiza juu utafutaji wa elimu na kujifunza kila kitachomuweka mtu karibu na Mwenyezi Mungu aliyetakasika na kinamuongezea kumjua Yeye. Imesemekana kuwa ndani ya Qur’ani kuna zaidi ya aya mia tano (500) zinazihimiza juu ya elimu, na kutafakari na kuwasifu wasomi, na huku zikitia dosari ujinga na wajinga na zikieleza mwisho wao. Qur’ani imefikia hatua ya kuifanya sifa ya ujuzi na elimu na kumjua Mwenyezi Mungu kuwa ni sababu ya kuongezewa nguvu waumini dhidi ya maadui wao mara kumi zaidi, kama inavyofahamika mwishoni mwa aya ifuatayo:

[يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ حَرِّضِ الْمُؤْمِنِينَ عَلَى الْقِتَالِ إِن يَكُن مِّنكُمْ عِشْرُونَ صَابِرُونَ يَغْلِبُواْ مِئَتَيْنِ وَإِن يَكُن مِّنكُم مِّئَةٌ يَغْلِبُواْ أَلْفاً مِّنَ الَّذِينَ كَفَرُواْ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لاَّ يَفْقَهُونَ]

“Ewe Nabii! Wahimize Waumini wende vitani. Wakiwapo kati yenu ishirini wanao subiri watawashinda mia mbili. Na wakiwapo kati yenu mia watawashinda elfu moja katika walio kufuru. Kwa sababu wao ni watu wasio fahamu”[٢٤٥] , wakati subira ambayo ni katika sababu muhimu za ushindi umepewa hadhi ya kuzidisha nguvu mara moja tu:

---

٢٤٣. Surat Yusuf: 92.

٢٤٤. Tafsirun Nuur At-Taqalayn: 2/460.

٢٤٥. Surat Al-Anfaal: 65.

[الآنَ خَفَّفَ اللهُ عَنكُمْ وَعَلِمَ أَنَّ فِيكُمْ ضَعْفاً فإن يَكُن مِّنكُم مِّئَةٌ صَابِرَةٌ يَغْلِبُواْ مِئَتَيْنِ وَإِن يَكُن مِّنكُمْ أَلْفٌ يَغْلِبُواْ أَلْفَيْنِ بِإِذْنِ اللهِ وَاللهُ مَعَ الصَّابِرِينَ]

"Sasa Mwenyezi Mungu amekupunguzieni, na anajua kuwa upo udhaifu kwenu. Kwa hivyo wakiwa wapo watu mia moja kati yenu wenye kusubiri watawashinda mia mbili. Na wakiwapo elfu moja watawashinda elfu mbili, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu yu pamoja na wenye kusubiri"[٢٤٦] .

MIONGONI MWA UFAHAMU WA KUPAMBANA NA MAKAFIRI NA MASHETANI

Ufahamu huu umekusanya nyanja zote za maisha. Basi ni fikra zipi zilizotolewa na Qur'ani, ambazo tunaweza kuzitambua kuwa ni uelewa wa kupambana na makafiri? Mwenywzi Mungu anasema:

[وَلاَ تَهِنُواْ فِي ابْتِغَاء الْقَوْمِ إِن تَكُونُواْ تَأْلَمُونَ فَإِنَّهُمْ يَأْلَمُونَ كَمَا تَأْلَمونَ وَتَرْجُونَ مِنَ اللهِ مَا لاَ يَرْجُونَ وَكَانَ اللهُ عَلِيمًا حَكِيماً]

"Wala msifanye ulegevu kuwafukuzia kaumu ya maadui. Ikiwa mnaumia, basi nao pia wanaumia kama mnavyo umia nyinyi. Nanyi mnataraji kwa Mwenyezi Mungu wasio yataraji wao. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye hikima"[٢٤٧] . Kwanini kukimbia kupambana nao wakati madhara huzipata mbande mbili? Na tofauti n kwamba nyinyi mnataji (malipo) yale yaliyopo kwa Mwenyezi Mungu siku ya Akhera wala kumna hasara, wakati wao hawaraji kwake chochote isipokuwa adhabu iumizayo. Na Mwenyezi Mungu anasema:

[وَظَنُّوا أَنَّهُم مَّانِعَتُهُمْ حُصُونُهُم مِّنَ اللَّهِ فَأَتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ حَيْثُ لَمْ يَحْتَسِبُوا وَقَذَفَ فِي قُلُوبِهِمُ الرُّعْبَ يُخْرِبُونَ بُيُوتَهُم بِأَيْدِيهِمْ وَأَيْدِي الْمُؤْمِنِينَ فَاعْتَبِرُوا يَا أُولِي الأَبْصَارِ]

"Nao walidhani kuwa ngome zao zitawalinda na Mwenyezi Mungu. Lakini Mwenyezi Mungu aliwafikia kwa mahali wasipo patazamia, na akatia woga katika nyoyo zao. Wakawa wanazibomoa nyumba zao kwa mikono yao na mikono ya waumini. Basi zingatieni enyi wenye macho"[٢٤٨] . Sehemu anasema: ٤

[٢٤٦] Surat Al-Anfaal: 66.

[٢٤٧] Surat An-Nisaa: 104.

[٢٤٨] Surat Al-Hash'r: 2.

[مَا كَانَ لأَهْلِ الْمَدِينَةِ وَمَنْ حَوْلَهُم مِّنَ الأَعْرَابِ أَن يَتَخَلَّفُواْ عَن رَّسُولِ اللهِ وَلاَ يَرْغَبُواْ بِأَنفُسِهِمْ عَن نَّفْسِهِ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ لاَ يُصِيبُهُمْ ظَمَأٌ وَلاَ نَصَبٌ وَلاَ مَخْمَصَةٌ فِي سَبِيلِ اللهِ وَلاَ يَطَؤُونَ مَوْطِئًا يَغِيظُ الْكُفَّارَ وَلاَ يَنَالُونَ مِنْ عَدُوٍّ نَّيْلاً إِلاَّ كُتِبَ لَهُم بِهِ عَمَلٌ صَالِحٌ إِنَّ اللهَ لاَ يُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ، وَلاَ يُنفِقُونَ نَفَقَةً صَغِيرَةً وَلاَ كَبِيرَةً وَلاَ يَقْطَعُونَ وَادِياً إِلاَّ كُتِبَ لَهُمْ لِيَجْزِيَهُمُ اللهُ أَحْسَنَ مَا كَانُواْ يَعْمَلُونَ]

“Haiwafalii watu wa Madina na Mabedui walio jirani zao kubakia nyuma wasitoke na Mtume, wala kujipendelea nafsi zao kuliko yeye. Hayo ni kwa kuwa hakiwapati kiu, wala machofu, wala njaa, kwa ajili ya Njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawendi mahali panapo waghadhibisha makafiri, wala hakiwapati chochote kutokana na maadui, ila huandikiwa kuwa ni kitendo chema. Hakika Mwenyezi Mungu haupotezi ujira wa wanao fanya mema. Wala hawatoi cha kutoa kidogo wala kikubwa, wala hawalivuki bonde, ila huandikiwa, ili Mwenyezi Mungu awalipe bora ya waliyo kuwa wakiya- tenda”[٢٨] , ni kwanini kuchelea na kupuuzia kuٹoa kile ambacho ndani yake kuna utii wa Mwenyezi Mungu aliyetukuka, katika juhudi na mali? Na kwanini kumdhania Mwenyezi Mungu vibaya, dhana ambayo huwapata watu pindi watu wanapohitajika kutoa haki za kisheria zilizoko katika dhima yao, kama vile: khumsi, zaka nk? Aya nyingine ni:

[ثُمَّ نُنَجِّي رُسُلَنَا وَالَّذِينَ آمَنُواْ كَذَلِكَ حَقّاً عَلَيْنَا نُنجِ الْمُؤْمِنِينَ]

“Kisha Sisi huwaokoa Mitume wetu na walio amini. Ndio kama hivyo, inatustahiki kuwaokoa Waumini”[٢٩] .

Na miongo mwa fikra za kupambana na makafiri, ni aya tukufu za surat Muhammad. Ikiwa utaweza kuhama kwa roho yako, na fikra zako na moyo wako kwenye kile kipindi cha furaha ya maisha mwanadamu, na ukajenga picha kwamba na wewe ni katika lile kundi la waumini lilimzunguka mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), kundi liliambatana naye katika wakati mgumu, mwanzo wa Uislamu, kipindi ambacho walikuwa wanyonge, wakiadhibiwa na Makuraishi adhabu kali, mpaka kufikia Washirikina walipogubikwa na hali ya kushindwa na wakakata tamaa baada ya vita ya Ahzab, kiasi kwamba mtu (s.a.w.w) alikuwa na uwezo wa kaunza mashambulizi, kisha ushindi wa Waislamu ukafululiza kuanzia

[٢٨] Surat At-Tawba: 120-121.

[٢٩] Surat Yunus: 103.

ushindi wa Hudaibiya hadi kwenye ufunguzi wa Makka na ushindi wa Khaibar na Taif, kisha Yemeni na bara nzima la Arabu, jalia kwamba na wewe ulikuwepo huko unateremkiwa na maneo matakatifu ya Qur'ani tukufu iliyotoka kwa Mola wako mlezi mwendeshaji wa mambo yako na muumba mbingu na ardhi, akiongea nawe moja kwa moja ili akuambie:

[بِسْمِ اللهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ] [الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَن سَبِيلِ اللَّهِ أَضَلَّ أَعْمَالَهُمْ، وَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَآمَنُوا بِمَا نُزِّلَ عَلَى مُحَمَّدٍ وَهُوَ الْحَقُّ مِن رَّبِّهِمْ كَفَّرَ عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ وَأَصْلَحَ بَالَهُمْ، ذَلِكَ بِأَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا اتَّبَعُوا الْبَاطِلَ وَأَنَّ الَّذِينَ آمَنُوا اتَّبَعُوا الْحَقَّ مِن رَّبِّهِمْ كَذَلِكَ يَضْرِبُ اللَّهُ لِلنَّاسِ أَمْثَالَهُمْ، فإذا لَقِيتُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا فَضَرْبَ الرِّقَابِ حَتَّى إذا أَثْخَنتُمُوهُمْ فَشُدُّوا الْوَثَاقَ فَإِمَّا مَنّاً بَعْدُ وَإِمَّا فِدَاء حَتَّى تَضَعَ الْحَرْبُ أَوْزَارَهَا ذَلِكَ وَلَوْ يَشَاء اللَّهُ لانتَصَرَ مِنْهُمْ وَلَكِن لِّيَبْلُوَ بَعْضَكُم بِبَعْضٍ وَالَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَلَن يُضِلَّ أَعْمَالَهُمْ، سَيَهْدِيهِمْ وَيُصْلِحُ بَالَهُمْ، وَيُدْخِلُهُمُ الْجَنَّةَ عَرَّفَهَا لَهُمْ، يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِن تَنصُرُوا اللَّهَ يَنصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ، وَالَّذِينَ كَفَرُوا فَتَعْساً لَّهُمْ وَأَضَلَّ أَعْمَالَهُمْ، ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ كَرِهُوا مَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأَحْبَطَ أَعْمَالَهُمْ، أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الأَرْضِ فَيَنظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ دَمَّرَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ وَلِلْكَافِرِينَ أَمْثَالُهَا، ذَلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ مَوْلَى الَّذِينَ آمَنُوا وَأَنَّ الْكَافِرِينَ لا مَوْلَى لَهُمْ، إِنَّ اللَّهَ يُدْخِلُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الأَنْهَارُ وَالَّذِينَ كَفَرُوا يَتَمَتَّعُونَ وَيَأْكُلُونَ كَمَا تَأْكُلُ الأَنْعَامُ وَالنَّارُ مَثْوًى لَّهُمْ، وَكَأَيِّن مِّن قَرْيَةٍ هِيَ أَشَدُّ قُوَّةً مِّن قَرْيَتِكَ الَّتِي أَخْرَجَتْكَ أَهْلَكْنَاهُمْ فَلا نَاصِرَ لَهُمْ، أَفَمَن كَانَ عَلَى بَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّهِ كَمَن زُيِّنَ لَهُ سُوءُ عَمَلِهِ وَاتَّبَعُوا أَهْوَاءهُمْ]

Kwa Jina La Mwenyezi Mungu Mwingi Wa Rehema Mwenye Kurehemu. ''Walio kufuru na wakazuilia njia ya Mwenyezi Mungu, Yeye atavipotoa vitendo vyao. Na walioamini, na wakatenda mema, na wakaamini aliyo teremshiwa Muhammad – nayo ni Haki iliyo toka kwa Mola wao Mlezi – atawafutia makosa yao na ataitengeneza hali yao. Hayo ni kwa sababu walio kufuru wamefuata upotovu, na walio amini wamefuata Haki iliyo toka kwa Mola wao Mlezi. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anavyo wapigia watu mifano yao. Basi mnapo wakuta walio kufuru wapigeni shingoni mwao, mpaka mkiwadhoofisha wafungeni pingu. Tena waachilieni kwa hisani au wajikomboe, mpaka vita vipoe. Ndio hivyo. Na lau angelitaka Mwenyezi Mungu angeliwashinda mwenyewe, lakini haya ni kwa sababu akutieni mitihani nyinyi kwa nyinyi. Na walio uliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu hatazipoteza a'mali zao. Atawaongoza na awatengezee hali yao. Na atawaingiza katika Pepo aliyo wajuulisha. Enyi mlio amini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu naye atakunusuruni na ataithibitisha miguu yenu. Na walio kufuru, basi kwao ni maangamizo, na atavipoteza vitendo vyao. Hayo ni kwa sababu waliyachukia aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, basi akaviangusha vitendo vyao. Kwani hawakutembea katika ardhi wakaona ulikuwaje mwisho wa walio kuwa kabla yao? Mwenyezi Mungu aliwaangamiza, na kwa makafiri hawa

itakuwa mfano wa hayo. Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa walioamini[٢٥]. Na makafiri hawana mlinzi. Hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza walio amini na wakatenda mema katika Bustani zipitiwazo na mito kati yake. Na walio kufuru hujifurahisha na hula kama walavyo wanyama, na Moto ndio makaazi yao. Na miji mingapi iliyo kuwa na nguvu zaidi kuliko mji wako huu ulio kutoa; nao tuliwateketeza na wala hawakuwa wa kuwanusuru. Je! Mwenye kuwa na bayana kutoka kwa Mola wake Mlezi ni kama aliye pambiwa uovu wa vitendo vyake, na wakafuata pumbao lao?[٢٥] ”

[وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُم فِي الأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَى لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُوْلَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ]

“Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia Dini yao aliyo wapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na watao kufuru baada ya hayo, basi hao ndio wapotovu”[٢٥].

Na Mwenyezi Mungu wakati huo huo anawatahadharisha na wanafiki ambao huwatosa waumini wakati wa mapambano na maadui na wakidharau udhaifu wa zana zao hali ya kuwa wameghafilika kuhusu siri ya nguvu ya waumini ambayo ni mahusiano yao na Mwenyezi Mungu aliyetukuka, na hapo ndio akaamua kuwasikilisha kauli yake:

[إِذْ يَقُولُ الْمُنَافِقُونَ وَالَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ غَرَّ هَؤُلاء دِينُهُمْ وَمَن يَتَوَكَّلْ عَلَى اللهِ فإن اللهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ]

“ Na walipo sema wanaafiki, na wale wenye ugonjwa nyoyoni mwao: Watu hawa dini yao imewadanganya. Na Mwenye kumtegemea Mwenyezi Mungu basi

---

[٢٥] Aya hii ndio imebeba sura kamili ya mahujiao haya, kwamba waumini wao wana mlinzi anayesimamia ulinzi wao na malezi yao, furaha na kufaulu kwao, ambaye si mwengine isipokuwa Mwenyezi Mungu aliyetukuka, katati makafiri hawana mlinzi, bali mlinzi wao ni shetani dhaifu anayekumbia wakati wa mapigano na kuwatosa: “Na pale Shet'ani alipo wapambia vitendo vyao, na akawaambia: Hapana watu wa kukushindeni hii leo, na hali mimi ni mlinzi wenu. Yalipo onana majeshi mawili, akarudi nyuma, na akasema: Mimi si pamoja nanyi. Mimi naona msiyo yaona. Mimi namwogopa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu”. Surat Al-Anfaal: 48.

[٢٥] Surat Muhammad: 1-14.

[٢٥] Surat An-Nur: 55.

hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Ametukuka, na Mwenye hikima”[٢٩٤].

Na huingia ndani ya aya za ufamu wa mapambao na makafiri kila ahadi ya Mwenyezi Mungu ya ushindi, na kurithisha ardhi, na kwamba mwisho mwema ni waumini, na kwamba Mwenyezi Mungu yupo nao, na huwateremkiwa na malaika kwa utulivu kutoka kwa Mola wao mlezi, na kwamba atawaondolea hofu na huzuni, na mkataba alioufunga nao kwamba anazinunua nafsi na mali zao na kwamba malipo yao itakuwa ni pepo, vile vile zidisho la kumkopesha Mwenyezi Mungu na kutoa katika njia yake, na ahadi zingine nyingi ambazo hatuwezi kuzifafanua katika muhtasari huu.

Ama ukeli mkubwa unaothibitishwa na Qur’ani katika hili ni kwamba kushindwa na adui wa nje na dhahiri –makafiri– ni tawi la kushindwa na adui wa ndani ya nafsi yenyekuamrisha maovu, ambaye ni shetani. Ndio maana utaiona Qur’ani inapowaahidi waumini uongozi wa ardhi na kwamba ndio watakaoirithi na walioko juu yake, inafanya hatua ya kwanza kabisa kuwa ni kujenga na kusuluhisha mambo na kutekeleza mfumo wa Mwenyezi Mungu juu ya nafsi, anasema Mwenyezi Mungu:

[وَنُرِيدُ أَن نَّمُنَّ عَلَى الَّذِينَ اسْتُضْعِفُوا فِي الأَرْضِ وَنَجْعَلَهُمْ أَئِمَّةً وَنَجْعَلَهُمُ الْوَارِثِينَ، وَنُمَكِّنَ لَهُمْ فِي الأَرْضِ وَنُرِي فِرْعَوْنَ وَهَامَانَ وَجُنُودَهُمَا مِنْهُم مَّا كَانُوا يَحْذَرُونَ]

“Na tukataka kuwafadhili walio dhoofishwa katika nchi hiyo na kuwafanya wawe waongozi na kuwafanya ni warithi. Na kuwapa nguvu katika nchi, na kutokana na wao kuwaonyesha kina Firauni na Hamana na majeshi yao mambo yale waliyo kuwa wakiyaogopa”[٢٩٥]. Hivyo kwanza kawafanya viongozi, ambayo ina maana kuwa kuzitaka dhati zao na kuzitenga mbali na uchafu, na linalotia nguvu hilo ni kuwa hakuna thamani ya kuwashinda makafiri ikiwa ushindi huo hautambatana na kumshinda shetani na kufanya mambo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu aliyetakasika, kwa sababu jambo lisilokuwa kwa ajili ya kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu,

---

٢٩٤. Surat Al-Anfaal: 49.

٢٩٥. Surat Al-Qasas: 5-6.

wakati huo hakutakuwa na tofauti ya waumini na makafiri, bali wote watakuwa sawa, na wote watakuwa ni watu wa dunia na Akhera hawatakuwa na fungu lolote.

Kwa mfano: kushindwa waislamu katika vita ya Uhudi na hasara kubwa iliyowakuta, Mwenyezi Mungu anawambia:

[إِنَّ الَّذِينَ تَوَلَّوْاْ مِنكُمْ يَوْمَ الْتَقَى الْجَمْعَانِ إِنَّمَا اسْتَزَلَّهُمُ الشَّيْطَانُ بِبَعْضِ مَا كَسَبُواْ]

"Hakika wale waliorudi nyuma miongoni mwenu siku yalipo pambana majeshi mawili, Shetani ndiye aliye watelezesha kwa sababu ya baadhi ya makosa waliyo yafanya..."[٢٩٦] , kwamba kushindwa na kukimbia kwâo vilikuwa ni kwa sababu ya maovu waliyoyafanya, wakati mukabala wa hayo anasema:

[إِن تَنصُرُوا اللَّهَ يَنصُرْكُمْ]

"Mkimnusuru Mwenyezi Mungu naye atakunusuruni"[٢٩٧] , na ushindi wa Mwenyezi Mungu hupatikana kwa kumtii yeye, tofauti na hivyo, Yeye si muhitaji wa walimwengu, na hali ipo hvyo hivyo katika iliyotangulia isemayo: "Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini katika nyinyi...", na ndio maana bwana mtume (s.a.w.w) akazungumza na msafara wa wapingana jihadi waliokuwa wamerudi kutoka vitani kwa kusema: "Karibuni, mmemaliza jihadi (vita) ndogo na mmebakiwa na jihadi kubwa. Wakamuuliza: Ni ipi jihadi kubwa ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu? Ni jihadi ya nafsi. Mtume akajibu"[٢٩٨] .

UTAWALA GHASIBU WA KIZAYUNI NI ATHARI YA UGONJWA, BASI NYINYI TIBUNI ASILI UGONJWA

Waislamu wanapolipa umuhimu suala la utawala ghasibu wa Kizayuni na wakafanya juhudi za kuuondoa, ni lazima watambue kuwa utawala huu si chochote ila ni moja athari za ugongwa ambao unaonekena kwenye mwili wa Umma wa Kiislamu ikiwa ni tija ya uwepo wa ugonjwa lililojificha ndani yake, ugonjwa ambao ndio asili na sababu ya maumivu haya. Ama ugonjwa wenyewe ni Waislamu kujitenga na mfumo na njia ya Mwenyezi Mungu maishani mwao. Hivyo,

---

٢٩٦. Surat Al-Imran: 155.

٢٩٧. Surat Muhammad: 7.

٢٩٨. Al-Kafii: 5/12, mlango wa: wojouhul-jihaad.

hawapaswi huyapa umuhimu maumivu na wakasahau sababu ya mauvu hayo, kwani wakifanya hivyo mfano wao utakuwa ni kama kile kinachofanyika katika uwanja wa mieleka ya ng'ombe –kama mwanafikra mmoja alivyoshabihisha[٢٩٩] – kwamba ng'ombe alikasirika yeye huwa hima yake, mbio zake, hasira zake na nguvu zake anavielekeza kwenye kitambaa chekundu anamsahau mpinzani wake halisi ambaye ndio kabeba kitambaa hicho, na hivyo kumpa fursa adui yake kuzanisha visu shingoni mwake na husababisha kufa hali ya kuwa amemsahau hadi anakufa na kutoweka. Hali yetu isije ikwa kama ya yule ng'ombe! Na hapo utaona kuwa umma huwa unakaukaribia kumshinda adui yake kila unavyokaribia kuishinda nafsi yake, na kwa kadri unavyorudi na kurejea kwa Mwenyezi Mungu aliyetukuka.

FAIDA YA VISA KUJIKARIRI NDANI YA QUR'ANI

٧. Ni kurudia na kuendeleza dozi ya matibabu na kutokutosheka na dozi moja pindi unaposimamia usahihishaji wa hali mbaya au kuziba mapungufu au kutatua tatizo liliopo katika fikra ya jamii au katika Imani yake au mwenendo wake. Kwa mfano utakuta baadhi ya visa vya mitume vijikariri zaidi ya mara kumi, lakini kila kikielezwa huwa na onjo yake, na athari yake na nafasi yake katika kulifanikisha lengo, na huacha athari tofauti na ile iliyoachwa na kilipotajwa sehemu nyingine na njia nyingine hata kama vyote madhumuni yake ni mamoja.

Tunapozungumzia suala la mwanamke kujishauwa mbele ya mwanamme, na kutojistiri na kujifanya shetani anayezuwia kumkumbuka Mwenyezi Mungu aliyetukuka; ili kimatendo awe mfano uliowazi wa kauli ya Ibilisi:

[لأَقْعُدَنَّ لَهُمْ صِرَاطَكَ الْمُسْتَقِيمَ، ثُمَّ لآتِيَنَّهُم مِّن بَيْنِ أَيْدِيهِمْ وَمِنْ خَلْفِهِمْ وَعَنْ أَيْمَانِهِمْ وَعَن شَمَآئِلِهِمْ وَلاَ تَجِدُ أَكْثَرَهُمْ شَاكِرِينَ]

"Basi nitawavizia katika Njia yako Iliyo Nyooka. Kisha nitawazukia mbele yao na nyuma yao na kuliani kwao na kushotoni kwao. Wala hutawakuta wengi wao wenye shukrani"[٢٠٠] , na hawa wanawake wahuni hutumïia njia mbali za kuwapotosha wanaume na kuwadumbukiza katika maasi, kuanzia kujishauwa

---

٢٩٩. Naye ni sheikh Jawdah Sai'd.

٢٠٠. Surat Al-A'araaf: 16-17.

wawapo barabarani, kuja kujipamba wawapo vyuoni na kuonyesha viungo vya miili yao, na michezo na kwenye maonyesho ya kisanaa wakiwa watupu.

Hivyo tukitaka kuyakabili maradhi haya yenye kuangamiza katika jamii, tunaweza kuyatibu kwa kutumia vitabu vituatavyo: kitabu kuhusu hali za kijamii zilipotoka[٢٣] , kitabu kuhusu masuala ya mwanamkē[٢٤] , kitabu kinachohusu athari za michezo na Sanaa katika kubomoa maadili ya jamii, kitabu kuhusu matatizo ya wanafunzi wa vyuo vikuu, wasiwasi zao na matamanio yao[٢٥] , na kitabu kingine chenye maudhui hayo hayo kuhusu vijana[٢٦] na kitabu kinachohusu fikihi ya familia kinachozungumzia mahusiano ya kifamilia na kijamii kwa mujibu wa mafunzo ya sheria na vitabu vingineyo[٢٧] , kwani tatizo hili ni hatari na linaingia kwenye Nyanja zote zilizotajwa, na kulisoma katika Nyanja zake zote kunatoa tija tofauti na ile ambayo ingepatikana kwa kulidurusu katika uuga mmoja, na si haba kuwa vitabu hivi vinaongeza idadi ya hadhira inaowazungumzisha, na hatimaye tija inakamilika kwa kulisoma tatizo katika pande zake zote[٢٨] .

8. Kutumia njia tofauti katika kuwaongoza wanadamu. Kwa kuwa mwanadamu na aina tatu za ulimwengu ambazo ni: nafsi, akili na moyo, utaiona Qur'ani imeviandaa vyote ili kumuwezesha mwanadamu kumtii Mwenyezi Mungu aliyetukuka. Haya nimeyafafanua katika masomo kwa anuwani (Hebu turudi kwenye Qur'ani[٢٩]).

Utaikuta mara nyingi ikizungumzisha maumbile na kuyaamsha, kwani Qur'ani katika baadhi ya hadithi imeelezea sababu ya kuteremka kwake kwamba: (Ili iyaamshe maumbile yao yaliyojificha), kwa sababu maumbile ni dalili iliyozawi na yenye kusema kweli zaidi, kiasi kwamba hakuna mtu anayeweza kuyajadili.

---

٢٣. Kitabu a'n Ad-Dawahiril Al-Ijtimaai'yah Al-Munfarifah.

٢٤. Kitabu a'n Qadhaayal- Al-Mar'ah.

٢٥. Kitabu a'n Mashakil Al-Jaamia't, Humuumuhum wa Tat'wallua'tuhum.

٢٦. Kitabu a,n Ash-Shabaab.

٢٧. Fiqihul Usrah.

٢٨. Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu, kumetolewa vijitabu na majarida ambavyo vinazungumzia hizi nyanja zote.

٢٩. Falnarji'i Ilal Qur'ani.

Msikilize Mwenyezi Mungu anavyoongea na maumbile katika kuthibitisha uwepo wa Muumba:

[أَفَرَأَيْتُم مَّا تُمْنُونَ، أَأَنتُمْ تَخْلُقُونَهُ أَمْ نَحْنُ الْخَالِقُونَ]،[أَفَرَأَيْتُم مَّا تَحْرُثُونَ، أَأَنتُمْ تَزْرَعُونَهُ أَمْ نَحْنُ الزَّارِعُونَ]،[أَفَرَأَيْتُمُ الْمَاء الَّذِي تَشْرَبُونَ، أَأَنتُمْ أَنزَلْتُمُوهُ مِنَ الْمُزْنِ أَمْ نَحْنُ الْمُنزِلُونَ]،[أَفَرَأَيْتُمُ النَّارَ الَّتِي تُورُونَ، أَأَنتُمْ أَنشَأْتُمْ شَجَرَتَهَا أَمْ نَحْنُ الْمُنشِؤُونَ]

(Je, Mnaiona mbegu ya uzazi mnayo idondokeza? Je, mnaiumba nyinyi, au ni Sisi ndio Waumbaji? Je, mnaona makulima mnayo yapanda? Je, Ni nyinyi mnayo yaotesha au ni Sisi ndio wenye kuotesha? Je, mnayaona maji mnayo yanywa? Je, ni nyinyi mnayo yateremsha kutoka mawinguni au ni Sisi ndio wenye kuyateremsha? Je, mnauona moto mnao uwasha? Ni nyinyi mlio uumba mti wake au Sisi ndio Waumbaji?[٢٦]) na semehu nyingine Mwenyezi Mungu anasema hali yakuwa akimkemea mwanadamu muasi: ٨

[هَلْ جَزَاء الإِحْسَانِ إِلا الإِحْسَانُ]

(Hakuna malipo ya ihsani isipokuwa ihsani[٢٧]), bila shaka nawe unaogelea katika neema za Mwenyezi Mungu aliyetukuka: ٦

[وَإِن تَعُدُّواْ نِعْمَتَ اللهِ لاَ تُحْصُوهَا]

(Na mkizihesabu neema za Mwenyezi Mungu hamuwezi kuzidhibiti)[٢٨] .

NI VIPI TUTARUDI KUIHUISHA NAFASI YA QUR'ANI?

Nirudi kwenye swali nililouliza kwamba ni vipi tutaweza kuirudisha Qur'ani kwenye maisha na na vipi tunaweza kufaidika nayo? Hakika makundi mawili ndio wanaobeba jukumu hilo: kundi la kwanza ni jamii, na kundi la pili ni hauza (vyuo vya dini) ambayo ndio alama ya ufahamu na uelewa wa Umma, ndio fikra yake na kiwango chake cha kidini. Hapo nyuma tulisema kwamba wadhifa mkubwa unaosimamiwa na Hauza katika jamii ni kuipa mafunzo ya Qur'ani, mitazamo na miono yake, maadili na Imani yake, mambo ambayo tumeashiria baadhi yake huko nyuma, kwa ufahamu sahihi na safi kama itakavyo Qur'ani, na kwa mfumo unaoendana na nafasi yake kuwa huwa hai katika maisha ya Umma, na hili kutimia

[٢٦] Surat Al-Waaqia'h: 58-72.

[٢٧] Surat Ar-Rahman: 60.

[٢٨] Surat Ibrahim: 18.

kwa njia mbalimbali kama vile: mimbari za Imamu Hussain (a.s), mihadhara, mukutano, khutba za sala ya Ijumaa na Jamaa, vitabu, majarida na mfano wa hivyo.

Isipokuwa kabla ya hayo ni lazima kuirudisha Qur'ani kwenye mitaala ya masomo kihauza, na hili litatimia kwa namna mbili:

Yakwanza: kuirudisha kwenye masomo ya awali, yaani masomo ya kiwango cha Muqadimati na Sutuhu, ambapo katika hatua hizi inabidi watoe mitaala ijayo[٢] :

١. Kuhifadhi, kusoma Qur'ani Tukufu na kuidhibiti kwa shakli kwa mujibu wa kanuni za lugha ya Kiarabu, na kuzisoma kwa umadhbuti kanuni za Tajuwidi zilizo ndani ya sheria.
٢. Tafsiri kwa ufupi ya maneno, walau kwa mfumo wa kufafanua maana za misamiati kama ilivyo katika Tafsiri ya Shibr na mfano wake, ile mwanafunzi apate fikra za ujumla kuhusu maana za Qur'ani.
٣. Kusoma Uloomul Qur'an, na kitabu bora katika hili ni (Al-Bayaan) au (Muqaddamatu Kitabil A'laaur Rahman kilichochapishwa mwanzoni mwa Tafsir Shibr.
٤. Kufanya mashindano katika elimu mbalimbali zinazohusu Qur'ani na kuandaa zawadi kwa ajili ya washindi na waliowapita wengine.

Yapili: Masomo ya juu, na hili hutimia katika hatua zifuatazo:

١. Kufungua malango wa kubobea katika masomo ya Qur'ani, na mda muwafaka zaidi wa hilo ni baada ya kukamilisha masomo ya levo ya juu (As-Sutuhul Ulyah) kiasi kwamba mwanafunzi anayebobea huandaliwa mtaala maalumu kwa ajili yake, na inawezekana kunufaika na baadhi ya vitabu vilivyopo baada ya kufanyiwa mtihani maalumu ili kubaini uwezo wa mwanafunzi anayetaka kubobea katika sehemu hii na kutumia muda wake mwingi kwa ajili masmo haya ikiwa ni pamoja kukusanya vyanzo zinavyohusiana na taaluma ile, ili mwanafunzi huyo aje kuwa mwalimu, au mfasiri au mtafiti wa masuala ya Qur'ani.
٢. Kusoma tafsiri ya Qur'ani kwa kina, ima Qur'ani yote au baadhi ya aya na baadi ya sehemu zilizochaguliwa kwa lengo maalumu, inaweza kuchaguliwa tafsiri moja ikawa kama kitabu cha kusomea, kiasi kwamba mkufunzi hukisherehesha, hutoa maoni yake, huongeza maarifa yanayofaa kutoka

[٢] Mheshimiwa sheikh ameyaingiza masomo haya katika mitaala ya masomo ya Chuo Kikuu cha kidini cha Sadr anachokisimamia.

kwenye vitabu vingine vya tafsiri na kutoka kwenye vyanzo vinginevyo, na kwa mtazamo wangu mvinyu naona kuwa vyanzo hivi viwili ni bora zaidi, ambavyo ni: Al-Miizan na Fii Dhilaalil Qur'an, kwa sababu kila kimojawapo kila mlengo wake maalumu katika tafsiri unaotofautiana na mlengo wa kingine, milengo ambayo haifahamu isipokuwa yule aliyevisoma vitabu hivyo.

٣. Kuwekwe mitaala ya masomo ya maarifa ya Qur'ani, miono na mitazamo ya Qur'ani, tafiti na falsafa ya Qur'ani juu ya uwepo na maisha, baada ya mwanafunzi kujifunza tafsiri kwa ufupi ya maneno ya Qur'ani na kuyasoma hapo kabla. Na yote haya hupatikana kwa kuzidurusu aya za Qur'ani kimaudhui na si kwa njia ya kusoma ya aya mojo kama ilivyozoeleka, hata kama kufanya hivyo ndio msingi wa hayo. Katika kitabu changu nilichokiita (Madkhal Ilaa Tafsiiril Qur'an) ambacho ni kitabu cha kinafaa kuwa utangulizi wa maudhui hii, nilijaribu kuilinganisha mifumo hii hii miwili.

Katika mitaala inabidi kuzingatiwe zile maudhui za kielemu, yaani zile ambazo zina uhalizi katika maisha, sawasawa kwa upande wa Imani, au maadili au fikra. Kwa mfano ikawa na maudhui kama vile: Taquwa (Uchamungu), subira, fiqihi, tauhidi, uimamu, utawala (wilayah), shetani, siku ya marejeo, jamii ya kiislamu, mambi yanayoijenga nay ale yanayoibomoa, matarajio na matumaini, mawaidha na mazingatio, suna na kanuni za Mwenyezi Mungu kwa umati na jamii, na kuendelea, wakati huo bila shaka fikra zetu nyingi zitabadilika, kwa sababu maana za maneno ya Qur'ani zilizo zoweleka leo hii haziendani ufahamu zahihi wa Qur'ani kwa mujibu wa uchunguzi uliofanywa kwenye Qura'ni, na sababu yake ni mrundikano wa vumbi la taawili na kutafsiri Qur'ani kwa rai binafsi, kuyafadhilisha matamanio na kufuata chuki, lakini pia mashambulizi ya maadui wa Qur'ani na sababu nyinginezo nyingi.

FIQIHI NA FAQIHI KATIKA MSAMIATI WA QUR'ANI

Huko nyuma tumezungumzia maana ya Ujahilia katika msamiati wa Qur'ani, tukaelezea sifa za jamii ya kijahilia na njia mbadala za Mungu zilizotolewa na Qur'ani. Na huu ulikuwa ni kama mfano wa maana ya kijamii.

Na sasa nitatoa maana ya Qur'ani ya neno na msamiati wa hauza ambao ni (Fiqihi) ili uwe ni mfano mwingine. Neno Fiqihi limezoeleka kwetu (wanahauza)

kuwa ni elimu ya hukumu za kisheria, wakati masamiti huu wa kiqur'ani ndani ya Qur'ani hutambulika kwa maana ya kumtambua Mwenyezi Mungu aliyetukuka. Na uhusiani uliopo baina ya maana hizo mbili upo wazi, kwamba zinakutana sehemu na sehemu nyingune hazikutani.

Kwa mfano katika aya hii:

[فَلَوْلاَ نَفَرَ مِن كُلِّ فِرْقَةٍ مِّنْهُمْ طَآئِفَةٌ لِّيَتَفَقَّهُواْ فِي الدِّينِ وَلِيُنذِرُواْ قَوْمَهُمْ إِذا رَجَعُواْ إِلَيْهِمْ لَعَلَّهُمْ يَحْذَرُونَ]

(… lakini kwa nini halitoki kundi katika kila taifa miongoni mwao kujielimisha vema dini na kuwaonya watu wao watakapowarudia,ili wapate kujihadhari?[٢٧٢]), sote tunajua kuwa tahadhari na uchamungu havitokani na kuzifahamu hukumu za kisheria, bali chanzo cha tahadhari ni cha kiroho, kinafsi na kiakili kisha ndio hupatikana uchamungu na maarifa moyoni, ambayo ndio humsukuma mtu kwenye kujifunza hukumu za kisheria na kuzifanyia kazi, mwenye unaweza kulijaribu hilo, soma vitabu vya fiqih na uzame ndani yake kuanzia mwanzo hadi mwisho, je utaviona vikiushibisha moyo moyo wako chochote au kukuongezea kuchukua tahadhari na uchamugu? Tumeona mafakihi wangapi waliofahamu maana ya fikihi kwa maana ya kwanza, lakini wamejishughulisha na dunia na wamejitenga mbali kweli na Mwenyezi Mungu?

Qur'ani inatusimulia mfano wa faqihi huyu ikisema:

[وَاتْلُ عَلَيْهِمْ نَبَأَ الَّذِيَ آتَيْنَاهُ آيَاتِنَا فَانسَلَخَ مِنْهَا فَأَتْبَعَهُ الشَّيْطَانُ فَكَانَ مِنَ الْغَاوِينَ، وَلَوْ شِئْنَا لَرَفَعْنَاهُ بِهَا وَلَكِنَّهُ أَخْلَدَ إِلَى الأَرْضِ وَاتَّبَعَ هَوَاهُ فَمَثَلُهُ كَمَثَلِ الْكَلْبِ إِن تَحْمِلْ عَلَيْهِ يَلْهَثْ أَوْ تَتْرُكْهُ يَلْهَث ذَّلِكَ مَثَلُ الْقَوْمِ الَّذِينَ كَذَّبُواْ بِآيَاتِنَا فَاقْصُصِ الْقَصَصَ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ]

(Na wasome khabari za yule tuliyempa aya zetu, kisha akajivua nazo, na shetani akamfuata na akawa miongoni mwa waliopotea. Na kama tungelitaka tungelimuinua kwazo, lakini yeye akagandamana kwenye ardhi na akafuata matamanio yake. Basi hali yake ni kama hali ya mbwa, ukimpigia kelele anahema au ukimwacha (pia) anahema. Hivyo ndivyo hali ya watu waliokadhibisha Aya zetu, basi simulia hadithi huwenda wakafikiri)[٢٧٣] .[٧]

[٢٧٢] Surat At-Tawbah: 122.

[٢٧٣] Surat Al-Aa'raaf: 175-176.

Na miongoni mwa dalili kwamba maana ya Fiqihi ni kumtambua Mwenyezi Mungu, ni kwamba katika aya tkufu, ameifanya mahala pake kuwa ni moyo ambao ndio sehemu ya maarifa ya kweli ya Mwenyezi Mungu, wakati hukumu za kisheria sehemu yake ni akili, anasema Mwenyezi Mungu aliyetukuka:

[رَضُواْ بِأَن يَكُونُواْ مَعَ الْخَوَالِفِ وَطُبِعَ عَلَى قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لاَ يَفْقَهُونَ]

(Wameridhia kuwa pamoja wanaobakia nyuma, nan yoyo zao zikapigwa muhuri, kwa hiyo hawafahamu)[٢٧٤] , na

[لَهُمْ قُلُوبٌ لاَّ يَفْقَهُونَ بِهَا]

(Nyoyo wanazo lakini hawafamu kwazo)[٢٧٥] , ndio maana aya ikalifanya neno fiqihi,[٢٧٦] yaana maarifa madhubuti ya Mwenyezi Mungu, na maarifa ya Muumba na siku ya marejio, kuwa ni sababu ya kuongezewa nguvu mara kumi zaidi, pale Mwenyezi Mungu aliposema:

[يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ حَرِّضِ الْمُؤْمِنِينَ عَلَى الْقِتَالِ إِن يَكُن مِّنكُمْ عِشْرُونَ صَابِرُونَ يَغْلِبُواْ مِئَتَيْنِ وَإِن يَكُن مِّنكُم مِّئَةٌ يَغْلِبُواْ أَلْفاً مِّنَ الَّذِينَ كَفَرُواْ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لاَّ يَفْقَهُونَ]

(Ewe Nabii! Wahimie walioamini waende vitani, kama wakiwa miongini mwenu ishirini wanaosubiri, watawashinda mia mbili. Na kama wakiwa mia moja miongoni mwenu watawashinda elfu moja katika waliokufuru, kwa sababu wao ni watu wasiofahamu)[٢٧٧] .

Na hadithi tukufu kutoka kwa bwana mtume (s.a.w.w) anatilia mkazo maana hii, alisema:

(ألا أخبركم بالفقيه حقاً؟ من لم يقنط الناس من رحمة الله ولم يؤمنهم من عذاب الله ولم يؤيسهم من روح الله، ولم يرخص في معاصي الله ولم يترك القرآن رغبة عنه إلى غيره، ألا لا خير في علم ليس فيه تفهم، ألا لا خير في قراءة ليس فيها تدبر، ألا لا خير في عبادة ليس فيها تفقه)

(Je, nikuelezeni faqihi na mwanazuoni wa kweli? Ni yule asiyewakatisha watu tamaa na rehema za Mwenyezi Mungu, na wahaaminishi na adhabu ya Mwenyezi Mungu, na wahakatishi tamaa na faraja ya Mwenyezi Mungu, na haruhusu kumuasi

---

٢٧٤ Surat At-Tawbah: 87.

٢٧٥ Surat Al-Aa'raaf: 179.

٢٧٦ Surat Al-Anfaal: 65.

Mwenyezi Mungu, na hamwachii mwingine Qur'ani kwa kuichukia. Tambueni kuwa hakuna kheri kwenye elimu isiyo na ufahamu ndani yake, tambueni kuwa hakuna kheri katika usomji usio na mazingatio ndani, tambueni kuwa hakuna kheri katika ibada isiyo na uelewa ndani yake)[٢٧٤] , hivi ndivyo ilivyo katika kitabu cha Al-Wasaail.[٢٧٥]

Na hadithi hii ina chanzo kingine[٢٧٦] , kama ifuatavyo:

(فإنه إذا كان يوم القيامة نادى مناد: يا أيها الناس إن أقربكم من الله تعالى مجلساً أشدكم له خوفاً، وإن أحبكم إلى الله أحسنكم عملاً، وإن أعظمكم عند الله نصيباً أعظمكم فيما عنده رغبة، ثم يقول عز وجل: لا أجمع لكم اليوم خزي الدنيا وخزي الآخرة، فيأمر لهم بكراسي فيجلسون عليها، وأقبل عليهم الجبار بوجهه وهو راض عنهم وقد أحسن ثوابهم).

(Kwa hakika itakapokuwa siku ya Kiyama, mnadi atanadi: Enyi watu! Hakika atakayekaa karibu zaidi na Mwenyezi Mungu ni mwenyekumuogopa zaidi, na hakika mpendwa zaidi kwa Mwenyezi Mungu ni mwenyekutenda mema zaidi, na hakika mwenye fungu kubwa kuliko, ni yule utashi zaidi wa kile kilichoko kwake, kisha atasema Mwenyezi Mungu: Sitakupeni fedheha ya dunia wala fedheha ya Akhera, kisha ataamuru wapewe viti na wataketi juu yake, na Mwenyezi Mungu atawaelekea kwa uso wake hali ya kuwa akiwa radhi nao na akiwa amewalipa thawabu iliyo nzuri kuliko).

Utaona kuwa sifa za faqihi ni kila kinachmuweka karibu na Mwenyezi Mungu aliyetukuka, imekuja katika hadithi kutoka kwa Amirul muunina (a.s) kuwa alisema:

(كانت الفقهاء والحكماء إذا كاتب بعضهم بعضاً كتبوا ثلاثاً ليس معهن رابعة: من كانت الآخرة همته كفاه الله همه من الدنيا، ومن أصلح سريرته أصلح الله علانيته، ومن أصلح فيما بينه وبين الله عز وجل أصلح الله فيما بينه وبين الناس)

(Wanazuoni na watu wa hekima walikuwa wanapoandikiana wao kwa wao, huandika mambo matatu, yasiyo na la nne: Yeyote ambaye Akhera itakuwa ndio hima yake, basi Mwenyezi Mungu atamtoshelezea hima yake ya dunia, na yeyote atakayeisuluhisha na kuitakasa siri yake, basi Mwenyezi Mungu ataisulusha dhahiri yake, na mwenyekusuluhisha lile lililopo baina yake na Mwenyezi Mungu aliyetukuka, basi Mwenyezi Mungu atayasuluhisha yaliyo baina yake na watu)[٢٧٧] .

---

٢٧٤. Biharul Anwaar: 2/49, mlango: sifaatul Ulamaa wa Asnaafuhum, hadithi: 8.

٢٧٥. Madinatul Balaaghah: Uk: 98, kutoka kwenye kitbu cha Al-Ja'fariyaat.

٢٧٦. Al-Khisaal: Uk: 129, mlango: 3.

Na katika hadithi ya kutoka kwa Abul Hassan (a.s) alisema:

(من علامات الفقه الحلم والعلم والصمت، إن الصمت باب من أبواب الحكمة وإن الصمت يكسب المحبة وإنه دليل على كل خير)

(Katika alama za fiqihi ni upole, elimu na ukimya, hakika ukimya ni mlango katika milango ya hekima, na hakika ukimya huleta mapenzi na ni kiashiria cha kila kheri)[٢٨] .

Na inawezekana kuipata maana hii pia kwa kukusanya hadithi hizi mbili: katika kitabu cha Al-Khisaal kutoka kwa mtume (s.a.w.w) alisema:

(صنفان من أمتي إذا صلحا صلحت أمتي وإذا فسدا فسدت أمتي: الأمراء والفقهاء)

(Makundi katika Umma wangu wakisalimika, basi Umma wangu utasalimika, na wakiharibika, basi Umma wangi pia utaharibika: watawala na mafaqihi –wanazuoni-)[٢٩] , na katika kitabu cha Wasaail akinukuu kutoka kwenye kitabu cha Al-Amaali, ambapo badala ya wanazuoni ni wasomaji. Tukiiongezea hadithi ijayo katika sifa za wasomaji, tunapata maana iliyotajwa.

Hivyo basi, katika ya Faqihi kwa msamiati wa Qur'ani na Faqihi kwa mujibu wa maana ya kihauza mahusiano yake ni kuwa zinakutana sehemu na kupishana sehemu nyingine, kwa sababu atu anaweza kuwa faqihi kwa mujibu wa maana ya Qur'ani lakini asiwe faqihi kwa mujibu wa maana ya kihauza,kwani wapo mawalii wengi wa Mwenyezi Mungu wenyekumtambua na wenye karama zilizoshuhuduwa licha ya kuwa walikuwa hawakufikia daraja la juu katika elimu za kihauza, na kinyume chake pia, unamkuta mtu akili yake imesheheni nadharia na fikra za Kiululi, kiakili na masilala za kifiqihi kiasi ambacho utamkuta mjuzi wa zile masiala za ndani, lakni moyo wake ukawa haujajengeka na ukumbusho wa Mwenyezi Mungu, kiasi ukimuuliza suala kidogo tu la malezi ya nafsi na mwenendo mwema wa kueleke kwa Mwenyezi Mungu, na kujisataka nafsi na kuutakasa moyo, basi hubaki amedua na akishangaa, mfano wa mtu huyu sio faqihi kwa mujibu wa maana ya Qur'ani ya neno faqih. Na faqihi aliyekamilika ni yule aliyekusanya maana zote mbili, kama ilivyo kwa wanazuoni wetu watukufu, walifikia kiwango cha juu katika Fiqhi na Usoul na wakawa ni vinara wa

---

٢٨ Al-Ikhtisaas: 232.

٢٩ Chanzo chake imekwishatajwa mwanzo wa kitabu hiki.

kumtambua Mwenyezi Mungu, bila shaka hawa ndio wale waliokusudiwa katika hadithi:

المقدسين (الفقهاء أمناء الرسل)

(Wanazuoni ni waminifu wa mitume)[٢] , kwa mtazamo huu wa Qur'ani ٨
ndivyo tunavyopaswa kuzifahamu hadithi pia, ili maana zake za juu zisitupotee.

JUKUMU LA HAUZA KATIKA KUENDESHA HARAKATI ZA QUR'ANI

Na mimi hapa nitataja hadithi moja tu ambayo inabainisha majukumu ya hauza tukufu katika kuiamsha jamii, kuiongoza na kuirekebisha.

Imepokelewa kutoka kwa Mtume Muhammad (saw); 'alihutubia akamuhimidi Mwenyezi Mungu na akamsifu kisha akataja makundi ya Waislamu akawasifia na akasema; kuna nini kwa watu wasiojifunza kutoka kwa majirani wao na hawafahamu wala hawaelimiki? Ninaapa kwa Yule ambaye nafsi yangu iko mikononi mwake, (ni lazima) wawafundishe majirani zao, wawafahamishe, wawaelimishe au (niwaombee dua) niwaharakishiwe adhabu ya duniani, kisha (Mtume) akashuka mimbari na akaingia nyumbani kwake. Masahaba wakajiuliza, Mtume alikusudia nini katika maeneo yake? Wakasema, hatujui alikusudia nini labda aliwakusudia Ashaairah (wafuasi) miongoni mwa wasomi na maulama wao, wenye majirani wajinga na wasio na elimu. Kundi miongoni mwa Ashaairah wakakusanyika wakaingia nyumbani kwa Mtume (saw) wakasema; umeitaja jamii fulani miongoni mwa Waislamu kwa kheri kisha ukatutaja sisi kwa shari, tumefanya nini? Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema; (mnatakiwa) kuwafundisha majirani zenu, muwaelimishe na muwaamrishe (mema) na muwakataze (machafu) au nikuharakishieni adhamu hapa duniani. Wakasema, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu tupatie muda wa mwaka mmoja, katika muda wa mwaka mmoja, tutawaelimisha na kuwafundisha. Mtume akawapa muda wa mwaka mmoja kisha akasoma aya inayosema: (Wamelaaniwa wale waliokufuru miongoni mwa wana wa

[٢] Biharul Anwaar: 2/36, Hadith: 38.

Israel kupitia ulimi wa Nabii Daud na Issa mwana wa Maryam (a.s), hayo ni kwa kuwa waliasi na walikuwa wakikiuka sheria. Walikuwa hawakatazani mabaya waliyoyafanya, kwa hakika walikua wakifanya mabaya.)[٢٨]

Haya ni baadhi ya mapendekezo ambayo nayawasilisha kwa hawza (chuo) tukufu katika uwanja huu na wadhifa shirikishi kwa wote ni kuzingatia kuisoma Qur'ani na kunufaika nayo majira ya usiku na mchana na utapata kufahamu mengi kupitia hadithi tufu inayofuatia. Na wadhifa huu kwa hauza hauwahusu wao pekee, bali tumewahutubu kwa kauli hiyo kutokana udharura wake ulivyo kwao kuliko watu wengine. Lakini jamii yote ina jukumu la kufuata hatua hizi kwa kuzingatia na inavyomfaa kila mtu. (kwa mfano) watu wenye maarifa wataanza kwa kuzo tafsiri nyepesi kama vile tafsiri ya Shobar.

Ninamnasihi kila Mwislamu kwa kuzingatia tajriba (uzoefu) niliyoitumia mimi, aanze maisha yake pamoja na Qur'ani, aisome katika msahafu wa tafsiri kama tulivyoitaja (ya Shobar), ili aweze kuenzi ufahamu wa misamiati ya aya, wakati wa kusema kwake. Na aendelee na hali hiyo kwa mahitimisho kadhaa hadi aweze kumiliki maarifa jumla ya Qur'ani, kisha anarejea tena kwenye nakala ya msahafu akisoma ndani yake; na kujiendeleza kwa kusoma vitabu vya tafsiri kubwa, kama vile tafsiri ya Al-Mizan sambamba na (kusoma) Qur'ani, huku akisoma vitabu ambavyo vimebainisha maana ya Qur'ani au ambavyo vimeifafanua Qur'ani kwa kuzingatia maudhui, ambapo atapata kuchukua mojawapo kuwa ndio anuani ya uchunguzi wake. Baadaye aitafiti Qur'ani kwa kukusanya aya zote zinazohusiana na anuani husika kisha atoe natija kwa majimui ya malengo ya Qur'ani na nadharia zake- Na mimi hapa nitaazima istilahi hizi za kifikra kwa lengo la kuziliwaza nazo akili sambamba na kuzingatia-maudhui hii ambayo inatakiwa kutatuliwe ndani yake matatizo halisi yanayoikabili jamii sawa sawa iwe tatizo ya kiitikadi, kiakhlaqi, kifikra na kadhalika.

---

٢٨ Mizanu fi Tafsiril-Qur'ani juzu ya 6 ukurasa wa 84 katika tafsiri ya aya, kutoka kitabu cha Al-Durrul-Manthur.

Na huwenda ikawa ni bora kulifuatilia hilo pamoja na baadhi ya wasomi wakubwa wa hauza tukufu, ili waweze kuwaelekeza na wajibu maswali yao, na wawaongoze kwenye mambo yenye kuwafaa, kwa kuwa jamii na hauza kila kimoja kinamkamilisha mwingine. Kwani hauza inaielekeza jamii, huku jamii nayo ikiiwekea mashinikizo hauza, ili iwe kwenye kiwango cha kubeba majukumu na kiwango cha hitajio la umma, matumaini na mazingatio ya zama ambazo unaishi ndani yake. Wakati huo itawezekana kuainishwa vipengee vya sifa stahiki za hauza, na isiyo hauza na umma utapata kujua ni upande gani ulio sahihi.

Hakika Qur'ani haiwezi kufahamika uhalisia wa maana yake, hadi pale mwanadamu atakapoichukulia kuwa ni ujumbe ambao anairekebisha nafsi yake, pamoja na watu wanaomzunguka kwa ujumbe huo; na anaweza (kutumia ujumbe huo) kukabiliana na makosa na upotofu unaoikabili jamii ya mwanadamu. Wakati huo ataweza kuishi sawa na mazingira iliyoshuka ndani yake Qur'ani hiyo. Ni hapo ambapo kutafunguliwa milango ya siri zake na haitotosha kuisoma tu au kupata baraka zake, ingawa hayo yana fadhila isiyopingika. Ni suala la dharura (lazima) tutupie macho, moja ya masomo ya Qur'ani kwa mujibu wa historia ya kushuka aya zake, kwa kudondoa baadhi ya nukta zake, ambapo tutapata kunufaika na bahthi (tafiti) zilizo na faida nyingi katika uga wa maarifa ya hatua za Qur'ani katika kurekebisha jamii. Kwa kuzingatia kuwa ilishuka taratibu kwa mujibu wa matukio.

Hakika ushukaji huu wa taratibu wa Qur'ani uliojiri mbadala wa kushuka mara moja tu, una nafasi yake ya moja kwa moja na taathira tendaji kwenye mazingira iliyoyatatua, kuhusiana na hilo Mwenyezi Mungu anasema: "Na Qur'ani tumeigawanya sehemu mbalimbali ili uwasomee watu kwa kituo, na tumeiteremsha kidogokidogo." Surat Isra aya ya 106. Na kwa kuwa Qur'ani ni kitabu cha malezi, uongofu na kuhuisha mioyo, hakuna budi ila iteremke taratibu na kwa upole. Izungumzie ponyo inayofaa katika muda mwafaka na kwa uthubutu mwafaka usiopungua au usiozidi, si kabla ya wakati au baada yake. Hivyo ndivyo Qur'ani ilivyoendana na umma huu kwa upole ambapo ghafla ulijikuta (umma) baada ya vipindi virefu vya muda mrefu kwenye kilele cha ubora, ukamilifu, utukufu, izza na nguvu.

BAADHI YA DESTURI NA SUNA ZINAZOHUSIANA NA USOMAJI WA QUR'ANI

Ninapenda hapa nitaje baadhi ya desturi, mienendo na suna zinazohusiana na usomaji wa Qur'ani kwa kutegemea riwaya tukufu:

1-Ni suna kuhitimisha Qur'ani mara moja kwa kila mwezi na isizidi miezi minne. Yaani kwamba ahitimishe kwa mwaka mmoja mara tatu, isipokuwa ziada ambazo zinatakiwa kuzidisha ndani ya mwezi mtukufu wa Ramadhani.

2-Usomaji uwe kwa namna ya uhitimishaji. Yaani kwamba aanze mwanzo wa Qur'ani hadi mwisho wake, na sio usomaji wa sura tofauti hata kama iwe ni kwa kuzingatia umuhimu wake. Bali apitie Qur'ani yote ili aweze kupata baraka zote kama ilivyoelezewa katika hadithi tukufu inayofuata ya: (Muhitimishaji muanzishaji …)[٢٨]

3-Uhitimishaji usadifiane na siku ya Ijumaa na asome wakati wa kuhitimisha Qura'n dua yake maalumu nayo ipo kwenye kitabu cha Al-Sahifatus-Sajjadiyah.

4-Wakati wa kuhitimisha Qur'ani asisimame mwishoni pake, bali aiunganishe moja kwa moja kwa ufunguo wa hitimisho lake mpya angalau aanze kwa surat Al-Fatiha na mwanzo wa aya tano wa surat Al-Baqarah.

5-Awe katika hali ya tohara (usafi wa kimaanawi) na akalie msala huku akiwa ameelekea kibla.

6- Imepokelewa kuhusiana na kauli yake Mwenyezi Mungu inayosema: "Enyi mlioamini! Subirini na shindaneni kusubiri na kuweni makini na mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kufanikiwa." Surat Aal Imran aya ya 200, kwamba miongoni mwa watu walio makini, wapo wanaotulia kwenye eneo lao la kusalia wakisubiria kutimia muda wa swala ya faradhi. Hivyo kupata fadhila za umakinifu ni muumini kupitiwa na hali hiyo, nacho ni kipindi cha kusubiria (kutimia) muda

[٢٨] Usuulul-Kaafi Juzu ya pili ukurasa wa 605.

wa swala kwa kusoma Qur'ani, na malipo yake yanakuwa makubwa zadi iwapo jambo hilo litafanyika msikitini akisubiria swala ya jamaa.

7- Na imepokewa suna ya kulala ya tohara (usafi wa kimaanawi) na kusoma Qur'ani kabla ya muumini hajalala kwenye kitanda, kuhusiana na suala hilo imepokewa hadithi inayosema: "Atakayepatwa na hali ya kutokwa na udhu na akawa hakutawadha basi amenifanyia tabia mbaya. Na atakayetawadha na akawa hakusali rakaa mbili, atakuwa amenifanyia tabia mbaya na atakayesali rakaa mbili na akawa hajanisalimia, atakuwa amenifanyia tabia mbaya, na atakayenisalimia na kikakosa kumjibu, nitakuwa nimemtendea tabia mbaya na mimi si mlezi wa tabia mbaya.[٢] " Na ikiongezewa juu yake suna yenye nguvu kwenye sala ya usiku, suna kujisaidia kabla ya kulala na suna ya kupiga mswaki, tutatoka na majimui ya muhimu nayo ni kwamba kabla ya muumini hajalala kwenye kitanda chake hujisaidia, kupiga (meno) mswaki kisha anatawadha na kusali swala ya usiku, yote au baadhi yake na atekeleze nyingine kabla ya kuchomoza alfajiri. Baadaye atasoma kiasi kidogo cha Qur'ani Tukufu na amuombe Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kisomo hicho (kwa ajili yake) na kwa waumini, hapo atakuwa amekusanya suna zote hizo. Ama mtu ambaye anakesha usiku akiangalia vipindi na filamu chafu ambazo zinachosha mishipa yake na kumtwisha mzigo, ataishi katika maisha magumu nay a tabu.

8-Kwa wale wanaoanza usomaji wa Qur'ani uwe kwa tafsiri ya Shobar ambayo inajumuisha faida nyingi. Kwa kuwa kuna nakala ya msahafu mtukufu na ndani yake kuna tafsiri jumla ya maala ya Qur'ani, na hayo ndio tuliyasema kwamba imejumuisha mfumo wa masomo ya awali ya Qur'ani, kama ambavyo ndani yake kuna utangulizi wa elimu za Qur'ani nalo ni somo lingine. Na humo kuna mwambata wa orodha ya matamshi ya Qur'ani kiasi kwamba kila aya utakayotaka kufahamu eneo lake, hupatikana kwa namna hiyo na eneo la neno lolote kutoka humo. Na ndani yake kuna visomo mbalimbali vya maneno ya umoja iwapo yatapatikana katika faharasi yake. Na humo kuna utaratibu wa kushuka sura , katika

[٢] Wasaailush-Shia, Kitabu Al-Twaharah, Abwaabut-Twaharah, babu 11 hadithi ya 2.

anuani ya kila sura inasema kuwa ilishuka baada ya sura fulani. Faida zote hizo zinapatikana katika kitabu hicho cha kuvutia.

9-Aanze kwa kutoa zadi ya hitimisho kwa kuanzia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), pili kwa Amirul-Mu'minina Ali (a.s) aendelee hivyo hadi kwa maasumina wote 14 (a.s), kwani imepokewa riwaya tukufu kuhusiana na suala hiyo kwa kuwa watukufu hao kuliko viumbe watajibu zawadi (hiyo) kwa namna inayoendana na utukufu wao siku ya Kiama.

10-Kuinua sauti kwa Qur'ani wakati wa kusoma na awe ni mwenye huzuni na azingatie maana yake na isiwe huzuni ya mmoja wenu mwishoni mwa sura kama ilivyopokelewa katika hadithi.

11-Ni suna kusoma kwenye msahafu hata kama atakuwa amehifadhi yale anayoyasoma. Na ni suna kila mtu miongoni mwa watu wa familia awe na nakala yake maalumu ya msahafu mtukufu atakuwa akiweka ndani yake alama.

12-Kunyamanza kwa ajili ya Qur'ani, kwani kuzingatia yale anayoyasikia miongoni mwa aya ni fursa bora inayotolewa kwa ajili ya kuisikiliza. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atupe maisha kwa uhai wa Qur'ani na atupe shafaa yake (uombezi) na atujaalie kuwa miongoni mwa watu wanaoongoka kwa uongozi wake (Qur'ani) na kupata mwanga kwa nuru ya elimu yake. Hakika yeye ni Kiongozi wa neema naye ni mpole kwa waja wake na kwa upole wake ametuongoza kwenye dini yake iliyonyoka na atufunike kwa kitabu chake kitukufu na Mtume wake mtakatifu na watu wa nyumba ya Mtume wake watoharifu.

(Nina Mshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuongoza kwa haya, na hatukuwa ni wenye kuongoka lau kama si Mwenyezi Mungu kutuongoza.)

Muhammad Ya'qoobi

Muharram 1422 Hijiria.

HADITHI ARUBAINI KATIKA FADHILA YA QUR'ANI NA ATHARI NA DESTURI ZA KUISOMA

Na nitatosheka hapa na kutaja nasi (mapokezi) za hadithi sambamba na kuweka anuani inayohusiana na maudhui husika. Na pia kubainisha hadithi kwa mujibu wa malengo yake. Hata hivyo ufafanuzi wake na kubainisha nukta zilizomo, ni suala linaweza kutengewa eneo jingine. Na sitoweka ukomo wa idadi 40, kwa kuwa mapokezi ambayo yamehimiza juu ya kuzingatiwa hadithi 40 hatuyafahamu juu yake iwapo yanahusu sharti na si kuhusiana na ziada, hivyo ziada itakuwa kheri.

1–Ulazima wa kujifundisha (Qur'ani).

Imepokelewa kutoka kwa Abu Abdillah (a.s) amesema: "Inatakiwa kwa muumini asife hadi akiwa amejifundisha Qur'ani au awe katika kujifundisha.[٢] " Na imepokewa kutoka kwa Mtume wa Allah (saw) akisema: "Mwenyezi Mungu hatouadhibu moyo ulioifahamu Qur'ani.[٢] " [٨]

Na kutoka kwa Mtume wa Allah amesema: "Mtu bora kwenu ni atakayejifundisha Qur'ani na akaifundisha.[٢] " Na imepokewa kutoka kwa Mtume [٨] wa Allah (saw) akisema: "Wabebaji wa Qur'ani (vifuani) duniani, wanawafahamu watu wa peponi siku ya Kiama.[٢] " [٨]

Na kutoka kwake (saw) amesema: "Qur'ani ni utajiri ambao hakuna utajiri zaidi yake na hakuna umasikini baada yake.[٢] " Na pia kutoka kwa Mtume wa [٩] Allah (saw) amesema: "Mwalimu anapomwambia mtoto, Kwa Jina la Mwenyezi

---

[٢٨٦] Wasaailush-Shia, Kiatabu Al-Swalat Abewaabu Qira'atul-Qur'ani walaw fi ghairi al-Swalat. Mlango wa 1, hadithi ya 4,5,6,15,11,16 kwa Utaratibu.

[٢٨٧] Wasaailush-Shia, Kiatabu Al-Swalat Abewaabu Qira'atul-Qur'ani walaw fi ghairi al-Swalat. Mlango wa 1, hadithi ya 4,5,6,15,11,16 kwa Utaratibu.

[٢٨٨] Wasaailush-Shia, Kiatabu Al-Swalat Abewaabu Qira'atul-Qur'ani walaw fi ghairi al-Swalat. Mlango wa 1, hadithi ya 4,5,6,15,11,16 kwa Utaratibu.

[٢٨٩] Wasaailush-Shia, Kiatabu Al-Swalat Abewaabu Qira'atul-Qur'ani walaw fi ghairi al-Swalat. Mlango wa 1, hadithi ya 4,5,6,15,11,16 kwa Utaratibu.

Mungu Mwenye Kurehemu, Mwingi wa Rehma, (kisha) mtoto akasema, Kwa Jina la Mwenyezi Mungu Mwenye Kurehemu, Mwingi wa Rehma, Mwenyezi Mungu huandika kumuepusha na (moto) mtoto, na kuwaepusha na (moto) wazazi wake, na kumuepusha na (moto) mwalimu.[٢] ”

Na kutoka kwa Abu Abdillah (a.s) amesema: “Mtu mwenye kuhifadhi Qur’ani, anayeifanyia kazi watakuwa pamoja na watukufu wema”.[٢]

2–Kujifundisha Qur’ani ni neema kubwa.

Imepokewa kutoka kwa Mtume (saw) akisema: “Atakayesoma Qur’ani akadhani kwamba kuna mtu aliyepewa jambo bora kuliko yeye, atakuwa amedharau kile alichokitukuza Mwenyezi Mungu, na kutukuza kile alichokidharau Mwenyezi Mungu.[٢] ”

3–Qur’ani ni muombezi, shifaa na mtetezi mkweli

Imepokewa kutoka kwa Mtume (saw), akisema kwenye hadithi kwamba: “Mtakapopatwa na fitina kama kipande cha usiku wenye giza, basi shikamaneni na Qur’ani, kwani yenyewe ni muombezi, shifaa na mtetezi mkweli. Atakayeitanguliza itamuongoza peponi, na atakayeiweka nyuma, itamuongoza motoni, nayo ni muongozaji kwenye njia ya heri. Nacho ni kitabu chenye ufafanuzi na ubainifu ndani yake”, pia akasema: “hayahesabiki maajabu yake na haufichuki ugeni wake. Ni taa za wongofu na mwanga wa hekima”.[٢]

4–Sifa ya msomaji wa Qur’ani

Imepokewa kutoka kwa Abu Abdillah (a.s) akisema: “Inatakiwa kwa anayesoma Qur’ani wakati anapopita kwenye aya ndani ya Qur’ani

---

[٢٩١] Wasaailush-Shia, Kiatabu Al-Swalat Abewaabu Qira’atul-Qur’ani walaw fi ghairi al-Swalat. Mlango wa 1, hadithi ya 4,5,6,15,11,16 kwa Utaratibu.

[٢٩٢] Ushahidi uliotangulia.

[٢٩٣] Ushahidi uliotangulia.

[٢٩٤] Ushahidi uliotangulia, kwenye hadithi ya 2,3,6 kwa utaratibu.

inayozungumzia suala la hofu, amuomabe kwayo Mwenyezi Mungu heri anayoitarajia na amuombe kuepushwa na moto na adhabu".[٢]

Na kutoka kwa Mtume wa Allah (saw) amesema: "Ninashangaa ni kwa nini siwi mzee wakati ninaposoma Qur'ani.[٢] " Na katika hotuba ya Amirul-Muuminna Ali (a.s) kwenye kuwataja wachamungu alisema: "Ama usiku wameweka safu kwa miguu yao wakisoma juzu za Kitabu, wanasoma taratibu, wanazihuisha nafsi zao kwa hicho kitabu, na wanaibua (kwa kitabu hicho) hamasa ya huzuni wakilia kwa dhambi zao kwa uchungu mithili ya maumivu ya jeraha zao. Wanapopita kwenye aya ambayo inatia hofu, wanaielekezea masikio, mioyo na macho yao, pia ikasisimka kwayo ngozi zao, na mioyo yao ikaogopa, mithili ya ukelele wa Jehannam na mipapatiko na mikoromo yake kwenye masikio yao. Na wanapopita kwenye aya yenye kuvutia, huitegemea kwa tamaa na kufungamana nafsi zao kwa mvuto".[٢]

5-Wajibu wa kuwakirimu wabeba Qur'ani na uharamu wa kuwadharau

Imepokewa kutoka kwa Mtume (saw) akisema: "Hakika watu wa Qur'ani wako kwenye daraja ya juu kati ya wanadamu ispokuwa Manabii na Mitume. Msipuuze haki za watu wa Qur'ani kwani wana nafasi mbele ya Mwenyezi Mungu Mukufu Mtenza nguvu.[٢] "

6-Thawabu za yule inayemuwea vigumu kujifunza Qur'ani na kuihifadhi

Imepokewa kutoka kwa Imam Swadiq (a.s) akisema: "Yule ambaye Qur'ani itamuwea ngumu, atakuwa na malipo ya aina mbili na yule ambaye itamuwea nyepesi, atakuwa pamoja na mwanzo.[٢] " Na kutoka kwake (Imam Swadiq-A.S) pia amesema: "Hakika yule anayeweza (kuisoma) Qur'ani na anaihifadhi kwa

---

[٢٩٥] Ushahidi yliotangulia, kwenye mlango wa 5 hadithi ya 3.

[٢٩٦] Ushahidi uliotangulia, hadithi ya 2.

[٢٩٧] Ushahidi uliotangulia, hadithi ya 6.

[٢٩٨] Ushahidi uliotangua mlango wa 4 hadithi ya 1.

[٢٩٩] Ushahidi uliotangulia mlango wa 5 hadithi ya 3.

matatizo kutoka kwake na kutokana na uwezo mdogo wa kuhifadhi, atakuwa na malipo ya aina mbili[٣] ".

7–Wajibu wa kusoma Bismillah kabla ya kila sura

Imepokewa kutoka kwa Imam Swadiq (a.s) akisema: "Wakati mtu anapowasalisha watu, huja shetani kwa shetani (mkuu) ambaye huwa karibu na imam na kusema, je amemtaja Mwenyezi Mungu? Yaani amesoma, 'Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema mwenye kurehemu' ikiwa atasema ndio, basi hukimbia. Na akisema, hapana basi hupanda shingo ya imamu na kunyoosha miguu yake kwenye kifua cha (Imamu). Basi shetani ataendelea kubakia mbele ya watu hadi watakapomaliza swala yao".[٣]

8–Suna ya kusoma Qur'ani wakati wa kutembelea makaburi

Katika kitabu cha (Man laa Yahdhurul-Faqih) imepokewa hadithi kutoka kwa Imam Ridha (a.s) akisema: "Hakuna mja muumini atatembelea kaburi la muumini akasoma kwenye kaburi (surat) Qadr mara 7, ispokuwa Mwenyezi Mungu atamsamehe (yeye) na yule aliye ndani ya kaburi".[٣]

Na katika riwaya nyingine inasema: "Atapata amani kutokana na hofu kubwa." Na katika maana hiyo kuna riwaya nyingi. na sehemu nyingine inazungumzia suala la sunna ya kuzidisha Surat Al-Faatiha, Muawwadhataini, Tauhidi na Ayat Kurusiyyu kila moja mara tatu. Na imepokewa kuhusu thawabu zake kwamba: "Hakika Mwenyezi Mungu, humtumia malaika anayemwabudu Allah kwenye kaburi yake, na kumuandikia yeye (msomaji) na maiti thawabu zinazotokana na ibada ya yule malaika. Na Mwenyezi Mungu atakapomfufua kutoka katika kaburi yake hatokumbwa na hofu ispokuwa Mwenyezi Mungu atamuepusha nayo

---

[٣١] Ushahidi uliotangulia, hadithi ya 2.

[٣٢] Bihaarul-Anwaar 82/20.

[٣٣] Wasaailush-Shia, Kitabu al-Twaharah, Abewaabu Swalaatil-Janaazah, mlango wa 57, hadithi ya 5.

kutokana na (ibada za) yule malaika aliyewakilishwa, hadi atakapomuingiza peponi". [٣]

9–Fadhila za kujifundisha Qur'ani katika rika la ujana na athari zake

Kutoka kwa Imam Swadiq (a.s) amesema: "Atakayesoma Qur'ani naye akiwa ni muumini, basi Qur'ani itachanganyika na nyama na damu yake na Mwenyezi Mungu atamfanya kuwa pamoja na watukufu na wema. Na Qur'ani itakuwa kwake mtetezi siku ya Kiyama. Itasema: Ewe Mola wangu hakika kila mtendaji amepata ujira wa matendo yake ispokuwa aliyenishughulikia, hivyo mkirimu kwa malipo yaliyo bora. Kisha Mwenyezi Mungu Mtukufu mtenza nguvu, atamvisha mavazi mawili miongoni mwa mavazi ya peponi, na kutawekwa kichwani kwake taji takatifu, kisha atasema kuiambia je, tumekuridhisha ndani yake (kwa malipo ya huyu mtu?) kisha Qur'ani itasema: "Ewe Mola wangu nilikuwa ninamtakia yaliyo bora zaidi ya haya. Anasema (as), basi atapewa amani upande wake wa kulia na kubakia milele upande wake wa kushoto, kisha ataingia peponi na ataambiwa soma aya upande daraja, kisha ataambiwa, je tumekutosheleza kwa hayo na kukuridhisha? Itasema, ndio.[٣] "

10–Ulazima wa kuwafundisha watoto Qur'ani

Imepokelewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) katika hadithi akisema: "Watavishwa wazazi wake– yaani wazazi wa aliyehifadhi Qur'ani, mavazi mawili iwapo watakuwa waumini kisha wataambiwa, haya ni malipo ya mliyomfundisha Qur'ani".[٣] Na katika hadithi nyingine iliyopokelewa kutoka kwa Amirul–Muuminina Ali (a.s) imesema: "Hakika Mwenyezi Mungu hajali kuwaadhibu watu wote wa ardhini hata asiepukwe kati yao yeyote iwapo watafanya maasi na watatenda makosa. Lakini anapowaangalia wazee wakiielekeza miguu yao

---

[٣] Jaamiul-Ahaadithush-Shia, Kiatabus-Swalat, Abewaabu Ziyaaratul-Qubuur, mlango wa 2, na humu kuna makumi ya hadithi.

[٣] Al-Kaafi juzu ya 2 ukurasa wa 604.

[٣] Nahajuls-Saadah juzu ya 7 ukurasa wa 223.

kuelekea kwenye swala, na watoto wakijifundisha Qur'ani, huwarehemu na kuwacheleweshea (adhabu)".[٣٤]

11–Aina za wasomi wa Qur'ani na sifa ya msomi wa kweli

Imepokelewa kutoka kwa Abu Ja'far (a.s) amesema: "Wasomaji wamegawanyika sehemu tatu; mtu aliyesoma Qur'ani akaichukulia kuwa ni bidhaa akajikaribisha kwayo kwa wafalme na akapata umashuhuri kwa watu, na mtu aliyesoma Qur'ani akahifadhi herufi zake lakini akapoteza sheria zake[٣٥] na akaichukulia kwa namna mbaya, basi Mwenyezi Mungu asiwajaalie hao kuwa wabebaji wa Qur'ani, na mtu ambaye aliisoma Qur'ani akaweka ponyo ya Qur'ani juu ya ponyo la moyo wake, akakesha usiku na akashinda nayo mchana wake, akaidumisha katika maeneo ya ibada, kwa watu hao Mwenyezi Mungu huondoa balaa na kwa wao Mwenyezi Mungu huwashinda maadui na kwa wao Mwenyezi Mungu huteremsha mvua kutoka mbinguni. Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu! Wasomi hao wa Qur'ani ni watakatifu kuliko (madini) ya kibiriti nyekundu".[٣٦]

Na imepokewa kutoka kwa Mtume Muhammad (saw) amesema: "Ewe uliyebeba Qur'ani (uliyehifadhi) kuwa mnyenyekevu kwake Mwenyezi Mungu atakuinua. Usijitweze kwake Mwenyezi Mungu akakudhalilisha. Ewe uliyebeba Qur'ani jipambe nayo kwa Mwenyezi Mungu, naye atakupamba kwayo. Na usijipambe nayo kwa watu akakuchafua nayo Mwenyezi Mungu".[٣٧]

12–Kuifahamu Qur'ani ni daraja iliyo karibu na utume

---

[٣٤] Wasaailush-Shia, Kitabus-Swalaat Abewabu Ahkamul-Masaajid, mlango wa 3 hadithi ya 3.

[٣٥] Nao ni wale ambao wanafuatilia sana sheria za tajweed walizoziweka wao, na wakasahau maana ya kile wanachokisema.

[٣٦] Wasaailush-Shia, Kitabus-Swalaat Abewabu Qurraul-Qur'ani walau fii ghairis-Swalaat, mlaango wa 8 hadithi ya 1-3.

[٣٧] Dalili iliyotangulia, mlango wa 11 hadithi ya 18.

Imepokelewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akisema: "Atakayehitimisha Qur'ani, basi atakuwa amepiga hatua za Utume kati ya pande zake, ispokuwa tu hashushiwi wahyi".[٣] [١]

13-Njia kamilifu kwa wasomaji wa Qur'ani, waanze mwanzo wake hadi mwisho wake na sio kusoma sura tofauti.

Imepokewa kutoka kwa Al-Zuhri amesema: "NIlisema kumwambia Ali bin Hussein (a.s), ni matendo gani yaliyo bora? Akasema; (Muhitimishaji muanzishaji) nikasema, na ni nini maana ya Muhitimishaji muanzishaji, akasema (a.s), anayeifungua Qur'ani na kuihitimisha, kila atakapoanzia mwanzo wake, anakwenda hadi mwisho wake.[٣] Na mwishoni akaulizwa; ni matendo gani yaliyobora akasema: ni (Muhitimishaji muanzishaji) ikasema, ni nani huyo? Akasema; Muhitimishaji muanzishaji, ni yule ambaye anahitimisha Qur'ani kwa kuisoma kisha anaanza usomaji mwanzoni mwake. Alimfananisha na msafiri anayefika nyumbani akakaa hapo kisha akaanzisha upya safari nyingine yaani anaianzisha. Na kadhalika kisomo cha watu wa Makkah wanapohitimisha Qur'ani kwa kisomo huanza (tena) wakasoma Al-Fatiha na aya tano za mwanzo wa surat Al-Baqarah hadi kauli ya Allah inayosema; (hao ndo waliofaulu.) Kisha wanasimama na kumtaja anayefanya hivyo kuwa ni muhitimishaji muanzishaji, yaani kwamba anahitimisha Qur'ani na akaanza tena mwanzo wake bila kutenganisha muda mrefu".

Na kwa maana ya hadithi hiyo imepokewa kutoka kwa Imam Swadiq (a.s) akisema: "Ikasemwa ewe mwana wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, ni watu gani wabora? Akasema (a.s) ni (Muhitimishaji muanzishaji), ikasemwa ewe mwana wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) ni nani huyo muhitimishaji muanzishaji? Akasema (a.s); muanzishaji na muhitimishaji ni ambaye anasoma Qur'ani na

---

٣١٠.

٣١١Dalili iliyotangulia, mlango wa 11, hadithi ya 2.

anaihitimisha, huyo atakuwa na maombi yenye kupokelewa mbele ya Mwenyezi Mungu".[٣]

14–Usia kwa kukithirisha kuisoma Qur'ani

Na katika usia wa Mtume (saw) kwa Ali (a.s) alisema: "Jibidishe kusoma Qur'ani katika hali yoyote".[٣]

15–Thawabu za kusoma Qur'ani

Imepokewa kutoka kwa Imam Swadiq (a.s) akisema: "Jibidisheni kusoma Qur'ani hakika daraja za pepo ziko kwenye idadi ya aya za Qur'ani. Itakapokuwa siku ya Kiama itaambiwa msomaji wa Qur'ani, soma na upande daraja, kila anaposoma aya, anapanda daraja".[٣]

Na imepokewa kutoka kwa Abu Ja'far (a.s) amesema: "Alisema Mtume (saw); atakayesoma aya 10 usiku, hatoandikwa miongoni mwa wasahaulifu. Na atakayesoma aya 50 ataandikwa ni miongoni mwa wakumbukaji. Na atakayesoma aya 100 ataandikwa miongoni mwa watiifu. Na atakayesoma aya 200 ataandikwa miongoni mwa wanyenyekevu. Na atakayesoma aya 300 ataandikwa miongoni mwa waliofaulu. Na atakayesoma aya 500 ataandikwa miongoni mwa wenye kujitahidi. Na atakayesoma aya 1000 ataandikiwa fungu, na fungu la uzito wa elfu 15 (au elfu 50) la dhahabu. Uzito wa fungu la elfu 24, uchache wake unalingana na mlima wa Uhud na zaidi yake ni kati ya mbingu na ardhi".[٣]

16–Umuhimu wa kuhifadhi yale unayojifundisha katika Qur'ani na asiache kwa kiasi cha kusahau

Imepokelewa hadithi kutoka kwa Ya'qub Al-Ahmar amesema: "Nilisema kumwambia Abu Abdillah (a.s), nina dinar nyingi na nimeingiwa na kitu ambacho kimekaribia kuifanya Qur'ani iniondoke. Akasema Abu Abdillah (a.s); Qur'ani

---

[٣] Dalili iliyotangulia, hadithi ya 8.

[٣] Dalili iliyotangulia, mlango wa 11, hadithi ya 1.

[٣] Dalili iliyotangulia, hadithi ya 10.

[٣] Dalili iliyotangulia, mlango wa 17, hadithi ya 2.

Qur'ani, hakika aya za Qur'ani na sura zitakuja siku ya Kiama hadi zitapanda daraja 1000-yaani peponi- na zitasema; lau kama ungenihifadhi ningekufikisha hapa".[٣]

Nami nasema kwamba, huko nyuma ulitangulia kusoma kwamba kuhifadhi Qur'ani kimaanawi, kuna maana ya kuchunga mipaka na maana zake sambamba na kuzingatia maamrisho na makatazo yake.

17-Suna ya kusoma Qur'ani ukiwa na udhu

Imepokewa kutoka kwa Muhammad Ibn Al-Fudhail kutoka kwa Abul-Hassan (a.s) amesema: "NIlimuuliza (kwamba) huwa ninasoma msahafu kisha natokwa na haja ndogo kisha ninasimama na kujisaidia haja ndogo, kujisafisha na kuosha mikono, halafu ninarudi kwenye msahafu na kusoma ndani yake? Akasema; hapana (utatawadha) hadi pale ukiwa unasali.[٣] " na kutoka kwao (Maimamu ١ watoharifu-as) wamesema: "Msomaji wa Qur'ani ana malipo ya mema 100 kwa kila herufi atakayoisoma katika swala akiwa amesimama, na mema 50 akiwa amekaa na mema 25 akiwa na tohara katika swala zisizo (swala) tano, na mema 10 iwapo hatokuwa na tohara." Lakini mimi nasema; kusoma herufi za Alif, Lam, Mim, Ra utapata thawabu 10 kwa Ali, 10 kwa lam, 10 kwa Mim na 10 kwa Ra.[٣]

18-Suna ya kujitenga mbali na shetani wakati wa kusoma Qur'ani

Imeokewa kutoka kwa Al-Halabi kutoka kwa Abu Abdillah (a.s) akisema: "NIlimuuliza kuhusu kujitenga mbali na shetani wakati wa kusoma kila sura itakayoanziwa. Akasema; ndio, utajikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kutokana na shetani mlaaniwa.[٣] " ١

Na imepokelewa kutoka kwa Amirul-Muminina Imamu Ali (a.s) amesema: "Na kujitenga mbali (na shetani) ni vile ambavyo Mwenyezi Mungu amewaamrisha waja wake wakati wa kusoma kwao Qur'ani, kwa kusema: (Na ukisoma Qur'ani

---

٣١٥. Dalili iliyotangulia, mlango wa 12, hadithi ya 3.

٣١٧. Dalili iliyotangulia, mlango wa 13, hadithi ya 1.

٣١٨. Dalili iliyotangulia hadithi ya 3.

٣١٩. Dalili iliyotangulia, mlango wa 14, hadithi ya 2.

Muombe Mwenyezi Mungu akulinde na shetani aliyelaaniwa.). Hivyo atakayejifunza desturi hii kwa ajili ya Mwenyezi Mungu itampelekea kufaulu milele.[٣] ”

19–Qur’ani ni ahadi ya Mwenyezi Mungu, ni mara ngapi Mwislamu anatakiwa kuisoma kwa siku

Imepokewa kutoka kwa Abu Abdillah (a.s) amesema: “Qur’ani ni ahadi ya Mwenyezi Mungu kwa viumbe wake, hivyo inatakiwa kwa Mwislamu kuangalia katika ahadi yake na asome aya 50 kwa kila siku.[٣] ”

Mimi ninasema; kwa mahesabu mepesi inapatikana natija kwamba kiwango kidogo anachotakiwa muumini kuhitimisha Qur’ani kwa mwaka ni mara tatu. Kwa kuwa idadi ya aya za Qur’ani ni zaidi ya 6000 ambazo atazigawa kwa siku 120, yaani kwa kila baada ya miezi minne, kwa kufumbia macho juhudi zaidi za mwezi wa Ramadhani.

20–Aya za Qur’ani ni hazina hivyo nufaika nazo zote

Imepokewa kutoka kwa Ali Bin Hussein (a.s) akisema: “Aya za Qur’ani ni hazina, (hivyo) kila unapofungua hazina, unatakiwa uangalie yaliyo ndani yake.[٣] ”

21–Suna ya kusoma Qur’ani majumbani

Imepokewa kutoka kwa Abu Abdillah (a.s) akisema: alisema Amirul–Muuminina Ali (a.s) kwamba: “Nyumba ambayo husomwa Qur’ani ndani yake na anatajwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani yake, huzidi baraka zake na hutembelewa na malaika na kukimbiwa na shetani. Huwaangazia watu wa mbinguni kama vile nyota zinavyowamulikia watu wa dunia. Na nyumba ambayo haisomwi Qur’ani ndani yake na hatajwi Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani yake,

---

[٣٤] Dalili iliyotangulia, hadithi ya 1.

[٣٥] Dalili iliyotangulia, mlango wa 15, hadithi ya 1.

[٣٦] Dalili iliyotangulia, hadithi ya 6.

huwa na baraka kidogo na hukimbiwa na malaika na kutembelewa na mashetani.[٣] ”

22–Kupata na kutafuta rizki, hakumzuii mtu kuzingatia usomaji wa Qur’ani

Imepokewa kutoka kwa Abu Abdilla- (a.s) amesema: “Hazuiwi mfanyabiashara kati yenu anayejishughulisha sokoni, wakati anaporejea nyumbani kwake asilale hadi atakaposoma sura katika Qur’ani, basi huandikiwa mema 10 kwa kila mahala pa aya anayoisoma na kufutiwa machafu 10.[٣] ”

23–Suna ya kusoma kwenye Msahafu, hata kama (msomaji) amehifadhi yale anayoyasoma

Imepokewa kutoka kwa Abu Abdilllah (a.s) akisema: “Atakayesoma Qur’ani katika msahafu, hustarehesha macho yake na wazazi wake wanapunguziwa dhambi hata kama watakuwa makafiri.[٣] ”

Na kutoka kwa Mtume (saw) amesema: “Hakuna kitu kinamuweza uzito shetani kama mtu kusoma katika Msahafu akitazama.[٣] ”

Na katika hadithi nyingine anasema: “Kutazama kwenye msahafu (hata) bila ya kusoma, ni ibada.[٣] ”

Ninasema: na huu ni wadhifa mdogo anaotakiwa kuufanya yule asiyeweza kusoma Qur’ani, lakini tofauti na hapo anatakiwa kusikiliza. Na imepokewa kutoka kwa Is’haq Ibn Ammar kutoka kwa Abu Abdillah (a.s) amesema: “Nilimwambia, niwe fidia kwako, mimi nimehifadhi Qur’ani juu ya mgongo wa moyo wangu, je kuisoma juu ya mgongo wa moyo wangu ni bora au kuangalia kwenye Msahafu?

---

[٣٢٤] Dalili iliyotangulia, mlango wa 16, hadithi ya 2.

[٣٢٥] Dalili iliyotangulia, mlango wa 11, hadithi ya 6.

[٣٢٦] Dalili iliyotangulia, mlango wa 19, hadithi ya 1.

[٣٢٧] Dalili iliyotagulia, hadithi ya 2.

[٣٢٨] Dalili iliyotangulia, hadithi ya 6.

Akasema kuniambia: bali ukiisoma kwa kuangalia kwenye Msahafu ndio bora. Je hujapata kusikia kwamba kuangalia kwenye Msahafu ni ibada?[٣٢] ”

24–Suna ya kuwa na nakala ya Msahafu ndani ya nyumba

Kutoka kwa Imam Swadiq (a.s) amesema; “Inanivutia kuwepo Msahafu ndani ya nyumba, ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu anawafukuzia mashetani.[٣٣] ”

25–Suna ya kusoma taratibu na karaka kusoma kwa harakaharaka

Imepokewa kutoka kwa Abdullah Bin Sulaiman amesema: “Nilimuuliza Aba Abdillah (a.s) kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu unayosema (Na soma Qur’ani taratibu) akasema; amesema Amirul-Muuminina (Ali-as) kwamba; aliibainisha kwa uwazi, wala usiiharakishe mithili ya shairi wala kuisoma kwa vina vilivyoparaganyika, lakini ziamsheni kwayo (Qur’ani) nyoyo yenu migumu, na isijekuwa huzuni ya mmoja wenu mwishoni mwa sura.[٣٤] ”

Na katika tafsiri ya kauli ya Mwenyezi Mungu inayosema: (Wale tuliowapa kitabu, wakakisoma kama ipasavyo kusomwa….) imepokewa kutoka kwa Imam Swadiq (a.s) kwamba: usomaji wa kweli ni kusimama (kidogo) wakati kunapotajwa pepo na moto, akaomba dua sehemu ya kwanza (pepo) na kujiepusha sehemu nyingine (moto).[٣٥] ”

Na katika hadithi nyingine kutoka kwa Imam Swadiq (a.s) amesema: “Hakika Qur’ani haisomwi harakaharaka, bali inasomwa taratibu, na unapopita kwenye aya inayozungumzia pepo, simama kwenye aya hiyo na umuombe pepo Mwenyezi Mungu, na unapopita kwenye aya inayozungumzia moto, simama kwenye aya hiyo na umuombe Mwenyezi Mungu akuepushe na moto.[٣٦] ”

---

[٣٢] Dalili iliyotangulia, mlango wa 19, hadithi ya 4.

[٣٣] Dalili iliyotangulia, mlango wa 20, hadithi ya 1.

[٣٤] Dalili iliyotangulia, mlango wa 21, hadithi ya 1.

[٣٥] Dalili iliyotangulia, mlango wa 27, hadithi ya 7.

[٣٦] Dalili iliyotangulia, hadithi ya 3.

26–Suna ya kuisoma kwa huzuni kama vile inamuhutubu mwanadamu na kuheshimu wanayoyafanya watu wa jamii ya Sufiyah kwa kuzimia

Imepokewa kutoka kwa Imam Swadiq (a.s) akisema: "Hakika Qur'ani ilishuka kwa huzuni, hivyo isome kwa huzuni.[٣] " Na kutoka kwa Hafs amesema: "Sikuona mtu mwenye hofu kubwa kwa nafsi yake kama (Imam) Musa Ibn Ja'far (a.s) wala mtu mwenye kutaraji (pepo) kama yeye. Kisomo chake kilikuwa cha huzuni, na anaposoma ni kama vile anamuhutubu mwanadamu.[٣] " ٣

Na kutoka kwa Jabir kutoka kwa Abu Ja'far (a.s) amesema: "Nilisema, (kuna) watu wanaposoma sehemu ya Qur'ani au wanapoizungumzia baadhi yao huzimia kiasi kwamba lau mmoja wao akikatwa mkono au mguu wake hawezi kuhisi (uchungu wake), akasema; subhanallah! Ni watu gani hawa, hakika hali hiyo ni ulaini, wepesi, kutokwa na machozi na hofu.[٣] " ٣

27–Suna ya kuinua sauti wakati wa kusoma Qur'ani

Imepokewa kutoka kwa Muawiyah Bin Ammar akisema: "Nilisema kumwambia Abu Abdillah (a.s); (kuna) mtu anayeona kuwa hajafanya chochote katika dua na katika kisomo hadi ainue sauti, akasema; hakuna ubaya. Hakika Ali Ibn Hussein (a.s) alikuwa ana sauti nzuri (sana) katika kusoma Qur'ani na alikuwa akiinua sauti yake hadi wanamsikia watu wa nyumbani kwake. Naye Abu Ja'far (a.s) alikuwa ana sauti nzuri (sa) katika kusoma Qur'ani n alikuwa anaposimama (katika swala) ya usiku na akasoma Qur'ani, huinua sauti yake (kiasi kwamba) mtu aliyepita njiani miongoni mwa wenye kuomba maji na wengineo, walikuwa wanasimama na kusikiliza kisomo chake.[٣] " ٣

28–Uharamu wa kusoma Qur'ani kwa sauti mbaya

---

٣٣٢. Dalili iliyotangulia, mlango wa 22, hadithi ya 1.

٣٣٣. Dalili iliyotangulia, hadithi ya 3.

٣٣٤. Dalili iliyotangulia, mlango wa 25, hadithi ya 1

٣٣٥. Dalili iliyotangulia, mlango wa 23, hadithi ya 2.

Kutoka kwa Abu Abdillah (a.s) amesema: "Alisema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw); someni Qur'ani kwa mahadhi ya Kiarabu na sauti zake. Na ole wenu na kusoma kwa mahadhi ya watu wa ufuska na watu wa madhambi makubwa, kwani baada yangu watakuja watu watakuwa wanaikariri Qur'ani mithili ya nyimbo, makelele na sauti za vilio, lakini Qur'ani haitapanda kufika mioyo yao iliyopinduka na hata mioyo ya wafuasi wao.[٣] "[٣]

29–Wajibu wa kunyamanza kwa ajili ya kisomo cha Qur'ani, kiakhlaqi na suna, ispokuwa kwenye swala

Imepokewa kutoka kwa Abu Abdillah Ibn Abi Ya'fur kutoka kwa Abu Abdillah (a.s) amesema: "Nilimwambia, (kuna) mtu anasoma Qur'ani, je ni lazima kwa anayemsikiliza kusalia kimya na kuisikiliza? Akasema, ndio! Itakaposomwa Qur'ani karibu yako ni lazima unyamanze na kuisikiliza.[٣] "

Na katika hadithi ya Zurarah kutoka kwa Abu Ja'far (a.s) amesema: "Itakaposomwa Qur'ani katika swala ya faradhi nyuma ya imam, isikilizeni na msalie kimya, ili mrehemewe.[٣] "[٣]

30–Ni suna kuhitimisha Qur'ani mara moja ndani ya kila mwezi

Imepokewa kutoka kwa Muhammad Ibn Abdillah amesema: "Nilimwambia Abu Abdillah (a.s) kwamba; Nisome Qur'ani usiku? Akasema (sipendelei uisome katika muda ulio chini ya mwezi.[٣])"[٤]

31–Ni suna kutoa thawabu za kisomo kwa Maasumina (a.s) ili kuzidisha malipo

Imepokewa kutoka kwa Ali Ibn Al-Mughira kutoka kwa Abul-Hassan (a.s) kwamba: "Nilisema inapofika siku ya (Idi) Al-Fitri huwa ninahitimisha Qur'ani

---

[٣٣٧] Dalili iliyotangulia, mlango wa 24, hadithi ya 1.

[٣٣٨] Dalili iliyotangulia, mlango wa 26, hadithi ya 4.

[٣٣٩] Dalili iliyotangulia, hadithi ya 4.

[٣٤٠] Dalili iliyotangulia, mlango wa 27, hadithi ya 1.

kwa ajili ya Mtume[٣] (saw), na Ali (a.s), na Fatwimah (a.s) kisha kwa maimamu (a.s) hadi ninapomalizia kwako…. Ni hali gani hiyo inayonipata? Akasema; ni vyema kwako uwe nao (maasumina) siku ya Kiama. Nikasema, Mwenyezi Mungu ni Mkubwa, hivi kweli ninastahiki haya? Akasema; ndio mara tatu.[٣] "

32–Ni suna kulia au kujiliza wakati wa kusikiliza Qur'ani

Imepokewa kutoka kwa Imam Swadiq (a.s) amesema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu aliwajia vijana wa kabila la Answar akasema: ninataka nikusomeeni (Qur'ani) atakayelia basi atalipwa pepo. Akasoma sehemu ya mwisho wa surat Zumar inayosema: (Na waliokufuru wataongozwa kuelekea Jahannamu kwa makundi…..) Hadi mwisho wa sura hiyo, vijana wale wakalia wote ispokuwa kijana mmoja. Akasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu nimejililisha lakini macho yangu hayakutoa machozi. Mtume akasema: mimi nitarejea tena (kusoma), (hivyo) atakayejiliza basi ataingia peponi, akarejea tena kusoma, wakalia watu wote na yule kijana akajililisha, (hivyo) wakawa wameingia wote peponi.[٣] "

33–Elimu yote imo ndani ya Qur'ani

Imepokewa kutoka kwa Imam Ali (a.s) kwamba aliambiwa: "Je mnacho chochote katika wahyi? Akasema: hapana, ninaapa kwa yule aliyepasua mbegu na akaumba viumbe, ispokuwa Mwenyezi humpa (wahyi) mja mwenye uelewa katika kitabu chake.[٣] " [٤]

Imepokewa kutoka kwa Ibrahim Ibn Abbas amesema: "Sikuwahi kumuona Imam Ridha (a.s) akiulizwa kitu chochote ispokuwa alikuwa anajua elimu yake. Na sikuona mtu mwenye uelewa zaidi yake wa vitu vilivyokuwa zama za mwanzoni hadi katika zama na kipindi chake. Na Ma'mun alikuwa akimjaribu kwa maswali kuhusu kila jambo na alikuwa akimjibu. Na maneno yake yote, majibu na

---

[٣] Miongoni mwa aliyoyasoma ndani ya mwezi wa Ramadhan.

[٤] Dalili iliyotangulia, mlango wa 28, hadithi ya 1.

[٥] Dalili iliyotangulia, mlango wa 29, hadithi ya 1.

[٦] Tafsiru al-Swafi juzu ya 1 ukurasa wa 39.

mifano vilikuwa vinatokana na Qur'ani.[٣] " Na katika kitabu cha Nahjul-Balaghah imepokewa kwamba: "Hiyo ndio Qur'ani zungumzisheni, haitozungumza, ninakuelezeni kuihusu (hiyo Qur'ani), Ndio! Hakika ndani yake kuna elimu za yajayo na hadithi za waliopita na tiba ya maradhi yenu na mpingilio kati yenu.[٣] "

34–Qur'ani ni tiba kwa kila ugonjwa

Imepokewa kutoka kwa Abu Abdillah (a.s) amesema: "Lau kama utasoma Al-Hamdu kwa maiti mara sabini kisha akarejeshwa roho (uhai) haitakuwa kitu cha kushangaza.[٣] "

35–Ndani ya Qur'ani kuna usafishaji wa mioyo

Imepokewa kutoka kwa Mtume (saw) akisema: "Hakika hii mioyo hupata kutu kama vile chuma kinavyopata kutu, na kuzitakatisha, ni kusoma Qur'ani.[٣] "

36–Kuzidisha kuisoma ndani ya mwezi wa Ramadhani

Imepokewa kutoka kwa Abu Ja'far (a.s) amesema: "Kila kitu kina msimu, na msimu wa Qur'ani ni mwezi wa Ramadhani.[٣] "

Na imepokewa kutoka kwa Ali Ibn Hamzah amesema: "NIliingia kwa Abu Abdillah (a.s) Abu Basir akamwambi: niwe fidia yako, nisome Qur'ani (mara moja) ndani ya Ramadhani usiku? Akasema: hapana. Akasema, (kwa) nyusiku mbili? Akasema: hapana. Akasema: (kwa) nyusiku tatu? Akaashiria kwenye mkono wake kisha akasema: ewe Aba Muhammad hakika Ramadhani ina haki na heshima hailingani chochote na miezi mingine.[٣] "

37–Kusoma Qur'ani kufanyike ipasavyo

---

[٣٤٥] Dalili iliyotangulia, mlango wa 27, hadithi ya 6.

[٣٤٦] Hotuba ya 158 katika juzu ya kwanza.

[٣٤٧] Al-Kafi juzu ya 2 ukurasa 624.

[٣٤٨] Irshaadul-Quluub ukurasa wa 78.

[٣٤٩] Thawaabul-A'maal juzu ya 1 ukurasa 129, mlango wa thawabu za kusoma Qur'ani.

[٣٥٠] Wasaailush-Shia, Kitabus-Swalat, Abewaabu Qiraatul-Qur'ani fii Ghairis-Swalaat, mlango wa 27, hadithi ya 3.

Katika tafsiri ya Mwenyezi Mungu inayosema: "Wale tuliowapa Kitabu wakakisoma ipasavyo…Surat Baqara aya ya 121. Amesema Imam Swadiq (a.s): Wanasoma taratibu aya zake, wanaelewa na wanafahamu hukumu zake, na wanataraji ahadi zake (njema) na wanaogopa indhari zake huku wakizingatia visa vyake. Na wanaamrishika kwa amri zake na wanakatazika kwa makatazo yake, Wallahi sio kuhifadhi aya zake na kutalii herufi zake na kusoma sura zake, wala kutalii mafungu na khumusi zake. Kwa kuhifadhi herufi zake na wakapoteza sheria zake, bali ni kuzingatia aya zake na kutekeleza hukumu zake kama Mwenyezi Mungu alivyosema: (Hiki Kitabu tumekuteremshia wewe, kimebarikiwa, ili wazingatie aya zake…[٣] "

38–Maulama hawaishibi Qur'ani

Imepokewa kutoka kwa Mtume (saw) amesema katika hadithi inayozungumzia Qur'ani kwamba: "Ni kamba imara ya Mwenyezi Mungu, ni ukumbusho thabiti, njia iliyo nyoka nayo ndio ambayo haipotei kwayo mioyo na hawaishibi maulama na ndimi hazihitilafiani kwayo…Na hayaishi maajabu yake, atakayeizungumzia mwamini na atakayehukumu kwayo (Qur'ani) atapatia atakayeifanyia kazi atalipwa na atakayelingania (watu) kwenye Qur'ani) ataongozwa kwenye njia iliyo nyooka.[٣] "

39–Qur'ani katika Nahajul–Balaghah

Inasema: "Jifundisheni Qur'ani kwani yenyewe ni hadithi bora, na jielimisheni ndani yake kwani yenyewe ni msimu wa mioyo, na jiponyeni kwa nuru yake kwani yenyewe ni ponyo ya mioyo na isomeni vizuri hakika yenyewe ina visa vyenye manufaa. Na hakika mtendaji asiyefuata elimu yake (ya Qura'n) ni sawa na mjinga aliyetahayari ambaye hazinduki kutoka katika ujinga wake, bali hoja juu yake

---

٣٤ Mizanul Fi Tafsiril-Qur'ani juzu ya 1 ukurasa wa 260.

٣٥ Sunanud-Darimi juzu ya 2 ukurasa wa 435, kitabu cha fadhila za Qur'ani, na mfano wake katika vitabu maalumu.

itakuwa kubwa na hasara yake haiepukiki naye atalaumiwa kwa Mwenyezi Mungu.[٣] ”

40–Dua ya Imam Sajjad (a.s) wakati wa kuhitimisha Qur’ani

اللهم إنك أعنتني على ختم كتابك الذي أنزلته نوراً وجعلته مهيمناً على كل كتاب أنزلته وفضلته على كل حديث قصصته وفرقاناً فرقت بين حلالك وحرامك وقرآناً أعربت به عن شرايع أحكامك وكتاباً فصّلته لعبادك تفصيلاً.

Ewe Mola wangu! Hakika umenisaidia kuhitimisha Kitabu chako ambacho ulikiteremsha kuwa ni nuru na umekifanya mlinzi wa kila kitabu ulichokiteremsha. Na umekiboresha juu ya kila hadithi uliyoisimulia. Na ni kitenganishi kwacho umetenganisha kati ya halali yako na haramu yako. Qur’ani ambayo kwayo umeiweka wazi sheria ya hukumu yako. Kitabu umekipambanuwa kwa waja wako upambanuzi wa wazi.

ووحياً أنزلته على نبيك محمد صلواتك عليه وآله تنزيلاً وجعلته نوراً نهتدي من ظلم الضلالة والجهالة باتباعه وشفاء لمن أنصت بفهم التصديق إلى استماعه وميزان قسط لا يحيف عن الحق لسانه، ونور هدى لا يطفأ عن الشاهدين برهانه وعلم نجاة لا يضل من أمَّ قصد سنته، ولا تنال أيدي الهلكات من تعلق بعروة عصمته،

Ni Wahyi ulio uteremsha uteremsho kwa Nabii wako Muhammad Rehma Zako zimfikie na ziwafikiye Aali zake. Umeifanya kuwa nuru ituongoze katika giza ya upotevu na ujinga kwa kuifuata. Kiponyesho kwa mwenye kuisikiliza kwa kuifahamu na kuisadiki. Ni mizani ya kiadilifu isiyopotoka ulimi wake na kuwa mbali na haki. Nuru ya uongofu ambayo Burhani yake haiwazimikii watizamaji wake. Na alama ya uokovu ambayo hapotei mwenye kufuata mafunzo yake. Wala haitomfikia mikono ya maangamizi mwenye kujiambatanisha na kishiko chake cha ulinzi.

اللهم فإذا أفدتنا المعونة على تلاوته، وسهلت حواسي ألسنتنا بحسن عبارته، فاجعلنا ممن يرعاه حق رعايته، ويدين لك باعتقاد التسليم لمحكم آياته، ويفزع إلى الإقرار بمتشابهه وموضحات بيّناته،

Ewe Mola wangu! kwa vile umetusaidia kuisoma. Na umeturahisishia ugumu wa ndimi zetu kwa uzuri wa ibara yake hivyo basi tufanye tuwe miongoni mwa

[٣] Nahajul-Balagha juzu ya 1 hotuba ya 110.

wanaoichunga haki ya kuichunga na wakutumikia kwa itikadi ya kusalimu amri ya aya zake zilizothabiti waombao kimbilio kwa kuzikubali zile aya mutashabih na zile ufafanuzi wake uko bayana.

اللهم إنك أنزلته على نبيك محمد صلى الله عليه وآله مجملاً، وألهمته علم عجائبه مكملاً وورثتنا علمه مفسراً وفضلتنا على من جهل علمه، وقويتنا عليه لترفعنا فوق من لم يطق حمله،

Ewe Mola wangu! Hakika wewe umeiteremsha kwa Nabii wako Muhammad Rehema za mungu zimfikiye yeye na Aali zake kwa ujumla. Na umeturithisha sisi Elimu yake tukiwa wafasiri. Na umetuboresha juu ya wasioijuwa elimu yake. Umetupa nguvu juu yake ili utunyanyuwe juu ya wasio weza kuibeba.

اللهم فكما جعلت قلوبنا له حملة وعرفتنا برحمتك شرفه وفضله، فصل على محمد الخطيب به، وعلى آله الخزّان له، واجعلنا ممن يعترف بأنه من عندك، حتى لا يعارضنا الشك في تصديقه، ولا يختلجنا الزيغ عن قصد طريقه،

Ewe Mola wangu! kama vile umezifanya nyoyo zetu kuwa zenye kuibeba. Na kwa rehema zako umetutambulisha utukufu na ubora wake. Basi msaliye Muhammad, muhubiri wake na Aali zake wahifadhi wa Qur'ani. Utujaalie kuwa miongoni mwa wanaotambuwa kuwa yatoka kwako. Ili isituzukiye shaka katika kuisadiki. Wala upotovu usitutikise na kututowa nje ya njia yake nyofu.

اللهم صلّ على محمد وآله واجعلنا ممن يعتصم بحبله، ويأوي من المتشابهات إلى حرز معقله، ويسكن في ظل جناحه، ويهتدي بضوء صباحه، ويقتدي بتبلج أسفاره، ويستصبح بمصباحه ولا يلتمس الهدى في غيره،

Ewe Mola wangu!, mswaliye Muhammad na Aali Zake. Na tujaaliye sisi kuwa miongoni mwa wanaoshikamana na kamba yako, na wakimbiliao kutoka kwenye aya mutashabihati kwenda kwenye ngome yake madhubuti na kuketi kwenye kivuli cha bawa lake, na aongokaye na mwanga wake wa asubuhi. Aongokaye na kuchomoza kwa mng'aro wake. Anamulika kwa taa yake. Wala hatafuti uongofu katika kitu kingine.

اللهم وكما نصبت به محمداً عَلَماً للدلالة عليك وأنهجت بآله سُبل الرضا إليك، فصلّ على محمد وآله، واجعل القرآن وسيلة لنا إلى اشرف منازل الكرامة، وسُلّماً نعرج فيه إلى محل السلامة وسبباً نجزي به النجاة في عرصة القيامة، وذريعة نقدم بها على نعيم دار المقامة،

Ewe Mola wangu! Kwa hiyo Qur'ani umemweka Muhammad kuwa alama ya kukujuwa wewe. Na kupitia Ahlul-Bayt wake umeweka wazi njia za ridhaa zako. Msaliye Muhammad na Aali Zake na ifanye Qur'ani kwetu kuwa njia za kwenye daraja la utukufu. Na iwe ngazi tuipandayo kwenda mahali pa salama. Na iwe sababu tutakayolipwa uokovu kwenye uwanja wa kiyama. Na njia ambayo kwayo tutazifikia neema za nyumba ya kudumu.

اللهم صل على محمد وآله، واحطط بالقرآن عنا ثقل الأوزار، وهب لنا حسن شمائل الإبرار، واقف بنا آثار الذين قاموا لك به آناء الليل وأطراف النهار، حتى تطهرنا من كل دنس بتطهيره، وتقفوا بنا آثار الذين استضاؤوا بنوره، ولم يلْههم الأمل عن العمل فيقطعهم بخدع غروره،

Ewe Mola wangu! Msaliye Muhammad na Aali Zake. Kwa Qur'ani tupunguziye uzito wa dhana utupe sifa njema za watu wema na tufanye tufate athari za waliosimama kwa ajili yako nyakati za usiku na mwisho wa mchana. Ili ututakase na kila uchafu kwa utakaso wake. Utufanye tufate athari ya walioangaza kwa nuru yake. Wala matumaini hayakuwa zuiya kutenda kazi iliyowatenga mbali kwa vitimbi vya udanganyifu wake.

اللهم صل على محمد وآله، واجعل القرآن لنا في ظلم الليالي مؤنساً، ومن نزعات الشيطان وخطرات الوساوس حارساً، ولأقدامنا عن نقلها إلى المعاصي حابساً، ولألسنتنا عن الخوض في الباطل من غير ما آفة مخرساً، ولجوارحنا عن اقتراف الآثام زاجراً، ولما طوت الغفلة عنا من تصفح الاعتبار ناشراً، حتى توصل إلى قلوبنا فهم عجائبه، وزواجرَ أمثاله التي ضعفت الجبال الرواسي على صلابتها عن احتماله،

Ewe Mola wangu! Ijaliye Qur'ani iwe yenyekutuliwaza katika kiza cha usiku. Na yenye kutuhifadhi na upotevu wa shetani na hatari ya wasiwasi. Na yenye kuzuiya nyayo zetu zisiende kwenye maasi. Na yenye kuzuiya ndimi zetu kuingia kwenye batili bila kupatwa na maradhi. Na yenye kukemea na kutuzuia viungo vyetu kutenda madhambi. Na yenye kutuzindua kutokana na yale yaliyotughafilisha kuzingatia. Ili uufikishe ufahamu wa maajabu yake kwenye nyoyo zetu. Na tuifahamu mifano ambayo majabali thabiti yalishindwa kuibeba kwa ugumu wake.

اللهم صل على محمد وآله وأدم بالقرآن صلاح ظاهرنا، واحجب به خطرات الوساوس عن صحة ضمائرنا واغسل به درن قلوبنا، وعلائق أوزارنا، واجمع به منتشر أمورنا وارو به في موقف العرض عليك ظمأ هواجرنا، واكسنا به حلل الأمان يوم الفزع الأكبر في نشورنا،

Ewe Mola wetu! Idumushe kheri ya dhahiri yetu kwa Qur'ani. Na kwayo izuiye hatari ya wasiwasi kwenye usalama wa dhamiri zetu, na uondoshe uchafu wa nyoyo zetu na vikwazo vya madhambi yetu kwa Qur'ani. Na kwayo uyakusanye mambo yetu yaliyo sambaratika, na utuondolee kiu katika kisimamo siku ya kuja kwako. Na utuvishe kwa Qur'ani mapambo ya Amani siku ya mfadhaiko mkubwa katika kufufuliwa kwetu.

اللهم صل على محمد وآله، واجبر بالقرآن خلتنا من عدم الإملاق، وسق به ألينا رغد العيش خصب سعة الأرزاق وجنبنا به الضرائب المذمومة، ومداني الأخلاق، واعصمنا به من هوة الكفر ودواعي النفاق، حتى يكون لنا في القيامة إلى رضوانك وجنانك قائداً، ولنا في الدنيا عن سخطك وتعدي حدودك ذائداً، ولما عندك بتحليل حلاله وتحريم حرامه شاهداً،

Ewe Mola wangu! Mrehemu Muhammad na Ali Zake. Rekebisha kwa Qur'ani upungufu wetu tusiwe mafakiri. Kwa Qur'ani tusukumiye maisha ya raha na wasaa wa riziki. Tuepushe kwayo na tabia mbaya na mwenendo duni. Tuhifadhi kwa Qur'ani tusiingiye ndani ya shimo la maangamizi kufuru na mwendo wa kinafiki. Ili iwe mwongozo uelekezao kwenye maridhawa yako na bustani zako siku ya kiyama. Na iwe kwetu mlinzi hapa duniani dhidi ya makasiriko yako na kukiuka mipaka yako. Na iwe kwa yale uliyonayo kwa kuhalalisha halali yake na kuharamisha haramu yake shahidi.

اللهم صل على محمد وآله، وهوّن بالقرآن عند الموت على أنفسنا كرب السياق وجهد الأنين، وترادف الحشارج، إذا بلغت النفوس التراقي[وَقِيلَ مَنْ رَاقٍ]، وتجلّى ملك الموت لقبضها من حجب الغيوب ورماها عن قوس المنايا بأسهم وحشة الفراق، وداف لها من دعاف مرارة الموت كأساً مسمومة المذاق، ودنا منا إلى الآخرة رحيل وانطلاق، وصارت الأعمال قلائد في الأعناق، وكانت القبور هي المأوى إلى ميقات يوم التلاق،

Ewe Mola wangu! Mrehemu Muhammad na Aali Zake na kwa Qur'ani urahisishe umauti nafsini mwetu wakati wa kufa. Na usumbufu wa kukokotwa (Roho) Uuguaji. Na taabu ya mauguzi, na mfuatano wa kutatarika. (Ifikapo roho kooni na itasemwa: Mganga ni nani?) Atajitokeza Malaika wa umauti ili aichukue toka nyuma ya pazia ya mambo yasiyojulikana. Na kuitupa toka upinde wa umauti

kwa mshale wa kuachwa peka na kuwa changanyiya sumu iuwayo kwenye kikombe chenye mwonjo wa sumu wakati msafara wa kuelekea akhera ukitusogelea. Kazi zitakuwa ukosi wa shingo makaburi yatakuwa ndio kimbilio mpaka wakati wa siku ya kukutana.

اللهم صل على محمد وآله، وبارك لنا في حلول دار البلى، وطول المقامة بين أطباق الثرى، واجعل القبور بعد فراق الدنيا خير منازلنا، وافسح لنا برحمتك في ضيق ملاحدنا، ولا تفضحنا في حاضر القيامة بموبقات آثامنا، وارحم بالقرآن في موقف العرض عليك ذلّ مقامنا، وثبت به عند اضطراب جسر جهنم يوم المجاز عليها زلل أقدامنا، ونجنا به من كل كرب يوم القيامة، وشدائد أهوال يوم الطامة وبيّض وجوهنا يوم تسود وجوه الظلمة في يوم الحسرة والندامة، واجعل لنا في صدور المؤمنين وداً، ولا تجعل الحياة علينا نكداً،

Ewe Mola wangu! Mrehemu Muhammad na Aali zake. Na utubariki wakati wa kuingia nyumba ya kuoza na makazi ya muda mrefu kati ya tabaka za udongo. Yajaaliye makaburi baada ya kuiaga dunia yawe mafikio yetu mema tupanulie mbano wa mwana ndani zetu kwa rehema zako. Usitufedheheshe mbele ya walio hudhudhiria siku ya Kiyama kwa sababu ya madhambi yetu ya angamizayo. Kwa Qur'ani irehemu hali yetu duni katika kikao cha kuletwa mbele yako. Kwa Qur'ani zithibitishe nyayo zetu zisiteleze wakati daraja la Jehannam litakapoyumba yumba. Kwayo ing'arishe giza ya makaburi yetu kabla ya kufufuka. Utuokowe kwa Qur'ani na kila taabu ya siku ya Kiyama na shida za kutisha siku ya maafa. Zing'arishe nyuso zetu siku ambayo nyuso za wadhalimu zitakuwa nyeusi siku ya kuhasirika na majuto. Utujaaliye upendo ndani ya nyoyo za waumini. Usiyafanye maisha kwetu kuwa ya shida.

اللهم صل على محمد عبدك ورسولك، كما بلغ رسالتك، وصدع بأمرك ونصح لعبادك . اللهم اجعل نبينا صلواتك عليه وعلى آله يوم القيامة أقرب النبيين منك مجلساً، وأمكنهم منك شفاعة، وأجلّهم عندك قدراً، وأوجههم عندك جاهاً،

Ewe Mola wangu! mrehemu Muhammad mja wako na mjumbe wako kwa vile ameifikisha risala yako na alitekeleza amri yako. Aliwanasihi waja wako. Ewe Mola wangu! Mjaaliye Nabii wetu Rehema Zako ziwe juu yake, na juu ya Aali zake - Awe karibu mno na wewe siku ya kiyama miongoni mwa Manabii watakaokuwa karibu ya kikao. Na mwenye uwezo mkubwa sana kwako wakuombea. Mwenye Enzi kubwa miongoni mwao kwako. Mwenye cheo kikubwa mno mbele yako.

اللهم صل على محمد وآل محمد، وشرّف بنيانه، وعظم برهانه، وثقل ميزانه، وتقبل شفاعته وقرب وسيلته، وبيض وجهه وأتم نوره وارفع درجته، وأحينا على سنته وتوفّنا على ملته، وخذ بنا منهاجه، واسلك بنا سبيله، واجعلنا من أهل طاعته، واحشرنا في زمرته، وأوردنا حوضه، واسقنا بكأسه، وصل اللهم على محمد وآله صلاة تبلغه بها أفضل ما يأمل من خيرك وفضلك وكرامتك إنك ذو رحمة واسعة وفضل كريم،

Ewe Mola wangu! Mrehemu Muhammad na Aali wa Muhammad. Itukuze nyumba yake, Bur'hani yake itukuze, Mizani yake ipe uzito, ya kubali maombezi yake usogeze karibu wasila wake, ufanye uwe mweupe uso wake, ikamilishe nuru yake iinue daraja yake. Tufanye sisi tuishi na sunna yake, tufishe tukiwa katika mila yake, tupeleke tufikishe kwenye njia yake. Tupitishe njia yake. Tujaaliye tuwe miongoni mwa watu watii wake. Tufufuwe katika kikundi chake tuelekeze kwenye dimbwi lake, tunyweshe kwa bilauri yake. Rehemu Muhammad na Aali zake. Rehema ambayo utamfikisha nayo kwenye ubora asio uwazia miongoni mwa kheri na fadhila zako, na heshima zako. Hakika wewe ni mwenye Rehma kubwa na fadhila tukufu

اللهم اجزه بما بلّغ من رسالاتك وأدّى من آياتك، ونصح لعبادتك، وجاهد في سبيلك، أفضل ما جزيت أحداً من ملائكتك المقربين، وأنبيائك المرسلين المصطفين، والسلام عليه وعلى آله الطاهرين ورحمة الله وبركاته

Ewe Mola wangu! mlipe kwa aliyoyafikisha katika jumbe zako. Na amefikisha aya zako, amepigana jihadi katika njia yako malipo yaliyo bora umepata kumlipa yeyote miongoni mwa Malaika wako wa karibu na Manabii wako walio Mursali wateule. Amani imfikie yeye na iwafikiye watoto wake watakatifu wema, na rehema za Mungu na baraka zake[٣] .

Kimeandikwa na:
Ayatollah, Sheikh Muhammad Yaqoobi

Kimetarjumiwa na:

[٣] Asw-Swahiifat As-Sajjadiyah, Dua yake pindi anahittmishapo Qur’ani.

Ustadhi, Abdallah Khamis Salum
Box, 113, Kalenge Kigoma Tanzania.